Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Pili - Tarehe 13 Aprili, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 16

**Kodi ya Majengo ya Udongo**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliamua kwa dhati kufuta kodi ya majengo kwa nyumba za udongo na kwa kuwa nyumba nyingi za Manispaa ya Mbeya yaani asilimia 75 zimejengwa kwa tofali mbichi:-

Je, Serikali inatoa ufafanuzi gani juu ya nyumba za aina hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuleta swali hili Bungeni ili lituwezeshe kuweza kutoa ufafanuzi zaidi juu ya suala hili ambalo limekuwa likileta utata kidogo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Serikali ilifuta baadhi ya kodi na ushuru uliokuwa unatozwa na Serikali za Mitaa. Uamuzi huu ulifuatiwa na marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 yaliyofanywa kupitia Sheria ya Fedha Na. 15 ya 2003 *(Finance Act No. 15*

*of 2003)* iliyopitishwa na Bunge lako Tkufu. Uamuzi huu ulitokana na sababu kubwa mbili zifuatazo:-

(a) Kuwapunguzia ugumu wa maisha wananchi wenye kipato kidogo ili waweze kutumia fursa hiyo ya Serikali kuondoa kodi na ushuru kujiongezea uwezo wa kupambana na umaskini.

(b) Kuwaondolea kero zinazojitokeza wakati wa kukusanya kodi na ushuru huo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, moja ya kodi iliyofutwa kwa kuzingatia maelezo niliyotoa hapo juu ni kodi ya majengo ya makazi ya tope *(mud-houses).* Baadhi ya majengo haya yamejengwa wa miti na udongo na mengine yamejengwa kwa matofali yasiyochomwa (mabichi) na yanapatikana katika sehemu mbalimbali za Miji yetu ikiwemo Mji wa Mbeya. Baadhi ya majengo haya pia yamo katika maeneo yaliyopimwa na mengine yako katika maeneo yasiyopimwa. Aidha, baadhi ya maeneo hayo yamejengwa siku za nyuma na watu wenye uwezo na mengine na watu wasio na uwezo wa fedha na haya mara nyingi yako katika hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya majengo yaliyopo katika Manispaa ya Mbeya ikiwemo *Mbeya Hotel* yamejengwa kwa matofali yasiyochomwa (mabichi). Ni dhahiri kwamba Serikali ilipokuwa inapitisha uamuzi wake haikuwa imedhamiria kusamehe kodi ya majengo kwa aina zote hizi za nyumba za udongo. Walengwa wakubwa wa uamuzi wa Serikali ni wananchi wenye kipato cha chini wanaomiliki nyumba hizo. Namna nzuri ya kubaini majengo yanayomilikiwa na wananchi wenye kipato cha chini ni kutumia utaratibu wa uthamini wa nyumba *(valuation roll).* Kufuatia zoezi la uthamini wa majengo uliofanyika katika Manispaa ya Mbeya, baadhi ya majengo haya yameonekana kuwa na thamani iliyo chini ambayo kodi yake ya majengo imewekwa kati ya shilingi elfu tatu hadi elfu tano kwa mwaka, kodi ambayo Serikali inaamini iko ndani ya uwezo wa wamilikaji wa majengo hayo. Majengo mengine mengi ambayo yameonekana kuwa na thamani ndogo sana kutokana na kujengwa na wananchi wenye uwezo mdogo hayatozwi kodi yoyote ya majengo na haya yanalingana na maamuzi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo isije ikaeleweka kwamba katika kusema hivi au kuamua hivi tunataka kuendeleza ujenzi wa nyumba zisizo bora katika Miji yetu. Naomba kusisitiza kwamba kwa mujibu wa Kanuni za Ujenzi Mijini, Sura ya 101 *(Township Buildings Rules Cap. 101),* ujenzi wa nyumba za aina hii hauruhusiwi katika Miji yetu. Kwa hiyo naomba kutoa rai kwa wananchi wote na hasa viongozi wa Halmashauri zetu kuendelea kuhimiza ujenzi wa nyumba zinazotakiwa kwa kufuata masharti ya kisheria yaliyopo. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kujua kwa sababu lengo la swali langu lilikuwa ni kuangalia hizi nyumba za maeneo ambayo

watu hawana uwezo kabisa. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutoa mwongozo ambao utaeleweka kabisa kwamba nyumba za namna hii zisilipiwe kabisa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mimi nadhani njia rahisi na nzuri zaidi ni kurudisha jukumu hili kwenye Halmashauri zinazohusika kwa sababu Halmashauri hizi ndio zinalea maeneo hayo na wanaweza kuwa katika nafasi nzuri sana za kuweza kuweka makundi mbalimbali ili kuweza kuondoa migogoro na mabishano yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, mimi napokea rai yake, tutashirikiana na wataalam pale ofisini tuone kama tunaweza kutoa mwongozo wa jumla kuhusiana na tafsiri ambayo tumeitoa hapa Bungeni kuhusiana na nyumba za tope.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Vitongoji vingine katika Miji yetu unakuta havipati huduma kabisa za Halmashauri na tayari vimeingizwa katika mpango huu wa kutozwa kodi mfano ni Kitongoji cha Chanji katika Mji wa Sumbawanga ambacho hakina nyumba nzuri na Vitongoji vingine hata katika Miji mikubwa ambayo unakuta Halmashauri wala hazijapima viwanja wala hazipeleki huduma zozote mfano Dar es Salaam eneo la ......

**SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuwatoza wananchi hizi kodi za majengo bila kuwapa huduma nayo inakuwa ni kero kubwa kwa kipindi hiki?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba yapo maeneo ambayo yapo kwenye maeneo ya mzunguko wa maeneo ambayo yapo katika maeneo ya Miji ambayo bado huduma zake si nzuri sana kwa ujumla wake. Kwa kweli sababu kubwa za kutaka kodi hizi ziendelee kutozwa kwa kiasi fulani ni katika kujaribu kutafuta fedha zinazoweza kuleta huduma bora katika maeneo hayo. Lakini kwa ujumla wake tunalikubali na ndio maana Serikali inaendelea kutoa ruzuku kwa Halmashauri zetu ili ziweze kutumia ruzuku hiyo kusaidia kuleta huduma bora katika maeneo yao yote.

Na. 17

**Mwongozo wa Uundaji wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI**

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa mujibu wa mwongozo wa uundaji wa Kamati za kudhibiti UKIMWI katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kila Halmashauri zimeagizwa kuunda Kamati ya Kudumu ya Kudhibiti UKIMWI na kila ngazi ya chini ya Halmashauri nayo

imetakiwa kuwa na Kamati Maalum ya Kudhibiti UKIMWI na kwa kuwa katika Muundo wa Kamati hizo hakuna mwakilishi wa Idara ya Afya, hata mwakilishi wa kukaribishwa:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kushirikisha wawakilishi wa Idara ya Afya katika Kamati hizo za Kudhibiti UKIMWI?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kutowashirikisha Idara ya Afya katika Kamati hizo ni kupunguza ufanisi katika utendaji wa Kamati hizo?

(c) Je, Serikali itakubali kuwa Idara ya Afya ni Idara muhimu na ya msingi katika kudhibiti UKIMWI na hivyo itakuwa tayari kurekebisha kasoro katika uwakilishi kwenye Kamati hizo ili kuweka mjumbe anayetoka katika Idara ya Afya katika Kamati hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetoa mwongozo wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI katika mamlaka za Serikali za Mitaa. Mwongozo huo umeainisha wajumbe watakaounda Kamati hizo katika ngazi mbalimbali kuanzia Kitongoji, Mtaa, Kijiji, Kata na Halmashauri zenyewe.

Kabla ya kutoa mwongozo Mratibu wa UKIMWI wa Halmashauri alikuwa ni Afisa kutoka Idara ya Afya. Kwa kuwa tatizo la UKIMWI limeonekana ni la kijamii au mtambuka na kwa kuwa sera na mkakati wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI zinaelekeza ushiriki wa sekta zote katika mapambano dhidi ya UKIMWI ilipendekezwa kwenye Mwongozo kwamba Mratibu wa UKIMWI awe ni Afisa kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa lengo la kuishirikisha jamii yote katika mapambano hayo. Hata hivyo baadhi ya Halmashauri zinaendelea kuwa na Waratibu wa UKIMWI kutoka Idara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, naomba tukubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa Idara ya Afya ina mchango mkubwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI na hasa yanapokuja masuala ya kitaalam kama upimaji wa damu, utoaji wa dawa za kurefusha maisha, ushauri nasaha na kadhalika. Kwa kutambua umuhimu wa Idara ya Afya tumeamua kuwe na co-opted members katika Kamati ya UKIMWI na wajumbe hao ni pamoja na wajumbe kutoka Idara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, katika marekebisho ambayo yatafanywa katika Mwongozo huo Idara ya Afya itakuwa na mwakilishi katika Kamati za Kudhibiti UKIMWI ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa Kamati hizo.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nina swali dogo tu la nyongeza. Pamoja na kuundwa kwa Kamati nyingi, pamoja na makongamano na warsha lakini bado inaonekana ugonjwa huu ni tatizo. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa umefika wakati muafaka kutafuta njia mbadala badala ya kuunda Kamati na makongamano?

**SPIKA:** Kama ipi hiyo mbadala? Atafikiria baadaye, basi na Waziri utajibu baadaye. *(Kicheko)*

Na. 18

**Sheria Iliyoanzisha *PSRC***

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria iliyoanzisha *PSRC (Public Corporation Amendment Act, 1993), Ibara* ya 39(2)(i), inaipa *PSRC* uwezo wa kujadili na kukamilisha Mikataba ya uuzaji au kuyakodisha mashirika na kwa kuwa sheria hiyo hiyo haitoi uwezo kwa *PSRC* wala kwa Wizara mama kufuatilia utekelezaji wa Mikataba iliyofikiwa kati ya *PSRC* na wawekezaji:-

(a) Je, ni nani mwenye dhamana ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mikataba hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa sheria hiyo ina upungufu, kwa hiyo inahitaji ifanyiwe marekebisho?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Khamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara Mama za Mashirika yanayobinafsishwa ndizo zenye dhamana za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mikataba ya ubinafsishaji na utendaji wa Mashirika yanayobinafsishwa. Wizara Mama katika kutekeleza jukumu hili zimeunda vitendo vya ufuatiliaji wa utendaji wa mashirika kwa mujibu wa Mikataba ya ubinafsishaji.

Aidha, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kama mratibu wa zoezi inapokea taarifa za Wizara za Kisekta na kuzichambua na hatimaye kuziwasilisha Serikalini kwa maamuzi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haioni kuwa sheria hiyo ina mapungufu isipokuwa mapungufu yamekuwa yakijitokeza katika kutekeleza baadhi ya Mikataba ya mashirika yanayobinafsishwa. Katika kupunguza baadhi ya matatizo kwa mashirika yanayobinafsishwa, mwaka 1999 Mheshimiwa Rais alitoa agizo la kuunda vitengo vya ufuatiliaji wa Mikataba hiyo Kiwizara na kila mwaka taarifa ya utekelezaji kwa mashirika yaliyobinafsishwa huwasilishwa Serikalini na hatimaye uamuzi kutolewa. Yapo mashirika ambayo Serikali imeshayatolea uamuzi na yapo mashirika ambayo yanafanyiwa kazi. Hili linaonekana wazi kutokana na taarifa mbalimbali na majibu ya hoja zinazojibiwa katika Bunge lako Tukufu.

Na. 19

**Fursa na Athari za Ushiriki wa Tanzania Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji imeshakamilisha zoezi la kubaini fursa na athari za ushiriki wa Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki:-

Je, ni fursa zipi na katika nyanja zipi zinaweza kutumiwa na Watanzania ili wafaidike na ushirikiano wa Jumuiya hiyo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwa Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Lengo la ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki ni kuharakisha maendeleo ya wananchi wa nchi hizi na kuimarisha uwezo wa Jumuiya wa kushiriki katika uchumi wa dunia. Kwa misingi ya lengo hili nchi wanachama wametia saini Itifaki ya Umoja wa Forodha ambayo utekelezaji wake ulianza tarehe 1 Januari, 2005. Ili Tanzania iweze kushiriki vizuri katika Jumuiya, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa kushirikiana na *Economic Research Bureau* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imefanya utafiti kubaini fursa na athari zinazojitokeza kwa Tanzania ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utafiti huu imebainika kuwa zipo fursa nyingi zinazoweza kutumiwa na Watanzania katika sekta za kilimo, viwanda, utalii, madini, biashara na miundombinu.

(a) Sekta ya kilimo: Ikilinganishwa na Kenya na Uganda, Tanzania ina eneo kubwa zaidi linalofaa kwa kilimo ekari arobaini na nne milioni, hali nzuri ya hewa kwa kilimo na ina maji mengi zaidi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Katika Afrika Tanzania ni ya pili baada ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa kuwa na maji mengi yanayofaa katika kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo Tanzania ina nafasi ya kuweza kunufaika kutokana na soko kubwa la Afrika Mashariki endapo itafanikiwa kuendeleza kwa ufanisi uzalishaji wa mazao ya kilimo. Baadhi ya mazao ambayo yameonyesha uwezo wa kupenya soko la nchi jirani ni mahindi, unga wa mahindi, maharage, mchele, mboga za majani, ndizi, matunda, karanga, kahawa na mifugo.

(b) Sekta ya Viwanda: Pamoja na kwamba mchango wa sekta ya viwanda katika uchumi wa Tanzania ni mdogo bado sekta ya viwanda inayo fursa nzuri katika Jumuiya

ya Afrika Mashariki tukizingatia ongezeko kubwa la uwekezajitoka nje. Kati ya mwaka 1997 na 2003, jumla ya uwekezaji kutoka nje ulikuwa dola za Kimarekani bilioni 2.2, kiasi kikubwa zaidi ya nchi zote za Afrika isipokuwa Afrika ya Kusini na nchi zinazotoa mafuta. Baadhi ya bidhaa za viwanda ambazo zimeonyesha uwezo mkubwa wa kupenya soko la Afrika Mashariki ni mafuta ya kupikia bidhaa za mafuta ya petroli, bia, vinywaji vikali, vinywaji baridi, vifaa vya umeme, vifaa vya ujenzi, viatu na chumvi.

(c) Sekta ya Utalii: Tanzania inazo mbuga nyingi za wanyama *National Parks na Game Reserves* kubwa na nzuri zaidi ikilinganishwa na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na mlima mrefu zaidi yaani Kilimanjaro na vivutio vingi vya pwani. Kinachohitajika ni kuendeleza na kuzingatia fursa hizi vizuri zaidi ndani na nje ya nchi.

(d) Sekta ya Madini: Tanzania inao utajiri mkubwa wa madini ikiwa ni pamoja na dhahabu, almasi, mawe ya thamani, chumvi, makaa, chuma, phosphates, gesi na kadhalika. Kuanzia mwaka 1995 hadi 2003 zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 1.5 zimewekezwa katika sekta hii. Mauzo ya madini nchi za nje yameongezeka toka dola za Kimarekani milioni 182 mwaka 2000 hadi kufikia dola za Kimarekani milioni 553 mwaka 2003. Ukuaji mkubwa katika sekta ya madini unatoa fursa zaidi ya ajira na mapato ya fedha za kigeni.

(e) Miundombinu: Ili kuweza kutumia fursa hizi vizuri ni muhimu Tanzania kuweka mkazo katika sekta za miundombinu na nguvu kazi. Miundombinu ya bandari, barabara, reli na nishati ni muhimu katika kuimarisha ufanisi wa uzalishaji na kutuunganisha na nchi zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, athari zinazoweza kutokea kwa Tanzania kutokana na kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki ni katika maeneo yafuatayo:-

* Ushindani mkubwa kwa sekta ya viwanda: Kutokana na kuondolewa kwa ushuru katika biashara kati ya nchi wanachama, viwanda vyetu vinapata ushindani mkubwa wa bidhaa kutoka Kenya na Uganda. Viwanda vitakavyoshindwa kushindana vinaweza kufungwa.

* Mapato ya Serikali yatokanayo na kodi: Kutokana na kuondoa ushuru wa bidhaa kati ya nchi wanachama na kushuka kwa ushuru wa forodha kwa bidhaa za nje, mapato ya Serikali kutokana na vyanzo hivi yatapungua. Hii ni kwa kuwa Tanzania na Uganda huagiza bidhaa nyingi kutoka Kenya.

Pia upo uwezekano kwamba bidhaa zinazoagizwa kutoka nchi zingine zitaagizwa kutoka Kenya pale viwango vya kodi vitakapopunguzwa au kufutwa kabisa. Mikakati ya kukabiliana na hali hii ni pamoja na makubaliano ya kuondoa au kupunguza ushuru hatua kwa hatua. Kenya ikifungua soko lake haraka zaidi ili kutoa nafasi ya Tanzania na Uganda kujenga uwezo.

Aidha, ni muhimu kuendeleza hatua ya kuimarisha uchumi ili vyanzo vikubwa vya mapato ya Serikali viwe kodi za ndani na sio ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, fursa ambazo Tanzania itazipata kutokana na kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kubwa, kitu cha msingi sasa hivi ni kuzitumia fursa hizo vizuri. Aidha, ni muhimu wakati huu kuzichukulia athari mbalimbali kuwa changamoto zinazohitaji ubunifu zaidi kwa upande wa Serikali, wazalishaji na wafanyabiashara.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri sana yanayotia moyo Watanzania, nina maswali madogo mawili tu ya nyongeza.

La kwanza, katika fursa ambazo amezielezea mojawapo ni uwezekano wa nchi yetu kuweza kuuza unga wa mahindi katika nchi za Kenya na Uganda na sisi Kongwa tunajulikana kwamba ni wakulima wazuri sana wa mahindi na tuna soko la Kimataifa la mahindi pale Kibaigwa. Sasa swali langu ni kwamba Serikali ina mpango gani wa kusaidia kupatikana kwa wawekezaji watakaoweka vinu vya kusagisha na kukoboresha mahindi pale ili tuweze kuuza Kenya na Uganda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Watanzania wana wasiwasi katika ushirikiano huu wa Afrika Mashariki hasa katika hatua zinazokuja kwamba vijana wao wengi wanaweza kupoteza ajira kwamba ardhi yao kwa kiwango kikubwa inaweza kuchukuliwa na Wakenya na Waganda, wakianzia na huko Same. Je, Serikali inasemaje kuhusu suala hilo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kusaidia kupata wawekezaji kuleta vinu vya kusagisha mahindi kule Kibaigwa, jibu langu ni kwamba, kwa wakati huu ambapo tunahimiza sekta binafsi kufanya kazi hiyo, ningemshauri Mheshimiwa Mbunge awe wa kwanza kabisa kwenda benki na mradi wake ambao umeandikwa vizuri wa shughuli hiyo ya kusagisha mahindi ili akachukue mkopo, ajenge mashine yake, asagishe unga na aweze kuuza Tanzania pamoja na nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwamba labda ardhi yetu itachukuliwa na ajira itapotea, ni kweli tukifungua soko na mipaka yetu tutashindana na wenzetu, ndio maana Serikali inahimiza sana elimu ya msingi, sekondari na hata elimu ya juu ili tuweze kuwa na wataalam wetu wenyewe ambao wanaweza kushindana na wale wa Kenya. Sasa hivi unawakuta wengi kwenye mabenki yetu. Ukiangalia mabenki mengi hapa yanaendeshwa na watu wa Zambia, Zimbabwe na Kenya, ndio Mameneja kwenye haya mabenki ambayo yapo hapa nchini.

Kwa hiyo, wakati sasa umefika na sisi tuwe na Watanzania ambao wataweza kushika nafasi hizo. Lakini nafasi hizo tutazipata ikiwa tutaboresha elimu yetu kama tunavyofanya kutoka na MMES ambayo inakuja na Vyuo Vikuu.

Halafu kufanya kazi kwa bidii na tuwe wabunifu, tukitegemea Serikali kila wakati kwamba ije itufanyie hili na lile kwa kweli hatutafika. Wenzetu wa Kenya hawangoji Serikali, yenyewe inakuja baada ya yeye kuwa ameshaanza, kwa hiyo anasaidiwa na anaendelea mbele. Kwa hiyo, tuwe tayari kupambana na ushindani kutoka Kenya na Uganda. *(Makofi)*

Na. 20

**Mafanikio ya Kupambana na Rushwa**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kupambana na rushwa ni ajenda ya kudumu kwa watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla:-

(a) Je, mkakati wa Kitaifa wa kupambana na rushwa nchini umefanikiwa kwa kiwango gani na katika nyanja zipi?

(b) Je, ni Maafisa Wahasibu wa Wizara na Idara za Serikali zipi wamebainika kufuja fedha za umma au kuitia Serikali hasara na ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa dhidi yao?

(c) Je, ni nini wajibu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa *(PCB)* pale ambapo Afisa Mhasibu katika Wizara au Idara ya Serikali amebainika dhahiri kujihusisha na rushwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mkakati wa Kitaifa wa kupambana na rushwa ulioidhinishwa na Baraza la Mawaziri mwaka 1999 unaendelea kutekelezwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mafanikio makubwa.

Vita dhidi ya rushwa sambamba na vita dhidi ya umaskini ni vya kudumu. Serikali ikishirikiana na Bunge, Mahakama na wananchi imeweza kudhibiti rushwa ndogo ndogo (petty corruption) na rushwa kubwa (grand corruption) kwa mafanikio karibu katika nyanja zote. Muda hautoshi kuyaeleza yote katika jibu hili kwa mujibu wa kanuni za Bunge.

Kwa hiyo, tutasambaza na Waheshimiwa Wabunge taarifa juu ya hatua na mafanikio katika kupambana na rushwa na kuimarisha utawala bora, kuna vijitabu. Kimoja ni cha tulipotoka na tulipo kuanzia 2000-2005.

Mheshimiwa Spika, nikitoa mifano michache rushwa ndogo ndogo (petty corruption) kutokana na ukusanyaji wa kodi za maendeleo na ushuru Vijijini na Mitaani imedhibitiwa kabisa kwa kufuta kodi ya maendeleo na ushuru wa kero. Rushwa katika

uandikishaji watoto darasa la kwanza hakuna kwani kuandikisha mtoto darasa la kwanza ni bure. Aidha, karo ni michango ya aina yote imefutwa.

Rushwa katika sekta ya ardhi katika kupata viwanja na hati imedhibitiwa kwa kiwango kikubwa. Rushwa katika sekta ya biashara katika kupata leseni imedhibitiwa kwa kuzitoa bure kwa wafanyabiashara wadogo na kupunguza ada ya leseni hadi shilingi 20,000/= kwa wafanyabiashara wa kati na wanalipa mara moja.

Mheshimiwa Spika, rushwa kubwa *(grand corruption)* imedhibitiwa katika sekta za ujenzi na fedha. Ujenzi wa barabara unasimamiwa kwa uadilifu mkubwa sana. Wananchi wanaziona hizo barabara za lami na hata zilizojengwa kwa kiwango cha changarawe.

Kwa mfano, barabara ya Chalinze - Morogoro - Melela kilomita 129 imejengwa kwa kusimamia kwa uadilifu wa hali ya juu, fedha ikaokolewa kuweza kujenga kilomita nane kutoka Chalinze hadi Lugoba. Dar es Salaam - Bagamoyo mkandarasi amepigwa faini ya shilingi 447m/=. Nyakanazi - Kigoma faini 127 kwa kuchelewa kumaliza mradi. Penye rushwa fedha haibaki wala faini hakuna. Manunuzi ya Umma *(Public Procurement)* yanafanyika kwa uwazi na kwa kuzingatia sheria. Mapato ya Serikali yanakusanywa kwa uadilifu mkubwa na yameongezeka kufikia wastani wa fedha za Kitanzania shilingi 130bn/= kwa mwezi badala ya shilingi 25bn/= hadi 28bn/= kwa mwezi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika uchunguzi uliofanywa na Taasisi ya Kuzuia Rushwa *(PCB)* kwa mwaka 2004/2005, katika Wizara ya Fedha, Idara ya Bajeti na *Computer,* Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imebainika ufujaji wa fedha za umma na kutia hasara Serikali kwa kiwango kinachokadiriwa kuwa shilingi 2.5bn/=.

Maafisa Wahasibu waliohusika na ufujaji huo wamesimamishwa kazi na tayari maafisa 54 wamefikishwa Mahakamani. Miongoni mwao wamo Wakurugenzi Watendaji kumi na moja, Halmashauri za Wilaya ya Singida, Kondoa, Korogwe, Magu, Nzega, Kisarawe, Ulanga, Mkuranga, Musoma, Manispaa za Mbeya na Tabora. Wapo Waweka Hazina katika ngazi za *Sub Treasury* saba, Wahasibu 28, Maafisa Elimu wanane, Afisa Biashara mmoja, Mganga Mkuu wa Wilaya mmoja na Afisa Utumishi mmoja.

Zoezi la uchunguzi linaendelea ili kuzuia ubadhirifu wa fedha za umma ambalo linafanywa na Taasisi ya Kuzuia Rushwa ikishirikiana na vyombo vya dola ikiwemo Polisi na Mahakama.

(c) Mheshimiwa Spika, wajibu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa umeelezwa katika Sheria ya Kuzuia Rushwa Na. 16 ya Mwaka 1971 pamoja na marekebisho yake. Kwa

kifupi inapobainika kuwa Afisa Mhasibu katika Wizara au mtumishi yeyote yule anayejihusisha na vitendo vya rushwa uchunguzi wa kina hufanywa kukusanya ushahidi na kumpeleka Mahakamani kwa kuzingatia taratibu za Sheria.

Kama ushahidi hautoshelezi kumpeleka Mahakamani basi Taasisi ya Kuzuia Rushwa hutoa ushauri juu ya hatua za kinidhamu na utawala za kumchukulia Afisa au mtumishi husika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hivi vile vitabu alivyovitaja Mheshimiwa Waziri vitawekwa katika visanduku vya barua za Waheshimiwa Wabunge asubuhi hii kule kwenye pigeon holes. Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani ngoja,ni nani aliuliza swali la msingi? Mwenyewe ameridhika.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa hivi sasa kuna Taasisi nyingi za Kidini vile vile hata *PCB* ambazo zimekuwa zinalalamikia sana suala la takrima kwamba linabeba kwa kiasi kikubwa njia mojawapo ya kupitisha rushwa. Na kwa kuwa hata viongozi wa kiroho mmojawapo amezungumza kwamba huu ugonjwa wa takrima ni ugonjwa wa kiroho. Swali ni kwamba Serikali hivi sasa baada ya kung'amua kwamba wengi wanailalamikia sheria hii ya takrima ina jitihada gani za kurudisha ndani ya Bunge ili kufutilia mbali suala hili la takrima kupitia njia ya sheria ili kama takrima ya Kiafrika ipite katika njia na desturi za kikawaida? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, niliwahi kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kutamka kwamba takrima *(Traditional Hospitality)* Bunge hili lilifafanua katika Sheria za Uchaguzi kwamba kwa usimamizi wa Mahakama haitahesabiwa kwamba ni rushwa. *(Makofi)*

Mwanasheria Mkuu wa Serikali nikiwa sipo Bungeni, Bunge lililopita aliulizwa akazungumza kwa niaba ya Serikali kwamba kwa mujibu wa sheria za nchi hii ukarimu si rushwa. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaloweza kutamka kosa la jinai, sio kanisa si kongamano. *(Makofi)*

Nisingependa kuanzisha mdahalo na viongozi wa dini. Ninachosema kwa sasa sheria za nchi hii zimetoa mwongozo namna ya kuendesha uchaguzi kwa kudhibiti rushwa na ikaainisha kwamba vitendo vyote vyote ambavyo kwa mujibu wa sheria hiyo vinaweza vikaelezeka kwamba ni ukarimu kwa viwango vya sheria basi si rushwa. Kama kuna utata kama ni rushwa au si rushwa Mahakama iwajibike kutoa tafsiri hiyo na kuchukua hatua. *(Makofi)*

Bunge lina wajibu wa kulinda Jamhuri ya Muungano na watu wake tusitishwe na Makongamano lakini tuongozwe pia na tafsiri za wananchi endapo Kiongozi wa

Upinzani ataona ni vizuri Muswada huo tuubadili na mifano dhahiri mimi niko tayari kuchangia wakati wa kurekebisha sheria hiyo. *(Makofi)*

Na. 21

**Ushughulikiaji wa Kesi Mahakamani**

**MHE. THOMAS NGAWAIYA (K.n.y. MHE. PHILEMON NDESAMBURO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna kesi nyingi sana ambazo huchukua miaka nenda rudi bila maamuzi ya Mahakama; na kwa kuwa, baadhi ya kesi zina maslahi ya Serikali na wananchi wake:-

(a) Je, kwa nini kesi zenye maslahi ya nchi zisipangiwe utaratibu wa kumalizika katika kipindi maalum ambacho maslahi ya Taifa hayatadhurika?

(b) Je, ni kesi ngapi zenye maslahi ya Taifa bado hazijatolewa maamuzi na Mahakama?

(c) Je, Serikali imeshapata hasara ya kiasi gani kutokana na kesi za namna hiyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI K.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kabla ya kulijibu swali la Mheshimiwa Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, naomba kutoa maelezo ya jumla yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kesi zote ambazo zinafunguliwa Mahakamani na wananchi na hata Serikali yenyewe kwa ajili ya kutolewa maamuzi zinao uzito sawa na Serikali inapenda kesi zote zisikilizwe na kutolewa maamuzi haraka. Kwa kuzingatia azma hiyo, Serikali imekuwa ikijenga mazingira mazuri na thabiti ya utoaji haki hapa nchini ili kuhakikisha kuwa tatizo la ucheleweshaji wa kutatua migogoro na kutoa haki linamalizika. Serikali inao Mkakati wa Kuboresha Sekta ya Sheria *(The Legal Sector Reform Programme)* ambayo Wizara ya Sheria imekuwa ikielezea Bunge lako Tukufu mara kwa mara. Na hivi majuzi Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba alipata fursa ya kutoa mpango mpya wa Mkakati huo huo kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo. Mpango huo unazingatia dira ya Wizara ambayo kauli mbiu yake ni Haki kwa wote na kwa wakati, yaani *(Accessible and timely justice for all).* Baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kwa maslahi ya Taifa kwamba kesi zote zimalizike mapema iwezekanavyo. Mkakati na mipango ya kutekeleza azma hii ni kama nilivyoeleza katika maelezo ya

jumla. Kwa kuwa mazingira ya kila kesi yanatofautiana, Serikali haina mpango wa kuweka utaratibu wa kutoa kipaumbele kwa kesi zenye maslahi ya Taifa ili zimalizike katika muda maalum.

(b) Kama nilivyokwisha kueleza, kesi zote zina maslahi ya Taifa na kwa maana hiyo ni kesi zenye maslahi ya Taifa ni kesi zote zilizopo katika Mahakama za ngazi mbalimbali nchini zinazosubiri maamuzi ya Mahakama.

( c) Kuchelewa kwa kesi yoyote ni hasara kwa wahusika na kwa nchi kwa ujumla kwa jinsi ambavyo ucheleweshaji huo unakwamisha shughuli za biashara na shughuli mbalimbali kuwafanya watu watumie muda wao mwingi kufukuzia haki zao Mahakamani badala ya kufanya shughuli zao za maendeleo. Wanasheria wanao usemi usemao haki iliyocheleweshwa ni haki iliyonyimwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upana wa suala hili lenyewe ni vigumu kupata takwimu za kiwango cha hasara inayohusika kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nilitaka kuuliza maswali madogo mawili.

La kwanza kwa kuwa Shirika la Nyumba ambalo lilikuwa na kesi kwa muda wa miaka 11 na watu wakakaa bila kulipa kodi kwa miaka 11 Serikali ikakosa mapato. Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia vitu kama hivi maana ni muda mrefu mno. Serikali ina mpango gani wa kuweka angalau muda maalum?

Mheshimiwa Spika, pili, kutokana na ongezeko la watu na ongezeko la kesi Majaji ni wachache sana, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Majaji pamoja na maofisi yao?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli pamekuwa na kesi za siku nyingi zinazohusu Shirika la Nyumba la Taifa. Kwa sababu ni kesi ambazo zimekuwa Mahakamani zimekuwa zinafanya Shirika lisiweze kupata mapato yake kwa kiwango ambacho inataka.

Lakini hili nisingelipenda nilisemee sana kwa sababu naamini kama mlivyosoma kwenye magazeti jana bado kuna wananchi wapangaji wa nyumba hizi ambazo wako Mahakamani.

Lakini niseme tu kwa jumla ni nia ya serikali ni kuhakikisha kwamba Shirika hili linatekeleza majukumu ambayo lilikabidhiwa na Taifa katika kujenga nyumba ya kipato cha juu, cha kati na cha chini. Serikali imeazimia kabisa kuipatia sheria iliyoanzisha *National Housing* ili wapangaji waweze kutekeleza wajibu wake na pia *National Housing* iweze kutekeleza majukumu yake kwa wapangaji wake.

Pili, ni kweli idadi ya Majaji tulionao hasa kwa ngazi ya Mahakama Kuu bado haitoshelezi na hili limekuwa linasemwa na Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano wa

bunge uliopita wakati tunajadili Mabadiliko ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini kadri uwezo wa Serikali unavyoongezeka kwa maana uchumi wetu unavyoimarika ni azma ya Serikali kuendelea kuongeza idadi hii ya Majaji wetu ili kuharakisha uamuzi wa kesi ambazo zinafikishwa Mahakamani.

Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Ngawaiya, idadi ya Majaji lazima iendane na idadi ya nyumba za Mahakama. Na ndio katika mpango wa kuboresha sheria nchini eneo hili la kuboresha makazi ya Majaji, nyumba za Mahakama kuanzia ngazi ya Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mkoa na Mahakama Kuu linawekewa mkazo. Kwa hiyo, tuwe na subira lakini makubwa yatafanyika. *(Makofi)*

**MHE. ASHA ALI NGEDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa muda ni jambo muhimu katika kufanikisha jambo lolote na hata kumaliza kesi kwa haraka. Je, Mahakimu ana muda maalum wa kuanza kazi zao katika shughuli za kila siku?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, Mahakama kama taasisi yako ambayo ni mfano wa kuigwa hapa nchini kwamba saa 3.00 kamili shughuli za Bunge zinaanza. Saa 11.00 shughuli za Bunge zinaanza na Mahakama zetu zinapashwa zianze kazi saa 3.00 asubuhi rasmi. Sasa yawezekana yapo matatizo lakini tunavyofahamu shughuli za Mahakama saa 3.00 asubuhi ambapo ni siku ya kazi zinapashwa Hakimu ameingia yuko katika Mahakama yake. Yawezekana ucheleweshaji wa hapa na pale upo kama wengine wanaweza wakaanza saa 4.00 lakini hiyo naita sio *the normal.*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niweze kuuliza na mimi swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna kesi za maslahi ya nchi ambazo zimepelekwa katika Tume ya Haki za Binadamu na Tume hiyo kuwapata watu wana hatia na kuiomba Serikali itekeleze matakwa ya hiyo Tume lakini unakuta mpaka sasa haijatekeleza. Je, ni kwa nini hasa hii kuhusu jimbo la Serengeti? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Tume ya Haki ya Binadamu na Utawala Bora ilishughulikia suala la matatizo ya Serengeti. Lakini kama tunavyofahamu sheria iliyoanzisha Tume hiyo inaipa Tume uwezo wa kutoa taarifa na mapendekezo ya tatizo lililoletwa malalamiko yaliyofikishwa mbele yake. Ikishafanya hivyo Serikali na vyombo vyake inapashwa na vyenyewe vipewe muda wa kuiangalia mapendekezo ambayo yametolewa na pindi Serikali ikiridhika kwamba yapo ambayo yanaweza yakachukuliwa hatua za mara moja na yale ambayo yanahitaji yakafanyiwe kazi zaidi hayo ni masuala ambayo yanafanywa hivi sasa.

Hili la Serengeti nisingelipenda sana nilisemee kwa sababu ni sehemu ya mchakato wa maamuzi ya serikali kutokana na uamuzi huo wa Tume ya Haki za Binadamu.

Na. 22

**Suala la Haki za Binadamu**

**MHE. JANETH B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la haki za binadamu kimataifa limetiliwa mkazo sana; na kwa kuwa, bado Mahakama zetu wakati mwingine zinatumia Sheria za Utamaduni *(customary laws)* katika maamuzi kadhaa:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, utaratibu wa kuchambua sheria potofu ambazo zinakandamiza Wanawake na watoto zifutwe kabisa na badala yake Majaji waendeleze kutumia *International Laws* katika kuleta haki?

(b) Je, suala la kumrithi mke, Serikali haioni kuwa limepitwa na wakati na linakiuka haki za binadamu?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA )** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Sheria za kimila zimetokana na mila na desturi za jamii zetu ambazo zimejengeka na kudumu kwa muda mrefu. Nyingi ya sheria hizo zimeandikwa na kutangazwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 436/1963 baada ya Serikali kuratibu mapendekezo yaliyotolewa na wananchi kupitia Halmashauri zao. Sheria za kimila bado zinaendelea kutumiwa na Mahakama zetu katika kutatua migogoro ya kimila.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba pale ambapo sheria za kimila zimeonyesha kukiuka sheria za nchi na haki za binadamu, Mahakama za hapa nchini zimekuwa zikitoa maamuzi ya kuziharamisha mila na desturi hizo.

Kwa kuwa mila na desturi hizo zina wenyewe, Serikali inaamini kuwa ni vema tukaendelea kuzingatia jadi, mila na desturi zetu, ambazo sio potofu, kwa maana mila na desturi hizo ni sehemu muhimu ya hazina ya utamaduni wetu.

Baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ipo katika hatua ya kuandaa Waraka wa Serikali (White Paper) kwa ajili ya kupata maoni ya wananchi ambapo baadhi ya hoja katika waraka huo zitahusu haki za

Wanawake na Watoto. Kwa upande mwingine, pamoja na kwamba nchi yetu imeridhia Mikataba ya Kimataifa kuhusu haki za binadamu, kwa mujibu wa sheria zetu, Mahakama bado zinapaswa kuzingatia sheria za nchi na pale tu panapokuwa na pengo katika sheria za nchi ambapo pengo hilo hujazwa na sheria nyingine za Kimataifa ikiwemo Mikataba ya Kimataifa kuhusu haki za binadamu.

(b) Napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba suala la kumrithi mke aliyefiwa na mume hasa wakati huu ambapo UKIMWI ni tishio kubwa limepitwa na wakati. Hata hivyo, mke aliyefiwa na mume yuko huru na anazo haki zote za kujiamulia mambo yake kwa mujibu wa Sheria za Nchi. Napenda ifahamike kwamba suala la kumrithi mke aliyefiwa na mume msingi wake ni taratibu za kimila ambazo bado zimejikita katika baadhi ya makabila yetu na wala haiko sheria mahususi iliyotungwa na Bunge hili inayoweka utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, kwa vile suala la kumrithi mke aliyefiwa na mume ni suala la kimila na linahusu utawala binafsi kwa maana kwamba ni suala la hiari Serikali haina mpango wa kutunga sheria ya kuharamisha mila hiyo. *(Makofi)*

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kuna mikoa mingi na hasa Mkoa wa Mara ambao una hizi ndoa zinaitwa za *nyumba ntobo* yaani mwanamke mume, kumwoa mwanamke mke ambazo mwanamke huyo mke hupelekwa kwa wanaume mbalimbali akazalishwe watoto. Je, ataniambia Mwanasheria Mkuu kuhusu hilo wanafikiriaje kwa sababu ndio litaleta ambukizo kuu ya UKIMWI? *(Makofi)*

Pili, pamoja na yale aliyoyazungumza mimi nakubaliana nayo lakini sikubaliani katika hizi mila potofu. Serikali bado tunaiomba na ituambie ni lini itaweka na kutunga sheria ili kuhakikisha ndoa kama hizi ziishe kabisa? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi tumesema zipo mila potofu na pale ambapo mwananchi amekwenda Mahakamani kuhoji uhalali wa mila hizo nimesema Mahakama zetu zimekuwa msitari wa mbele kabisa katika kuharamisha mila na desturi hizo. Hasa hili la *nyuma ntobo* au *nyumba emboke* ambayo nadhani amesema ameyafanyia utafiti Mheshimiwa Kahama katika maeneo ya mikoa mbalimbali na hususan Mkoa wa Mara. Niseme tu mwanamke anayepelekewa wanawake hao kama wake zake. Kwanza kwa misingi tu ya ndoa sheria zetu hazitambui ndoa ya jinsia moja. Hilo la kwanza. La pili, mimi siamini kwamba huyo mama anayepelekewa hao wanawake au wasichana kwamba ana silaha za maangamizi yeye mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, yawezekana yeye anakodi silaha za maangamizi kutoka kwa wanaume wengine nadhani tunakuja katika suala zima la kusema wakati huu ambao tunapambana na UKIMWI ni vizuri hizi mila tuachane nazo. Suala la msingi ni elimu kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mimi siamini kabisa kwamba kwa kutunga sheria peke yake kwamba utaweza kuondoa tatizo hilo ambalo limejikita sana katika mila zetu. Utamaliza kuwasweka jela watu hawa lakini nadhani dawa yake ni elimu na pia kuwawezesha wanawake kiuchumi ili waweze kujitegemea na hilo nadhani nimejumuisha katika kujibu na swali lake la pili.

Na. 23

**Uchakavu wa Sarafu**

**MHE. ALHAJ AHMADI H. MPEME** aliuliza:-

Kwa kuwa, sarafu zetu za shilingi mia moja na shilingi hamsini zinapata uchakavu kwa haraka na kufikia kiwango cha kukataliwa katika matumizi na kusababisha wananchi kupata hasara hasa kwa wale wanaoishi mbali na Benki:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha sarafu hizo kuchakaa kwa haraka hadi kupoteza thamani yake?

(b) Kama tatizo ni uhafifu wa madini yanayotumika katika kutengeneza sarafu hizo. Je, Serikali haioni kuwa ni muhimu sasa kutumia madini yaliyo bora zaidi ili kuzifanya imara sarafu hizo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS D. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Ahmadi H. Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sarafu zote duniani hutengenezwa kwa madini kwa lengo kuwa zidumu muda mrefu zaidi ya noti. Madini yanayotumika duniani kutengeneza sarafu ni *curpronickel, nickel, copper and brass.* Na kwa sarafu zenye thamani ndogo hutumia mchanganyiko wa *brass* na chuma au *nickel* na chuma. Sarafu zetu zimetengenezwa kwa madini madhubuti. Kwani shilingi 200 imetengenezwa kwa *cupronickel,* na sarafu za shilingi 50 na shilingi 100 zimetengenezwa kwa mchanganyiko wa *brass* na chuma.

Tatizo lililopo ni kwamba sarafu nyingi zinakaa katika mzunguko kwa muda mrefu bila kurejeshwa Benki Kuu kubadilishwa. Sarafu za shilingi 100/= na shilingi 50/= ni sarafu zinazotumika sana katika mzunguko wa fedha, hivyo mzunguko huu huchangia kwa kiasi kikubwa, katika uchakavu wa sarafu hizi. Baadhi ya sarafu hizo zimekuwa katika mzunguko kwa miaka kumi sasa. Mabenki ya biashara, wafanyabiashara, na raia kwa ujumla hawazirejeshi Benki Kuu fedha chakavu ili zibadilishwe na sarafu mpya.

Katika uchaguzi wa madini ya kutengeneza sarafu Benki Kuu zote duniani, ikiwa ni pamoja na Benki Kuu ya Tanzania, lazima zichukue tahadhari ya kutokuboresha mno madini ya kutengenezea sarafu. Ikiwa madini yenyewe yanakuwa na thamani zaidi

kuliko ile inayoonyeshwa kwenye sarafu, wahalifu huziyeyusha sarafu na kuziuza kama madini.Ili kuhakikisha kwamba panakuwa na sarafu bora kwenye mzunguko nchini, Benki Kuu imetekeleza yafuatayo:-

(a) Benki Kuu imeyaelekeza Mabenki yote nchini kulipa noti na sarafu safi kwa wateja wao. Hii ni katika mpango wa Benki Kuu ujulikanao kama "Clean Money Policy". Wateja wana haki ya kukataa kupokea fedha chakavu katika Mabenki. Mabenki mengi yanajaribu kuepukana na gharama ya kuchagua sarafu chakavu ili zirudishwe Benki Kuu kubadilishwa na sarafu safi. Mabenki pia yameshauriwa kununua mashine za kisasa za kuhesabu na kuchambua sarafu.

(b) Kuendelea na utaratibu wa kupokea na kubadilisha sarafu zilizochakaa kwenye matawi yote ya Benki Kuu na Ofisi zote za Benki Kuu zilizopo kwenye matawi ya Benki za Biashara sehemu mbalimbali nchini.

(c) Kutumia Benki za Biashara, hasa zile zenye mtandao mkubwa nchini, kusambaza fedha safi na kukusanya fedha zilizochakaa kutoka kwenye mzunguko na kuzirudisha Benki Kuu ya Tanzania na Ofisi zote za Benki Kuu zilizopo kwenye matawi ya Benki za Biashara.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu itaendelea kutafuta mbinu za kufikisha sarafu nyingi na safi ambazo hazijatumika bado kwa raia. Na pia kuyahimiza Mabenki mengine yote nchini kushiriki katika kuondoa sarafu na noti chakavu katika mzunguko wa fedha.

**MHE. ALHAJI AHMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza ulisema kwa kuwa sarafu zote duniani huwa inatengenezwa kwa aina zinazofanana za madini. Na kuwa zipo sarafu ambazo zimetengenezwa hasa zile zilizotengenezwa na Wajerumani zipo mpaka leo zikiwa nzuri sana. Sasa hivi madini hayo kama yanafanana kwa nini zile zinaishi kwa muda mrefu na hizi za kwetu zinaishi kwa muda mfupi? *(Makofi)*

La pili, ni kwamba kwa kuwa wananchi vijijini wanapokataliwa kutumia fedha hizo kwa wafanyabiashara wanazitupa. Je, Serikali inatoa tamko gani hasa kwa wafanyabiashara wanazozipata fedha hizo ili kuwasaidia wale wananchi wasiendelee kupata hasara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilitaka majina ambayo yanatumika kutengeneza sarafu duniani kote. Tatizo kubwa nitakalolitaja ni kwamba zinakaa muda mrefu sana kwenye mzunguko na zingine zimekaa zaidi ya miaka kumi katika mzunguko. Nilisema kwamba Mabenki ya Biashara yanakwepa gharama za kuzipeleka hizo fedha Benki Kuu kwa ajili ya kubadilishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda nitoe wito tena kwamba Benki ya Biashara na Wafanyabiashara pamoja na wananchi kwa ujumla wanapopata sarafu chakavu wazipeleke kwenye benki. Siyo tu Benki Kuu pia kwenye benki nyingine ambazo ziko karibu na maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito pia kwa wananchi kwamba wanapokwenda benki wasikubali kupokea noti na sarafu chakavu wazikatae kwa sababu ni wajibu wa benki za biashara, wamepewa maelekezo na Serikali na Benki Kuu kwamba wazikusanye noti na sarafu chakavu wazirudishe Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, kama kuna wananchi wanatupa sarafu kwa sababu zimekataliwa ama zinakataliwa basi naomba tupate kama fedha hizo zipo na zilitupwa. Lakini mtu anayetupa fedha nafikiri akili yake siyo timamu kwa sababu fedha zote zikipelekwa benki lazima zikubaliwe. Hakuna Benki ya Biashara ambayo inakataa noti ama sarafu chakavu.

Na. 24

**Malipo ya Wastaafu**

**MHE. ALLY A. KARAVINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeamua kurudisha utaratibu wa pensheni ya mwezi kwa watumishi waliokuwa wamelipwa kwa mkupuo:-

Je, kwa nini watumishi wa Mashirika ya Umma waliolipwa kwa mkupuo hawajarejeshwa kwenye orodha ya pensheni ya mwezi hasa yale Mashirika yaliyokuwa na Mfuko wa Pensheni kama Serikali *(non-contributory)* kama *TRC, THA* na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ally Amani Karavina, Mbunge wa Urambo Mashariki, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Watumishi wa Mashirika ya Umma na wa Serikali wana utaratibu tofauti wa ajira na ulipaji mafao ya kustaafu, kufuatana na sheria iliyoliunda shirika husika na sheria za mifuko wanamochangia. Wakati mafao ya kustaafu kwa watumishi wa Mashirika ya Umma na sekta binafsi husimamiwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* na Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma *(PPF),* mafao ya kustaafu watumishi wa Serikali Kuu yalikuwa yakilipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na sasa husimamiwa na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF)* na Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali *(GEPF).* Aidha kwa watumishi walio chini ya Serikali za

Mitaa *(Local Government)* Mafao yao husimamiwa na Mfuko wa Akiba kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa *(LAPF).*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Amani Karavani, Mbunge wa Urambo Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Mashirika ya Umma waliokuwa wanachangia katika Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF)* walilipwa pehsheni zao kwa mkupuo kwa mujibu wa sheria baada ya kuomba wao wenyewe. Hivyo walilipwa stahili zao zote (100%).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Mashirika kama *TRC* na *THA* yalikuwa katika mfumo wa pensheni wa *non-contributory* watumishi wake hawawezi kurejeshwa katika utaratibu wa pensheni ya mwezi kwa kwa masharti yao ya Ajira ni tofauti na yale ya watumishi wa Serikali Kuu. Suala hilo lingewezekana kama sheria zilizoanzisha Mashirika hayo zingetoa fursa hiyo na Mashirika yenyewe kuwa na uwezo kifedha wa kuwalipa watumishi wao.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu baada ya kuvunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuanzisha mashirika yetu ya Tanzania, wafanyakazi wengi wa Serikali walihamishwa kwenye mashirika hayo ya umma kwenda kufanya kazi na baadaye wakastaafu wakiwa huko. Je na hawa nao hatima yao vipi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Amani Karavina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la watumishi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki lililotolewa ufafanuzi na Waziri wa Fedha wiki iliyopita na masuala yao yanashughulikiwa kwa maana ya kwamba madai yao yanachambuliwa na yatakapokuwa yamefikia ufumbuzi basi Serikali itatoa tamko ya namna ya kuyafanya. Lakini mambo ya *pension* kwa mashirika haya hayaingiliani moja kwa moja na matatizo haya ambayo hawa wastaafu kwa maana ya maslahi yao *pension* kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi na sheria yake na ni tofauti na zile za Serikalini. Kwa hiyo, kama mashirika yenyewe yana uwezo wa kulipa *pension* watumishi wake basi yana ruhusa ya kufanya hivyo na Serikali haitayaingilia mashirika hayo yakiamua kufanya hivyo.

Na. 25

**Walimu wa Kutosha - Sekondari za Kutwa**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa, imedhihirika wazi kuwa Shule za Sekondari za Kutwa *(Day Schools)* zimesaidia katika kuongeza idadi ya watoto wanaopata Elimu ya Sekondari, kwa kushirikisha pia juhudi za wananchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Sekondari hizo zinapatiwa walimu wa kutosha ili wanafunzi wake wapate elimu iliyo sawa na wenzao waliochaguliwa katika Sekondari za Taifa?

(b) Je, Serikali inafahamu mapengo ya nafasi za walimu wa shule hizo zilizopo Wilaya ya Masasi na inatarajia kuchukua hatua gani ili kuziba mapengo hayo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuinua kiwango cha taaluma katika shule hizo ili kilingane ama kupita shule zinazoendeshwa na Serikali moja kwa moja?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004-2009 ili kuhakikisha mahitaji yote muhimu pamoja na walimu yanapatikana kwa shule zote za Sekondari tulizonazo na mpya zitakazojengwa chini ya Mpango huu.

Hatua muhimu ya kuhakikisha kuwa tutakuwa na walimu wa kutosha ni kubadilishwa Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam na Sekondari ya Mkwawa kuwa Vyuo Vikuu vya Elimu za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kutuwezesha kuwa na walimu wa Sekondari wa kutosha kwa mahitaji ya sasa na ya shule mpya karibu 1500 zitakazojengwa katika utekelezaji wa MMES 2004/2009.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Masasi zipo shule 16 za Sekondari za Serikali, zilizosajiliwa. Shule hizo zinakabiliwa na upungufu wa jumla ya walimu 87 katika masomo mbalimbali. Wizara yangu ilipata kibali kutoka Idara Kuu ya Utumishi cha kuajiri walimu wapya 1,715 mwezi Machi 2004 na walimu 1,650 mwezi Septemba, 2004.

Walimu 28 wa Masomo ya Sanaa na 16 wa Sayansi jumla 44 wamepangwa katika Wilaya ya Masasi. Kwa hiyo, pengo la walimu katika shule zote nchini zikiwemo za Wilaya ya Masasi litaendelea kupungua, lakini inafaa ieleweke kuwa mapengo yatapungua upesi zaidi kwenye shule zenye Nyumba za walimu.

(c) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali ni kuinua kiwango cha taaluma katika shule zote za sekondari kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004-2009 ambao utahakikisha mambo yafuatayo:-

(i) Kutoa ruzuku ya maendeleo kuwasaidia wananchi wanaojenga majengo ya shule za sekondari za kutwa. Ruzuku hiyo itakuwa shs. 7 milioni kwa darasa na 9.0 milioni kwa nyumba ya mwalimu.

(ii) Kuongeza mafunzo na ajira ya walimu.

(iii) Kuzipatia shule za sekondari za Serikali ruzuku ya uendeshaji *(Capitation Grant)* ya shs. 60,000 kwa mwanafunzi kwa ajili ya ununuaji wa vitabu na vifaa vingine vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia.

(iv) Kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shule.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa majibu aliyoyatoa hapa Bungeni. Lakini ningependa kuzungumza kwamba kwa kuwa katika Jimbo la Masasi hasa katika shule za Mwenge, Mtapika, *Masasi Day,* Lukuledi, Mbemba, Chigugu, pamoja na Mwena shule hizi zote zina upungufu wa walimu kutokana na walimu waliopangiwa katika maeneo haya kutokwenda Masasi kwa sababu zao binafsi na wengine wanadiriki hata kuja Masasi wakiwa na barua za uhamisho kutoka Makao Makuu.

Je, Wizara inatoa kauli gani kuhusu tatizo hili ambalo limetusibu sana katika Wilaya ya Masasi na nafikiri hata *Mtwara Corridor* na hata Mikoa mingine ya pembezoni, Wizara inatoa kauli gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, hilo tatizo Wizara inalifahamu na kwa kawaida tunapopata taarifa pale Wizara kwamba kuna walimu ambao wamekwenda wakarudi au hawakwenda kabisa tunachofanya sisi ni kufuta ajira zao na kuhakikisha kwamba tunapanga walimu wengine wapya. Lakini kama nilivyosema vile vile tujitahidi kujenga mazingira ambayo yanavutia walimu wetu kukaa. Moja ya matatizo walimu wanayopata katika shule mbalimbali ni ukosefu wa nyumba. Kwa hiyo, tunaomba ndugu zangu wa Wilaya ya Masasi tujitahidi kujenga nyumba za kutosha kwa ajili ya kuvutia walimu.

**SPIKA:** Sijui kati ya hawa wawili nilimuona nani kwanza? Nadhani sikuwaona kwa wakati mmoja. Kwa kuzingatia muda Waheshimiwa Wabunge mnisamehe tuendelee na maswali mengine. *(Kicheko)*

Na. 26

**Mpango wa MMES**

**MHE. MUSA A. LUPATU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeanzisha mpango wa maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) kama ilivyotangazwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2004/2005.

(a) Je, fedha za mpango huo zitatolewa kwa vigezo gani?

(b) Je, usimamizi wa shughuli za mpango huo utakuwaje?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Lupatu Mbunge wa Korogwe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) zinatolewa kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-

(i) Lengo la mwaka husika la kupeleka sekondari asilimia ya watahiniwa wa Darasa la VII wa mwaka uliopita. Kwa mfano lengo la mwaka huu wa 2005 ni kupeleka Sekondari Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya asilimia 35 ya watahiniwa wa *Division II* wa mwaka jana 2004.

(ii) Nafasi zilizoko ndani ya Wilaya husika za kidato cha kwanza na nafasi za kitaifa ilizopangiwa Wilaya hiyo.

(iii) Madarasa mapya yanayohitajika kujengwa ili kuiwezesha Wilaya hiyo kufikia lengo kwa mfano la mwaka huu la kupeleka Sekondari asilimia 35 ya watahiniwa wa *Division II* wa mwaka jana. Madarasa hayo ndiyo yatakayopangiwa Ruzuku ya maendeleo ya Shs. 7 milioni kwa darasa. Ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu inapangwa kwa kuzingatia wingi wa walimu wa shule za sekondari wasio na nyumba.

Umuhimu wa kwanza unatolewa kwa Wilaya ambazo hazikupangiwa madarasa kwa sababu wanayo ya kutosha lakini wanao uhaba wa nyumba za walimu.

(b) Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mpango huu kitaifa unaratibiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Utamaduni, kupitia Idara ya Elimu ya Sekondari na Mkuu wa Shule kwa kushirikiana na Bodi ya Shule yake anasimamia utekelezaji wa mpango katika shule yake. Kwa shule mpya ambazo hazijawa na Bodi ya Shule fedha zinapitia Shule Mlezi *(Foster School)* iliyoteuliwa.

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini napenda kuuliza maswali mawili.

(a) Kwa kuwa fedha hizi za MMES kwa ujenzi wa shule za sekondari mpya kama alivyoeleza zinapitia kwa walimu wa Shule Mlezi na kwa kuwa katika shule hiyo mlezi wanaojenga shule hiyo wako katika eneo lingine. Je, wale wanaojenga ile shule wanasimamiaje matumizi ya fedha hizo ambazo zinapitia Shule Mlezi? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa baada ya Wilaya kutoa taarifa au ombi la kupatiwa fedha za MMES, fedha hizi hupelekwa moja kwa moja kwenye akaunti ya shule ya sekondari. Je, taarifa kutoka Wizara ya Elimu inapelekwa namna gani kwenye Wilaya ambayo imeomba fedha hizo kupelekwa kwa kuwa imepelekwa moja kwa moja kwenye shule ya sekondari? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili kutoka kwa Mheshimiwa Musa Lupatu, kama ifuatavyo:-

(a) Fedha kwa shule ambayo inajengwa haijawa na akaunti, fedha zinapelekwa kwa Shule Mlezi. Tunaamini kuna mawasiliano kati ya Shule Mlezi na shule inayojengwa. Kwa hiyo, usimamiaji wake unafanyika kwa kushirikiana. Anayepokea anatoa takwimu za matumizi yake kwa kumueleza yule ambaye ni Mlezi ili aweze sasa kupeleka Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba fedha mlizotuletea zimetumika na namna hii. Wizara ya Elimu ikiridhika inatuma hela zingine.

b) Fedha kutumwa moja kwa moja kwenye akaunti ili shule ile ikipokea zile fedha inazitumia, halafu inatoa maelezo kama nilivyoeleza katika kupitia katika Shule ya Mlezi. Kwa inakuwa kuna uoanisho kati ya matumizi yanayoendelea katika shule na mtoa fedha. Lakini ili kuhakikisha haya matumizi hayapotei katika kuelekeza katika Wizara ya Elimu na Utamaduni, kuna msimamizi maalum ambaye ameteuliwa katika Wizara ya Elimu na Utamaduni, kushughulikia fedha zinazotolewa na MMES na kuwasiliana na shule hizi. Yuko *desk officer* maalum kabisa.

**SPIKA:** Waziri sasa utajibu maswali ya Wizara mwenyewe. Maswali kwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Na. 27

**Mikopo ya Masharti Nafuu kwa Wazee**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa wazee wastaafu katika Mkoa wa Mtwara wamejiunga pamoja kwa lengo la kufanya shughuli mbalimbali kama vile kilimo, kutoa elimu ya UKIMWI na kadhalika na baadhi ya Wilaya zimejisajili.

Je, Serikali katika kuwawekea mazingira mazuri wastaafu wake inasema nini juu ya kuwasaidia wazee hao kupata mikopo yenye masharti nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa napenda kuwapongeza wazee wastaafu wa Mkoa wa Mtwara kwa uamuzi wao wa busara wa kujiunga pamoja na kufanya shughuli za kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya ushindani tuliyonayo, kuunganisha nguvu ni silaha muhimu katika kujiletea maendeleo. Serikali imehamasisha vyombo mbalimbali vya fedha, hasa mabenki kama Benki ya Posta, *CRDB Bank*, *Adili Bank* na *NMB Bank* ambavyo hutoa mikopo ya masharti nafuu kwa watumishi na makundi mbalimbali ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na wazee wastaafu wa Mtwara ili waweze kukopa kutoka kwenye mabenki hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa wito kwa vyombo mbalimbali vya fedha viendelee kubuni njia za kuwapatia mikopo nafuu zaidi makundi maalum katika jamii kama vile wazee na watu wenye ulemavu.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na Majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Tarehe 29 Machi, 2005 Wazee wa Mkoa wa Mtwara, ikiwemo Mtwara, Newala yenyewe wamekaa, matatizo waliyojadili ni hayo kwamba hawapati mikopo wana michanganuo mimi mwenyewe nimeona wanapeleka kwenye kitengo cha UKIMWI hawapati, je na hilo Waziri anasema nini kuhusu tatizo la Wazee hao wastaafu? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa kitengo cha kulipa mafao ya *pension* kimeshindwa kabisa kutekeleza majukumu yake kwa wakati muafaka kwa hawa wazee wanaolalamika tangu Serikali ilipoweka kitengo hiki. Je, Serikali inaboreshaji kitengo hiki ili kuendelea kuwatolea kero wastaafu wakiwemo Wanawake wa Mkoa wa Mtwara? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu mawili ya Mheshimiwa Lydia Boma, kama ifuatavyo:-

(a) Inawezekana tarehe 29 Machi, 2005 wazee hawa walikaa kujadili kukwama kwa michanganuo yao katika benki. Lakini kukwama huko hakumaanishi kwamba makundi mbalimbali ya uzalishaji mali yakiwemo ya wazee yanakataliwa kupata mikopo yao benki kwa sababu yako makundi yanayoendelea kupata mikopo benki.

Bila shaka inawezekana kuna tatizo la kitaalam ambalo limejitokeza na ningeomba basi Halmashauri zetu za Wilaya kupitia Maafisa Mipango, wajaribu kuwasaidia wazee hawa tuone walichokwama ni nini, utaratibu wa kuomba mikopo yenyewe, au hawatimizi sifa za kupata mikopo kutoka benki, ili jambo hilo litakapotokea Serikali kupitia Wizara zinazohusika ziweze kuwasaidia wazee hawa.

(b) Kuhusu mafao ya *pension* kwa kweli hivi sasa kuna maendeleo makubwa katika ulipaji wa pension kwa wazee wastaafu. Wazee wengi hata wale ambao walikuwa hawamo kwa maana walishachukua fedha zao za mkupuo wameendelea kupata pension

zao na kwa wale wachache ambao kulikuwa na matatizo ya rekodi zao Wizara ya Fedha inaendelea kushughulikia matatizo hayo kupitia sub treasuries huko mikoani ili kuhakikisha kwamba tatizo hilo linajiondosha. Mimi ningependa kumuomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wote kutoa taarifa katika Wizara inayohusika pale linapojitokeza tatizo maalum la pension badala ya kuamini tu kwamba pension ni tatizo kwa wazee wote jambo ambalo sasa hivi limesharekebishwa.

Na. 28

**Mpango wa Maendeleo ya Michezo**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kuhakikisha kwamba michezo inaendeshwa Kisayansi, Serikali imeandaa muundo wa kutengeneza mpango wa maendeleo ya Vyama vya Michezo ikiwa na maeneo kumi (10):-

(a) Je, ni maeneo gani hayo?
(b) Ni vyama vipi vilivyoonyesha mafanikio?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali imeandaa muundo wa kutengeneza mpango wa maendeleo ya vyama vya michezo yenye maeneo kumi. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

1. Uongozi na Utawala;
2. Ushiriki katika michezo;
3. Maendeleo ya wachezaji;
4. Maendeleo ya ufundishaji;
5. Maendeleo ya uamuzi;
6. Mpango wa mashindano;
7. Mpango wa ugharamiaji wa michezo;
8. Maendeleo ya Sayansi ya Michezo;
9. Miundo mbinu ya michezo;
10. Siku maalum kwa chama husika.

(b) Mheshimiwa Spika, vyama vilivyoonyesha mafanikio angalau kuyafanyia kazi baadhi ya maeneo ni Chama cha Kriketi Tanzania, Chama cha Mpira wa Wavu Tanzania, Chama cha Riadha Tanzania, Chama cha Olympiki Maalum na Chama cha Mpira wa Mikono Tanzania.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

(a) Sayansi haiwezi kuingia mahali ambapo hapana fedha, kwa maana hiyo, vyama vyetu vinashindwa kujitegemea kutokana na kuwa havina vyanzo vya kupatia fedha. Je, Wizara inasemaje kulishughulikia suala hili ili vyama vyetu viwezi kujitegemea kifedha?

(b) Kuna vyama ambavyo tayari vimeonyesha mwelekeo na bado vingine havina mwelekeo. Je, Wizara inavisaidia vipi vile ambavyo havijaonyesha mwelekeo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mzee Zubeir Ngwali, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

(a) Amesema sayansi haiwezi kuingia mahali pasipokuwa na fedha ndiyo maana katika maeneo yale kumi ya utawala kuna uongozi na utawala. Makusudio ya eneo hili kwa wale ambao wameshapata nafasi ya kupata mafunzo haya ni pamoja na kupanga taratibu za kupata fedha. Kwa sababu watu wanapojikusanya kwa pamoja wakaanzisha chama kiwe cha michezo au cha burudani, cha sanaa na kadhalika tayari wana utaratibu wa kujipatia fedha.

Serikali husaidia tu pesa ambazo tayari zimeshakusanywa na kikundi chenyewe. Kwa hiyo, sayansi haiwezi kusubiri fedha kusubiri utawala, utawala ndiyo utakaotengeneza mazingira mazuri ya kupata fedha, kuingiza sayansi katika michezo na yale mambo mengine tisa yaliyobakia.

(b) Kuna baadhi ya vyama havina fedha kabisa kutokana na mapato yake. Je, Serikali inasaidiaje? Nasema kitakuwa ni chama cha ajabu sana hicho, wanaanzisha chama, wanapanga na *program* ya mashindano yao, lakini hawana fedha hata senti moja.

Sasa chama hicho katika ulimwengu wa vyama vyetu tulivyovisajili sisi hapa Tanzania hakipo, wanapata fedha wengine kutoka nje, wengine hupata ndani lakini tatizo kubwa linakuja kwenye utawala, pesa zinafujwa na matokeo yake chama kinashindwa kusonga mbele na matokeo yake kinarudi nyuma mpaka kinakufa kabisa.

Kuna baadhi ya vyama katika ya vyama 78 tulivyovisajili vimeshakufa kwa sababu ya ufujaji wa fedha. Hata wakiletewa sare track-suit kutoka nje na zenyewe zinapigwa bei vile vile.

Na. 29

**Wizi Uliofanyika katika Benki ya Akiba na Mikopo**

**MHE. MEJA JESSE J. MAKUNDI** aliuliza:-

Kwa kuwa sheria mpya ya Ushirika na Masoko ilipitishwa Bungeni na kuwekewa saini na Mheshimiwa Rais na hatimaye kutungiwa Kanuni na kutolewa kwenye gazeti namba 274 la tarehe 30 Julai, 2004 na kwa kuwa kuna wizi uliofanywa katika Benki za Akiba na Mikopo ambapo Wakaguzi wa Hesabu wa nje na wa ndani na wa *(COASCO)* pamoja na Kamati ya muda walichunguza na kubaini wizi huo unaofanana na ule uliotokea katika benki nyingine nchini kama *CRDB, NBC, NMB* na *EXIM Bank* na wezi hao kukamatwa:-

(c) Kwa kuwa, wezi hao walioiba katika Benki ya Akiba na Mikopo hasa wa Jimbo la Vunjo wanawatambia maelfu ya waliowaibia wakisema kuwa Benki Kuu inaibiwa, sembuse vibenki uchwara, Je, kwa nini wasikamatwe, kufilisiwa na fedha kurudishwa benki ili walioibiwa waweze kulipwa fedha zao?

(d) Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Mkapa, aliyeingia madarakani tangu mwaka 1995 analifahamu tatizo hilo vizuri sana na amekwishatoa maelekezo kwa Wizara husika kuchukua hatua zipasazo kwa tatizo hilo lakini mpaka mwaka huu 2005 ambapo uongozi wa Wizara husika utakapoondoka madarakani haujawachukulia hatua yoyote wezi hao. Je, Serikali haioni kuwa anayemficha na kumlinda mwizi ni Waziri mwenyewe?

Je, ni kiasi gani cha hongo kimepokelewa Wizarani tangu mwaka 1995 - 2005 ili wezi hao walindwe na wasifilisiwe.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meja Jesse J. Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kutekeleza wajibu wake wa kusimamisha na kuvilinda vyama vya Ushirika na mali za wanachama wake ilielekeza na kusimamia kufanyika kwa ukaguzi aliouelezea Mheshimiwa Mbunge ambapo Hesabu za Vyama vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* vilivyoko katika jimbo la Vunjo vilikaguliwa na kutolewa taarifa. Vyama vilivyokaguliwa na taarifa zake kutolewa ni Mamba, Mwika *North - East,* Ngakoma, Marangu - *East, Marangu - West* na *Legho* - Mulo. *(Makofi)*

Taarifa za Wakaguzi za Vyama hivi zinaonyesha kuwa katika vipindi tofauti kati ya mwaka 1998 na 2003 kulikuwapo na matukio yaliyosababisha hasara ya Jumla ya Shs. 131,171,983/= ambazo zilitokana na uongozi mbaya na ubadhirifu uliofanywa na baadhi

ya viongozi. Kwa hali hiyo wizi huo haufanani na ule uliotokea katika mabenki aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa za ukaguzi zilizobainisha ubadhirifu huo, Serikali ilichukua hatua kupitia kwa Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoani Kilimanjaro kwa kuwaamuru viongozi waliohusika na ubadhirifu huo kufidia hasara hiyo kwa kuwaandikia *surcharge* kwa mujibu wa iliyokuwa sheria ya vyama vya ushirika Na. 15 ya 1991.

Hata hivyo viongozi hao walikata rufaa katika Mahakama Kuu wakipinga amri iliyotolewa na Mrajis Msaidizi ya kuwataka kurejesha fedha ili kufidia hasara waliyodaiwa kusababisha. Miongoni mwa viongozi waliopinga adhabu hiyo ni pamoja na wale wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Mwika - *North East* ambao wanadaiwa kiasi cha shilingi 23,181,196/= na eneo hili ndiyo analotoka Mheshimiwa Mbunge.

Katika rufaa hiyo Mahakama Kuu, ilitengua uamuzi wa Mrajis Msaidizi kwa misingi kwamba surcharge hiyo ilipaswa kutolewa na Mrajis mwenyewe. Wakati wa kutenguliwa kwa uamuzi huo Sheria ya Ushirika aliyokuwa ameitumia Mrajis Msaidizi ilikwishasitishwa kutumika kusubiri kuanza kutumika kwa sheria mpya Na. 20 ya 2003.

Hivi sasa Wizara yangu inaandaa taratibu za kuwachukulia hatua wahusika hao kwa kuwaandikia *surcharge* upya kwa mujibu wa sheria mpya ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2004 ambazo zote zimekamilika na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, hatua zote hizi zinazochukuliwa na Serikali zina lengo la kuvilinda Vyama vya Ushirika na mali za wanachama wake na ndiyo maana taarifa hizo za ukaguzi zilikuwa wazi kwa kila mtu kujua yaliyotokea ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Mbunge mwenyewe.

Kwa hiyo, naomba nisikubaliane kabisa na madai ya Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara yangu na Serikali kwa jumla inawaficha na kuwalinda wezi.

Aidha Wizara yangu haina ushahidi wala takwimu zozote zinazoelezea kiasi chochote cha hongo kilichopokelewa Wizarani ili kuwalinda wahalifu katika vyama vya Ushirika popote pale nchini katika miaka aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

Ninaomba kama anazo taarifa hizo asisite kuzifikisha katika vyombo vinavyohusika ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali gumu limejibiwa na mwenyewe ameridhika kwa hiyo, tunaendelea na swali la mwisho kwa leo.

Na. 30

**Soko Kwa Zao la Pamba**

**MHE. JAMES PHILIPO MUSALIKA** aliuliza:

Kwa kuwa bei ya zao la pamba katika soko la ndani hutegemea mwenendo wa bei ya zao hilo katika soko la dunia; na kwa kuwa, katika msimu huu wa 2004/2005 mabadiliko ya bei katika soko la dunia yamesababisha bei ya zao hilo kubadilika mara kwa mara katika soko la dnaini na hivyo kuwakatiksha tamaa wakulima wa zao hilo:-

(a) Je, soko la dunia liko wapi linaanza mwezi gani na ni akina nani wanunuzi na wauzaji wakubwa wa pamba na Tanzania inauza asilimia ngapi katika soko hilo?

(b) Je, Serikali inaweza kutoa mwenendo wa zao hilo katika soko la dunia kuanzia mwezi Machi, 2005 hadi Juni, 2005 wakati pamba ya Tanzania itaanza kuuzwa katika soko la ndani katika msimu ujao?

(c) Kwa kuwa, Kampuni za wanunuzi wa pamba ziliagizwa na Serikali zilipe mapunjo ya bei kwa wakulima na kwa kuwa Kampuni hizo hazijafanya hivyo kwa kisingizio kwamba ama bado wanahakiki madai hayo au Halmashauri husiks ikiwemo ya Geita hawajapeleka mchanganuo wa mada na kadhalika. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa tatizo hilo na kwa wanunuzi na Halmashauri hizo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, masoko Makuu ya Pamba duniani yako nchini Marekani na Ujerumani. Lakini pamba yetu hununuliwa na Makampuni mbalimbali na kusafirishwa kwa wingi katika nchi za Ujerumani, Ureno, Indonesia, Singapore, Malaysia, Kenya, Burundi na Rwanda. Masoko hayo yanafanya kazi kipindi chote cha mwaka. Orodha ya Makampuni ya wanunuzi na wauzaji wakubwa wa pamba ya Tanzania imeambatanishwa na wajibu ya swali hili ambayo nitampatia Mheshimiwa Mbunge na kuisambaza kwa Waheshimiwa wote. Takribani asilimia 80 ya pamba yote inayozalishwa hapa nchini huuzwa nchi za nje na kiasi kilichosalia, yaani asilimia 20 hutumika hapa nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za asasi inayoratibu masuala ya pamba duniani yaani *International Cotton Advisory Committee* ambako Tanzania ni mwanachama, uzalishaji wa pamba duniani unatarajiwa kupungua kwa asilimia 9 kutoka tani 25.43 milioni hadi 23.05 milioni kutokana na hushuka kwa beri ya pamba msimu wa 2004/2005.

Wastani wa bei ya pamba kwa sasa ni senti za Marekani 45 kwa ratili ya pamba nyuzi ikiwa kwenye kiwanda kukiwa na ongezeko la asilimia 15 ikilinganishwa na bei ya senti za Marekani 39 kwa ratili kuanzia mwezi Septemba, 2004. Hata hivyo bei hii inaweza kubadilika wakati wowote kutegemea hali halisi ya soko.

(c) Mheshimiwa Spika, kufuatia kusuasua kwa zoezi la kuwalipa wakulima mapunjo ya bei ya pamba ya msimu uliopita, Serikali kupitia Bodi ya Pamba iliitisha kikao cha pamoja baina ya wanunuzi na viongozi wa Wilaya Jijini Mwanza tarehe 17 Februari, 2005 kuzungumzia hatma ya malipo hayo. Katika kikao hicho ilikubalika, kuwa:-

(i) Uhakiki wa takwimu za mapunjo ya bei ufanyike chini ya Usimamizi wa Wakuu wa Wilaya na uwe umekamilika ifikapo tarehe 15 Machi, 2005.

(ii) Wanunuzi wote wanaodaiwa mapunjo ya bei wawe wamewalipa wakulima ifikapo tarehe 31 Machi, 2005.

(iii) Wanunuzi ambao hawatakuwa wamewalipa wakulima mapunjo ya bei ifikapo tarehe 31 Machi, 2005, hawatashiriki katika biashara ya pamba msimu ujao wa 2005/2006 na kwamba watachukuliwa hatua za kisheria ili kuhakikisha kuwa wakulima wanalipwa haki yao.

Kwa mujibu wa taarifa tulizozipokea kutoka Wilayani, Makampuni 9 kati ya Makampuni 34 yanayodaiwa tayari yamelipa mapunjo ya bei ya jumla shilingi 51,950,936/= katika Wilaya 11 za Geita, Magu, Kwimba, Misungwi, Sengerema, Ilemela, Nyamagana, Bariadi Maswa, Bukombe na Biharamulo.

Kwa hivi sasa Serikali kwa kupitia Bodi ya Pamba inafuatilia kwa uongozi wa Wilaya juu ya utekelezaji wa makubaliano ya kikao hicho ili hatua zinazostahili ziweze kuchukuliwa dhidi ya wanunuzi wote ambao hawajatekeleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musalika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, muda wa kuuliza maswali umeisha. Kwa hiyo tafadhali tufuate Kanuni. Naona unawapiga debe wengi wanataka uulize swali lako. Nakupa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. JAMES PHILLIPO MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na wapiga debe wangu. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa haraka. *(Kicheko)*

Kwa kuwa katika mwaka huu wa fedha Serikali ilitoa ruzuku kwa ajili ya wakulima wa mahindi kwa ajili ya kununulia pembejeo. Na Serikali hiyo hiyo inawasaidia wakulima wa Kahawa kupitia Mfuko wa *STABEX.*

(i) Je, kwa nini Serikali hawasaidii wakulima wa pamba iwape ruzuku kwa ajili ya kununua madawa ya pamba? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa Serikali haipangi ya bei ya zao la pamba kwa mujibu wa soko huria. Lakini wakati ule wanunuzi wanajipanga na kupanga zao la pamba. Je, Serikali inawasaidiaje wakulima wa pamba nao waweze kupanga bei yao kufuatana na gharama za uzalishaji wa zao la pamba? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Musalika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu zuruku ya mahindi aliyosema, nadhani Wabunge wote watakumbuka kwamba wakati Serikali inatoa tamko kuhusu ruzuku hii ilikuwa imelenga moja kwa moja kuhusu ongezeko la chakula ili kuweza kusaidia chakula hapa nchini. Kwa hiyo, haikulenga kwa mazao mengine ya biashara kama ambayo yanahusiana na pamba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika hilo, kulinganisha kwamba kwa sababu wakulima wa mahindi wamepata ruzuku kwa hivyo mazao mengine nayo yapate ruzuku itakuwa siyo sahihi. Kwa sababu lengo lilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunaongeza chakula nchini ndio maana ililenga katika ile mikoa minne inayozalisha chakula kwa wingi nchini.

Mheshimiwa Spika, la pili; kuhusu la bei. Tumeshasema mara nyingi hapa kwamba wanunuzi binafsi wanapokaa pamoja kupanga bei kwa kweli wanakiuka utaratibu. Kwa sababu hiyo si kawaida kwani wanatakiwa waende kwenye soko huria ili waweze kushindana kwa hurio uliyo wazi. Kwa hiyo, suala la kwamba wakulima pengine nao wangekaa wangeweza wakapanga bei yao, hiyo itawezekana kama wakulima wanaweza wakaungana katika vyama vyao vya Ushirika na kuweza kuhakikisha kwamba mazao yao yanauzwa kwa pamoja. Hiyo itawapa nguvu ambayo tunaita *collective bargain* badala ya kusubiri waweze kuyauza mazao yao kwa mkulima mmoja mmoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Hakuna matangazo ya vikao vya Kamati wala mengineyo. Kwa hiyo, tunaendelea na *Order Paper* kama ilivyopangwa.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Miswada ya Sheria ya Uendeshaji wa Vyuo Vikuu wa Mwaka 2005. *(The Universities Bill, 2005)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja jiandae tu ili Waheshimiwa wanaokwenda kunywa chai waondoke. Halafu nikuite utoe hoja yako.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote ningependa kuungana na wenzangu kutoa rambirambi zangu kutokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Raraleo Marehemu Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria. Aidha napenda kutoa rambirambi zangu kutokana na kifo cha aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Marehemu Balozi Paul Bomani. Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amina*

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Vyuo Vikuu, yamekamilika sasa. Na Muswada huu unawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu ili kusomwa kwa Mara ya Pili na hatua nyingine zitakazofuata.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wale wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu yote yaliyohusu ukamilishaji wa Muswada huu. Nawashukuru wataalam na wadau wote waliohusika katika utayarishaji na utoaji wa mawazo na mapendekezo ambayo yaliboresha` maeneo mbalimbali ya Muswada huu. Aidha shukrani zangu ziwafikie Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Huduma za Jamii chini ya uongozi Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki (CCM), kwa uchambuzi na ushauri wao wa makini.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Elimu ya Juu ya Mwaka 1995, inabainisha umuhimu wa kuwepo Sheria mama itakayoongoza Utoaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Elimu ya Juu. Muswada unaowasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu ni Utekelezaji wa Sera hiyo. Madhumuni ya maudhui ya Muswada wa Sheria ya Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Vyuo Vikuu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Vyuo Vikuu inayounda Tume ya Vyuo Vikuu itakayoweka utaratibu bora za Uanzishaji, Uendeshaji na Uongozi wa Vyuo Vikuu. Aidha Sheria hii inapendekeza kuundwa kwa utaratibu mpya wa kuanzisha Vyuo Vikuu kwa kutumia Hati yaani *Charter.* Kuvipa Vyuo mamlaka zaidi ya kuendesha mambo yao na kuondoa mwingiliano wa mamlaka baina ya Sheria Na. (10) ya mwaka 1995 iliyounda Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu na Sheria zilizounda Vyuo Vikuu vya Umma.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Muswada huu yanatokana na kuwepo kwa mabadiliko na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia Ulimwenguni. Mabadiliko ya kiuchumi ambayo yanahitaji utaalam mpya.

Kwa upande mwingine kumekuwepo na ongezeko kubwa la watu kutaka kupata elimu ya juu. Kwa sababu hiyo, Serikali imeamua kuanzisha na kuweka mazingira mazuri ya kupanda elimu ya juu kwa kutoa fursa zaidi kwa sekta binafsi kuanzisha Vyuo Vikuu ili kukidhi mahitaji ya jamii yetu. Kazi hii chini ya Usimamizi wa Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu imefanyika vizuri. Hata hivyo kumekukwepo ugumu wa kusimamia ubora wa elimu itolewayo katika Vyuo Vikuu vya Umma kutokana na mwingiliano wa Sheria zilizoanzisha Vyuo Vikuu hivyo na ile Sheria ya Baraza.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii inapendekeza kuboresha muundo na mamlaka ya Baraza kwa kuanzisha Tume ya Vyuo Vikuu na kuvipatia Vyuo Vikuu uhuru na uwajibikaji zaidi katika kutekeleza majukumu yake. Aidha Sheria hii inafuta Sheria iliyounda Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu. Angalia marekebisho ya Sheria ya mwaka 1995 ya Sheria Na. (10) ya mwaka 1978. Mpangilio wa Muswada. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Saba. Sehemu ya Kwanza; yenye Ibara (1 - 3) inahusu Masharti ya Utangulizi. Sehemu ya Pili; yenye Ibara ya (4 - 18) inahusu

Masharti ya Uundwaji wa Tume ya Vyuo Vikuu na Kamati zake. Aidha sehemu hii inahusu Muundo, Madaraka, Majukumu, Wafanyakazi na Masuala ya Fedha ya Tume.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada; yenye Ibara ya (19 - 20) inahusu utaratibu na aina ya Vyuo vinavyoanzishwa. Tunzo zinazotolewa na Vyeo vya Watumishi katika Vyuo hivyo. Sehemu ya Nne; yenye Ibara (21 - 23) inaainisha Masharti yanayohusu Utaratibu Mpya wa Kuanzisha Vyuo Vikuu kwa kutumia Hati yaani *Charter* au Katiba. Vile vile katika Ibara hii, Tume ya Elimu ya Vyuo Vikuu imepewa mamlaka ya kutoa Ithibati au Idhini au kutotoa idhini juu ya ombi la kuanzisha Chuo Kikuu kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa. Kusitisha kwa muda au kufuta leseni ya utoaji wa elimu ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano; yenye Ibara ya (34 - 47) inahusu Mambo ya Kiutawala na Muundo wa Vyuo Vikuu. Muswada unapendekeza kuwepo kwa Mkuu wa Chuo yaani *Chancellor* ambaye anaweza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Vyuo Vikuu vya Umma kwa Tanzania Bara au Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Vyuo Vikuu vya Umma vya Tanzania - Zanzibar au mtu mwingine yeyote atayeteuliwa na Rais. Kwa Vyuo Vikuu vya Binafsi, Mkuu wa Chuo atateuliwa na Mmiliki wa Chuo Kikuu Husika. Sehemu hii pia inahusu kuwepo kwa Makamu Mkuu wa Chuo atakayeteuliwa na Mkuu wa Chuo kwa Vyuo Vikuu vya Umma au Mmiliki wa Vyuo Vikuu vya Binafsi baada ya nafasi hiyo kutangazwa.

Aidha nafasi nyingine za uongozi katika Vyuo Vikuu pia zitatangazwa. Nafasi hizo ni kama ifuatavyo:-

Naibu wa Makamu Mkuu wa Chuo;
Mkuu wa Chuo Kikuu Kishiriki;
Msajili wa Chuo Kikuu.

Masharti mengine muhimu katika sehemu hii yanahusu kuwepo kwa Chombo Kikuu cha Kusimamia Utawala wa Chuo Kikuu ambacho ni Baraza au Bodi ya Uongozi *(Council or Governing Board)* na *Senator* au Kamati ya Taaluma *(Academic Committee)* kulingana na aina au ngazi ya Chuo Husika.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita; yenye Ibara (48 - 51) inafafanua masuala yanayohusu Jumuiya ya Wafanyakazi na Wanafunzi, Utawala na Ustawi wa Wanafunzi. Chini ya mapendekezo haya, shughuli za Vyama vya Kisiasa katika maeneo ya Vyuo Vikuu zimepigwa marufuku kwa sababu kama zinazojulikana. Sehemu ya Saba; yenye Ibara (52 - 62) inahusu Mambo Mengineyo ya Jumla yakiwemo Uanzishwaji, Majukumu na Madaraka ya Kamati ya Makamu Wakuu wa Vyuo na Wakuu wa Vyuo Vikuu Vishiriki. Sehemu hii pia inaainisha mamlaka aliyopewa Waziri juu ya kutengeneza Kanuni. Sheria zinazofutwa kutokana na kutungwa kwa Sheria hii, taratibu za Vikao vya Tume na Kamati mbalimbali za Mkuu wa Chuo ni mambo muhimu yaliyoanishwa katika jedwali chini ya Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba sasa kuwasilisha rasmi Muswada wa Sheria ya Vyuo Vikuu wa mwaka 2005 pamoja na Jedwali la Marekebisho ya Muswada huu kwa ajili ya kusomwa kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA BIASHARA NA VIWANDA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa kwa utaratibu wetu wa kawaida namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii ili ichambue Muswada huu ili atoe maoni ya Kamati.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI ZA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 *(The Universities Act 2005).*

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada utakaodhibiti Uendeshaji wa Vyuo Vikuu hapa nchini. Taifa letu linahitaji kupanua elimu ya juu ili vijana wengi wapate elimu hiyo itakayowawezesha kuhimili ushindani katika dunia hii ya utandawazi. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imeruhusu watu na Taasisi Binafsi zenye uwezo wa kuanzisha Vyuo Vikuu kufanya hivyo. Kwa hiyo, Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka kwa kuwa unalenga kudhibiti ubora na viwango vya taaluma itakayotolewa na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, Tume hii inayokusudiwa kuanzishwa itaboresha majukumu ya awali yaliyokuwa yakitekelezwa na Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu kama ilivyotajwa kwenye Muswada ikiwa ni pamoja na kumshauri Waziri juu ya jambo lolote linalohusu elimu ya juu. Kukagua mara kwa mara ubora wa elimu ya Vyuo Vikuu, kutoa mwongozo na kudhibiti Bajeti ya Vyuo vya Umma, kukusanya, kuchambua na kutunza na kuchapisha taarifa zinazohusu elimu ya juu na utafiti. Na vile vile kusimamia raslimali zinazotolewa na Vyuo Vikuu kwa ajili ya maendeleo ya kitaaluma. Kuhimiza uzalendo na umoja wa kitaifa na utambulisho wa Vyuo Vikuu. Vile vile kuhimiza usawa wa kijinsia katika Vyuo Vikuu. Kuratibu mahusiano baina ya Vyuo Vikuu nchini na nchi za nje na kutafuta fedha na kuzigawa miongoni mwa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho; ni kuthibiti ubora wa elimu katika Vyuo Vikuu ikiwemo kuwa na vigezo vinavyofanana katika ubora huu ili Vyuo Vikuu vyote viwe na adhi sawa kitaaluma. Kwa mujibu wa Kanuni ya (88) Kifungu cha (6) ya Kanuni za Bunge ya Toleo la 2005, Kamati ilishikirisha wadau mbalimbali ambayo walitoa maoni yao katika kuboresha Muswada huu. Wadau hao walitoka katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu za Serikali na za Binafsi Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Naomba niwataje kama ifuatavyo:- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Chuo Kikuu cha Serikali ya Zanzibar, Chuo Kikuu cha Tumaini, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - Dodoma, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo Kikuu Aghakhan, Chuo cha Ustawi wa Jamii Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu wa Majengo, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu Kishiriki cha Muhimbili. Chuo Kikuu Kishiriki cha Bugando, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Herbet Kairuki, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika - Moshi na Stadi za Biashara - Moshi, Chuo cha *IMTU.* Chuo cha Jamii Kivukoni na Chama cha Wafanyakazi katika Asasi na Taasisi za Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadili Muswada huu kwa kina, ikiwemo kuzingatia maoni ya wadau, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Katika Sehemu ya Pili ya Muswada, Ibara ya (5) inayoelezea kazi za Tume. Kamati inapendekeza kwamba Ibara Ndogo ya (5) Kifungu cha (1)(d) liongezwe neno *Consultancy* yaani ushauri ili kazi za Tume iwe ni pamoja na kusimamia utoaji wa elimu, utafiti na ushauri. Na Ibara Ndogo ya (5), Kifungu cha (1) (4) liongezwe neno programme yaani course ili kazi ya Tume iwe ni pamoja na kuandaa utaratibu wa namna ya wanafunzi kuhama kutoka chuo hicho hicho kimoja kwenda kingine na kutoka *course* moja kwenda nyingine. Ibara ya (5) Kifungu cha (1) (j) katika Sehemu ya Tano, yaongezwe maneno *outside the country* yaani nje ya nchi ili kazi ya Tume iwe ni kuhamasisha ushirikiano baina ya Vyuo Vikuu ndani na nje ya nchi. Mbali na kazi za Tume zilizoorodheshwa katika Ibara ya (5), Kamati vile vile inashauri Tume ifanye kazi zingine ambazo ni kuanzisha au kushiriki kuona vigezo vya ubora wa Vyuo Vikuu na kulinda vigezo hivyo. Ibara ya (9) Kifungu cha (4), Kamati inashauri idadi ya Kamati zitakazoundwa na Tume, zisitajwe kwenye Sheria bali idadi ya Kamati itokane na umuhimu wa Kamati hizo kadri itakavyoonekana inafaa.

Ibara ya (13) Kifungu cha (1), Kamati inashauri uteuzi wa Katibu Mtendaji wa Tume, uwe wa uwazi na nafasi hiyo itangazwe na kushindaniwa. Na Ibara ya (8) Kifungu cha (3) (b), Kamati inashauri kuwa, Taasisi itakayotoa taarifa za uongo mbele ya Tume ipewe adhabu ya angalau shilingi 1,000,000/= (millioni moja) za Kitanzania badala ya shilingi 500,000/= (laki tano) zilizoonyeshwa kwenye Muswada ambazo tunadhani ni kidogo mno. Kwenye Ibara ya (20) Kifungu cha (1) Sehemu ya Tano, Kamati inashauri Vyeo vya Wakutubi viongezwe na kuorodheshwa kama ilivyo kwa Wana-taaluma wengine. Aidha Cheo cha Mhadhiri-Mwanafunzi *Tutorial Assistant* kirejeshwe ili kuwa na taratibu endelevu wa kupata wahadhiri wa Vyuo Vikuu na vyeo vinavyohusika navyo vitajwe.

Ibara ya (36) Kifungu cha (1 - 3), Kamati inashauri kuwa Makamu wa Mkuu wa Chuo ateuliwe baada ya ushauri wa *Senator* na Baraza la Chuo badala ya ushauri wa Baraza pekee. Aidha utaratibu huu utumike pia wakati wa uteuzi wa Naibu wa Makamu wa Mkuu wa Chuo. Ibara ya (39) Kifungu cha (3 na 40) (3 na 6), tunashauri vyeo viainishwe kwenye Sheria. Sehemu ya Saba ya Muswada Ibara ya (51) Kifungu cha (1) (a); Kamati inashauri kuwa Wakurugenzi wa Idara wawe na uwezo wa kuwasiliana na

Kamati ya Makamu, Wakuu wa Vyuo na Makamu Wakuu wa Vyuo. Aidha uteuzi wa ngazi zote uzingatie masharti ya Utumishi wa Umma na uwazi. Kwenye Ibara ya (3) kwenye *first schedule* inayohusu Muundo wa Tume, Kamati inashauri kuwa; Vyama vya Wafanyakazi vishirikishwe katika Tume hii itakapoundwa.

Ibara ya (61) Kifungu cha (3 na 4) sehemu ya Kwanza, Kamati inashauri kuwa, Watumishi wote wa Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu wawe Watumishi wa Tume ya Vyuo Vikuu wakati wa kipindi cha mpito katika kutekeleza Sheria itakapopita. Na Ibara ya (51) ambayo inakataza shughuli zozote za Kisiasa kufanywa na umoja wa Wana-taaluma na wanafunzi katika maeneo ya Vyuo Vikuu. Kamati inashauri kuwa, Sheria itamke vile vile adhabu itakayotolewa kwa watakaokiuka Sheria hii. Pamoja na ushauri na maoni haya, Kamati inaamini kuwa Serikali itafanya marekebisho hayo kwa lengo la kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa mara nyingine natoa shukrani kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii, mbele ya Bunge lako Tukufu. Vile vile naomba pia nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa umakini wao wakati wa kujadili Muswada huu. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kushiriki wakati wa vikao vya Kamati. Aidha natoa pongezi kwa Mheshimiwa Pius Y. Ng'wandu, Mbunge na Waziri wa Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mbunge na Naibu Waziri wa Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Maofisa mbalimbali kwa kuwasilisha Muswada mbele ya Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Baada ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, wasemaji wanne wa kwanza watakaochangia ni Mheshimiwa Prof. Diamon M. Mwaga, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala na Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo, tafadhali wajiandae.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani hapa Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Tume ya Vyuo Vikuu *(The Universities Act 2005).*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara ya Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu na Serikali kwa kuletwa Muswada huu Bungeni. Imeelezwa kuwa madhumuni ya sababu za kutunga Sheria hii ni ili kuweka utaratibu au mfumo mmoja utakaouweka utaratibu wa kuanzisha na kuendesha Vyuo Vikuu nchini hasa kwa kuzingatia kuwa idadi ya Vyuo Vikuu inaongezeka ikiwemo ile ya Vyuo Vikuu vya Umma na vile vya Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inaelewa kuwa kila ilipotakiwa kuanzisha Chuo Kikuu hapa Tanzania, ilikuwa inalazimisha Chuo hicho kitungiwe Sheria yake hapa Bungeni.

Hii ilisababisha Sheria hizo kutofautiana kutoka Chuo hadi Chuo. Na kwa vile vya Binafsi taratibu zake hazikuoana na zile za Vyuo Vikuu vya Umma. Kwa madhumuni ya kuwa na chombo kimoja cha kisheria na Sheria moja inayoelekeza jinsi ya kuanzisha na kuendesha, Vyuo Vikuu nchini Tanzania, Kambi ya Upinzani inaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kuwa Wizara na Kamati ya Huduma za Jamii iliwaalika wadau mbalimbali kutoka Vyuo vyote Vikuu Tanzania, Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu, Viongozi wa Serikali za Wanafunzi, Baraza la Ithibati, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Baraza la Vyuo vya Ufundi Tanzania wote walihudhuria na kutoa maoni yao ambayo ndio yalipelekea kuletwa kwa mabadiliko yaliyowasilishwa na Muswada huu leo asubuhi.

Kwa kuwa wengi wa wadau walihusika katika kutoa maoni yao ni Watumishi au waajiriwa wa Serikali. Kuna hoja pengine walikuwa wanaogopa kuzigusa. Sasa ni katika zile hoja au sehemu ambazo hazikuguswa au ziliguswa lakini hazikuzingatiwa katika marekebisho ya Muswada ambako Kambi ya Upinzani inatoa maoni na mapendekezo yake.

Mheshmiwa Spika, Sehemu ya Kwanza inayohusu tafsiri ya maneno. Tunapendekeza kuongeza maneno: *Student Organisation,* na tunapendekeza itafsiriwe hivi:-

*Student Organisation means an organ representative of the University Student of University, University College made under section (19) also it means an Appex Organisation of Students Organisations of all Universities and University Colleges.*

Kama kuna Chama cha Wanafunzi ama Serikali ya Wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mzumbe na kadhalika waungane kwa pamoja na kuunda chombo ambacho ni cha jumla kwa nchi nzima.

Kambi ya Upinzani inapendekeza tafsiri hii kwa sababu tunaona umuhimu wa kuwepo Muungano wa Kitaifa wa Serikali za wanafunzi wa Vyuo Vikuu kwa sababu zifuatazo:-

(i) Mahitaji ya dhana za ushirikishwaji wadau katika vyombo mbalimbali vya maamuzi vinahitaji chombo hiki.

(ii) Hata muswada huu unapendekeza kuwepo kwa Kamati au chombo kinachounganisha Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu *Vice- Chancellors and Principals Committee.*

(iii) Sababu ya uzoefu uliojitokeza hii imetokana na pale ambapo Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu alipotakiwa kisheria kuteua mwakilishi wa wanafunzi wa Vyuo Vikuu kwenye Bodi ya Mfuko wa Mikopo ya Wanafunzi iliyofunguliwa hivi karibuni.

Nadhani alishindwa kumteua mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu kimoja, kwa mfano Mzumbe kwa kukosa vigezo vya kufuata wakati wa uteuzi huo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa Sheria unaopendekezwa kuanzishwa, utaihusisha Zanzibar, lakini haufuti Sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu cha Zanzibar yaani *State University of Zanzibar Act.No. 8 of 1999.*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sheria hiyo nadhani itakuwa kwenye maeneo haya kwa sababu walipoileta sikuwapo, lakini baadaye nitaitafuta tuseme ni ya namba ngapi, ya mwaka gani na Serikali ilijua uvunaji wa Katibu ya Muungano uliofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutunga Sheria hiyo na kuanzisha chuo hicho *The State University of Zanzibar.* Hii ni kwa sababu suala la elimu ya juu ni la Muungano. Lipo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tangu kitendo hicho kifanyike Serikali zote mbili zimefumba macho huku zikijua kuwa Katiba ya nchi imevunjwa.

Mheshimiwa Spika, kambi ya Upinzani inajua kuwa kihistoria Vyuo Vikuu vyote na vile vya elimu ya juu vilijengwa sehemu moja ya Muungano. Mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine, *Muhimbili University,* kilichokuwa Chuo cha Ardhi, Chuo cha Usimamizi wa Fedha na Vyuo vingine vyote halali huko Zanzibar hakukuwa na Chuo Kikuu kamili na hali hii kwa kiasi ilisababishwa kutoridhika kwa watu wa Zanzibar.

Hivyo ni haki kuwepo kwa Chuo Kikuu kamili huko Zanzibar lakini siyo kwa njia za kuvunja Sheria za nchi na Katiba ya nchi. Kwani kama kitu hicho kingetungiwa Sheria na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kambi ya Upinzani inaomba Serikali itoe maelezo ya kina vingenevyo ijiuzulu kwa sababu haikulinda Katiba ya nchi na adhabu muafaka ni kujiuzulu tu.

Katika sehemu (2) Ibara (4) Ibara ndogo ya (3) kuhusu idadi ya wajumbe wa tume kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la kwanza. Tunapendekeza kuongeza vipengele viwili, kimoja kipengele (L) ambacho kinaonyesha *One Member of the House of Representative Recommended by the Houses of Representatives From amongst Members.*

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza hivyo kwa sababu wale wajumbe makamishina hakukuwa na mwakilishi kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Japo kuna Wawakilishi wawili huteuliwa na Serikali ya Zanzibar, sasa wabaki vilevile lakini kiongezwe na hiki ili iwezekane kutoka mjumbe mmoja kule.

Pili tunapendekeza kuwa kiongezwe kipengele kingine (M) na kisomeke hivi: *Two Representatives From the Appex Organisation of the University Students Organisation* ili wanafunzi waweze kupata uwakilishi. Walikuwa hawakupata uwakilishi katika kamisheni hiyo. Hii ni kwa sababu wanafunzi wa vyuo vikuu hawakuwakilishwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya (5) Ibara ya (35) Ibara ndogo ya (1) inapendekezwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Rais wa Zanzibar, wawe wakuu wa Vyuo Vikuu Vya Umma. Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Ibara hii ifutwe na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, abaki na mamlaka ya kuteua tu wakuu wa Vyuo Vikuu Vya Umma ambao nao watateua Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu Vya Umma.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaelewa zana ya kuwepo kwenye Sheria nyingi za Vyuo Vikuu Vya Umma, sharti la Rais wa nchi kuwa mkuu wa Vyuo Vikuu, hii ni kutokana na sababu zifuatavyo:-

(1) Wakati wa miaka ya 60, miaka ya 70, miaka ya 80 kuwepo kwa mawazo ya kimapinduzi *Marxism Leninsm* katika vyuo vikuu. Huku wanafunzi na walimu wa vyuo vikuu wakionekana kuunga mkono mawazo hayo. Basi ilionekana kuwa Vyuo Vikuu vilikuwa kitovu cha kuchochea mapinduzi hata yale ya kijeshi. Hivyo kuwa na ulazima wa kuwa mkuu wa nchi awe ndiye mkuu wa Vyuo Vikuu katika nchi yake.

(2) Vyuo vikuu vilikuwa vichache mno na ukubwa wa Serikali ulikuwa mdogo hivyo Rais alikuwa anapata muda wa kutosha kujishughulisha na shughuli za Chuo Kikuu.

(3) Hakukuwepo Vyuo Vikuu binafsi katika nchi nyingi za Kiafrika.

Kwanza kwa sasa hali hii imebadilika Vyuo Vikuu Vya Umma vinaongezeka na vyuo vikuu binafsi vinaongezeka na Rais anakuwa na shughuli nyingi zikiwemo za utandawazi, demokrasia, masuala ya ugaidi, utawala bora na kadhalika. Kwa hiyo, Rais apunguziwe mzigo huu kutokana na shughuli zake nyingi na muhimu zaidi.

Pili kwa kuwa watu wasio Rais wa nchi wanaruhusiwa kuwa Wakuu wa Vyuo Vikuu na hakuna kinachoharibika. Basi Rais aendelee kuwateua wakuu hao na wao wawateue Makamu Wakuu wa Vyuo.

Tatu panapotokea Rais wa nchi ni Mkuu wa Chuo Kikuu fulani na akamteua makamu mkuu wa chuo hicho na wakati huo huo Mkuu wa Chuo Kikuu kingine anamteua makamu mkuu wa chuo hicho, makamu wakuu hao wa vyuo vikuu wawili wanatofautiana na hii ni kasoro kwa sababu:-

(1) Makamu Mkuu wa Chuo ambaye mkuu wake wa chuo anakuwa ni Rais ana nafasi ya kuonana moja kwa moja na Mheshimiwa Rais na wengine hawapati unafuu huo.

(2) Hata wanafunzi wa Chuo Kikuu ambao mkuu wao au mkuu wa chuo hicho ni Rais ikitokea wakataka kumuona Rais na wakakwama kwa sababu za kiitifaki wataelekeza mashambulizi kwa mkuu huyo wa chuo ambaye ni Rais na ushahidi tunao. Ni kutokana na ukweli huo inapendekezwa Rais asiwe mkuu wa Chuo Kikuu chochote Cha Umma.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya Muswada Ibara (36) Ibara ndogo ya (2) inapendekezwa kuwa Makamu mkuu wa Chuo Kikuu Cha Umma ateuliwe na mkuu wa chuo badala ya kushauriana na baraza la chuo. Kambi ya Upinzani inaona kuna utata katika hatua hizi na swali ni je, katika kuanzisha Chuo Kikuu kinachoanza kinachokuwepo kwanza ni baraza la chuo au Makamu Mkuu wa Chuo.

Je, kwa vile imependekezwa pia kuwa hata *SENATE* Chuo Kikuu ihusike kutoa mapendekezo katika mchakato mzima wa uteuzi makamu mkuu wa chuo. Je, yeye kama mtendaji mkuu *Chief Executive* haitampa matatizo katika kusimamia nidhamu kwa watu waliompendekeza. Je, isingekuwa vyema uhuru wa uteuzi akaachiwa mwenye chuo au mkuu wa chuo na ili kumdhibiti makamu mkuu wa chuo asiyejali maslahi ya jumuiya ya wanachuo, malalamiko yaanze kwa wanafunzi, *SENATE* baraza la chuo hadi kwa mwenye chuo au mkuu wa chuo.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya (4) Ibara ya (29) Ibara ndogo ya (4) inayosomeka: *"Where the charter is revoked under this section, the Commission Shall make arrangement for re-admitting of existing Student in some other Universities".* Hii ni katika *revocation of charter.* Sasa sababu zimetajwa kwa nini ile *chart* inaweza kuwa *revoked,* sasa tunapendekeza iongezwe Ibara ndogo ya (5) itakayotoa adhabu kwa aliyeanzisha chuo na kushindwa kukiendesha na kuwapotezea wanafunzi muda na pesa zao. Hii ni kwa sababu zifuatazo:-

(1) Itabidi wanafunzi hao wahamishiwe kwenye Vyuo Vikuu vya Serikali na kuongeza gharama.

(2) Amepoteza muda na karo ya wanafunzi wa chuo chake.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa ni busara kama mali au majengo ya chuo ambacho kimefutiwa hati au kibali kwa sababu zilizohainishwa kwenye Sheria hii yataifishwe. Vinginevyo kutakuwepo na mchezo kama wa kuanzisha chuo kama vile cha *Bukoba University* au ulaghai uliojitokeza kwenye *TTCL* au Shirika la Ndege au *Sheraton* watu wanabadilishana kwa kuwa Sheria sasa inawapa woga wa kukianzisha halafu baadaye anakiacha na anajua Serikali itakichukua hatajua hana cha kupoteza wakati ameshakusanya pesa na kujiondokea.

Mheshimiwa spika, katika sehemu ya (6) ya Muswada Ibara (49) tunapendekeza iongezwe Ibara ndogo ya (5) mbali na kuhusu ile *appex* ya wanafunzi na isomeke *The Constitution of Appex Organisation to be Approved by the Tanzania Council of Universities.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa mapendekezo mengine ya jumla kama ifuatavyo.

Kumekuwa na wimbi la kupandisha vyuo na taasisi za elimu ya juu kuwa vyuo vikuu. Hatuna tatizo na harakati hizo ila tuna wasiwasi kuhusu kuto jengwa vyuo vingine vya kuchukua kazi zilizokuwa zikifanywa na vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, utajua kuunganisha Chuo Cha Ushirika na vingine, lakini hakuna anayejenga vyuo kwa ajili ya kufanya zile kazi na kutoa taaluma zilizokuwa zikitolewa na vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, pili Serikali iangalie utaratibu wa kuvipa vyuo vikuu pesa za kutosha na kwa kufuata kanuni ya idadi ya wanafunzi walioko katika vyuo hivyo. Kwa maana ya kwamba *Student Unit Cost* angalieni wanafunzi wangapi halafu wapate hela ngapi kuliko inavyotoa kwa sasa. Kwa sababu kuna wengine wanapata hela nyingi wakati wana wanafunzi kidogo na wengi wanapata kidogo wakati wana wanafunzi wengi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iingilie kati tangazo la Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, la kuingiza Vyuo Vikuu wanafunzi waliomaliza kidato cha sita mwaka huu kama hakuna maandilizi kwenye vyuo hivi ili kuwapokea wanafunzi hao. Nakupa mfano, hakuna nyumba za kutosha kwa ajili ya vyumba vya kutosha vya mihadhara wala madawati, wala maabara.

Hakuna mabweni ya kutosha, hakuna vifaa vya kufundishia vya kutosha, hakuna walimu wa kutosha. Hata hivyo, kuna idadi kubwa ya waliohitimu miaka iliyopita wanastahili kwenda vyuo vikuu lakini sasa watalazimika kushindania nafasi kidogo zilizopo kwenye vyuo vikuu, na hii ina maana yake kwa utaratibu wa zamani kama walio na sifa za kwenda vyuo vikuu ni 15,000 na sasa wameongezeka 15,000 waliomaliza mwaka huu, jumla watakuwa 30,000. wakati huo huo vyuo vikuu vinauwezo wa kupokea wanafunzi 15,0000. Katika utaratibu huu inakuwa ni fujo kwa sababu kuna wengine watabaki wakati walikuwa na haki ya kwenda pale. Kambi ya upinzani inaoiomba Serikali itoe kauli humu Bungeni kuhusu jambo hili.

Nne tunaiomba Serikali hasa Wizara ya Ujenzi pamoja na Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam waharakishe kutoa kibali cha upanuzi na ujenzi wa barabara ya Sam Nujoma ili kuharakisha mradi wa ujenzi mlimani *City Centre* ili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiweze kunufaika na mradi huo.

Tunapendekeza Serikali kujiuzulu katika sakata la uvunjaji wa Katiba wakati wa uanzishwaji wa *State University of Zanzibar.* Sasa kwa kuwa Serikali inaweza kutumia nguvu kukataa kujiuzulu basi wakati njia za kuwajibisha zikitafutwa itoe kauli Bungeni kuhusu msimamo wa kisheria juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza jendwali la (3) kiongezwe kifungu Ibara ndogo ya F inayofuta Sheria ya kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kama mabadiliko hayo yaliyopendekezwa yatakubaliwa tutaunga mkono Muswada huu. Napenda kuwasilisha asante. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Muswada huu unaokusudiwa kutunga Sheria itakayoweka utaratibu wa kuanzisha Tume ya Vyuo Vikuu vya 2005, *The Universities Act 2005.* Kabla sijachangia niungane na Wabunge wenzangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibakwe kutoa pole kwa ndugu wa Marehemu wa Balozi Ahmed Hassan Diria na Balozi Paul Bomani, Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa sababu, Muswada huu ulioko mbele yetu unakusudia kuunda chombo ambacho kitaratibu na kuwiainisha aina na viwango vya elimu ya juu na kuweka utaratibu mzuri wa uendeshaji wa vyuo vikuu. Kwa hiyo, ni jambo la kupongezwa, ni jambo ambalo huko nyuma hakukuwepo utaratibu mzuri wa kuwiainisha aina na viwango vya elimu ya juu. Hata uendeshaji wa vyuo vikuu wenyewe ulikuwa hauna udhibiti unaofaa. Kwa Muswada huu matatizo yaliyokuwepo huko nyuma kwa kiasi kikubwa yatapatiwa ufumbuzi na mimi nina hakika Serikali kwa hatua hiyo itahamasisha na itatoa changamoto kwa wawekezaji mbalimbali kuanzisha vyuo vikuu nchini.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili inahusu masharti ya kuunda tume na Kamati zake na masuala ya wafanyakazi na fedha.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inaelezea kwa kikamilifu muundo na majukumu ya tume na Kamati na nyongeza nne ukienda kule nyuma mwisho kule inaweka kipindi cha mpito na kuhamisha majukumu ya baraza la uthibiti kwenda kwenye chombo hiki kipya. Lakini katika orodha za Sheria zilizoorodheshwa pale kwenye ile orodha ya nyongeza pale hii Sheria ya baraza la zamani hili haikuwemo, Mheshimiwa Waziri kaitaja katika hotuba yake lakini katika nyongeza hapa nafikiri kumekuwa na *omission* ambayo inaweza kuwa ni *typing error.* Lakini kunakuwa na *omission*, kilichoonyeshwa hapa katika nyongeza hii ni ile sheria ya Elimu ya 1978. Lakini ile iliyoanzisha lile baraza la zamani imekuwa *omitted* ingawa Mheshimiwa Waziri kaieleza.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 13 kinahusu Katibu Mtendaji wa Tume, ambacho hakisemwi hapa na mimi ndio napenda nishauri namna anavyopatikana huyu Katibu Mtendaji wa Tume. Nyongeza iliyoletwa inaonyesha sifa za huyu Katibu wa Tume lakini bado jinsi ya kupatikana kunahitaji kuboreshwa zaidi. Habari za nyongeza ya pili inajaribu kuboresha lakini mimi ningeshauri tuboreshe zaidi kwa kuweka utaratibu wa *search committee* ambao tunautumia katika nafasi nyingi muhimu ambazo kwa kweli Miswada mingi iliyopita bungeni hapa tumeaanza kukubali sasa utaratibu wa kuwa na *search committee* katika nafasi muhimu na hivyo basi katika nafasi hii ya Katibu Mtendaji wa Tume tutumie utaratibu huo huo na ionyeshwe katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyakazi wengine Muswada unavipengelea kipindi cha mpito. Ukiangalia ile nyongeza ya nne kuna mambo makubwa mawili yanajitokeza pale.

(1) Ni kwamba wafanyakazi waliokuwemo kwenye baraza lililopita la zamani wataendelea na ajira zao kwenye tume, yaani wanahamia moja kwa moja. Sasa swali tunajiuliza hapa je, wafanyakazi wenyewe walishirikishwa katika uamuzi huu, je, hakuna namna nyingine kwa mfano mfanyakazi angependa kuachana kabisa na baraza akachukua pesa zake akaendelea na shughuli zake. Je, hawezi kupewa *option* hiyo, nafasi hiyo ya kuamua.

(2) Ambalo liko katika nyongeza hiyo huku mwisho, ni kwamba wale ambao hawataajiriwa na tume kifungu cha (4) (2) katika *schedule* ya 4 kinasema kwamba Waziri anahiyari *Absolute Discreation,* kuielekeza tume imlipe mtu huyo kiinua mgongo chake na malipo mengine ambayo Waziri ataona inafaa.

Mheshimiwa Spika, sasa tunajiuliza hapa sasa hivi tumekwishapata uzoefu wa muda mrefu kidogo na wa kutosha kwa kweli juu ya kushughulikia tatizo la wafanyakazi ambao hawaendelei na ajira. Hivi kweli hakuna malipo ya msingi, hakuna haki za msingi za mfanyakazi hataWaziri apende mwenyewe kweli ni haki hiyo. Je, hakuna utaratibu unaoeleweka kiserikali juu ya haki ya mfanyakazi huyu. Lakini mpaka itegemee Waziri anasemaje siku hiyo ameamkaje na anafikiri nini juu ya mfanyakazi huyo. Mimi nafikiri tuna uzoefu mzuri sasa wa kushughulikia matatizo ya wafanyakazi ambao hawaendelei na ajira ya shirika jipya linaloanzishwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu inahusu aina ya vyuo, tuzo na vyeo vya watumishi. Ukiangalia ile sehemu ya tatu ina mlolongo mrefu wa aina ya vyuo. Mimi nasema huu mlolongo mrefu hauna sababu ya msingi kabisa ukitazama. Angalia kwa mfano maana ya *Connected College* na *Affliated College.* Ukisoma ainisho zake ni mstari mwembamba sana umechorwa baina ya aina hizo mbili za vyuo. Ukiangalia *Associated College* na *Constituent College* tofauti yake ni ndogo ndogo sana. Kwa kweli unachoweza kusema hapa ni maneno tu yamebadilishwa yamepangwa vizuri ili kuonyesha kwamba kuna aina nyingi za vyuo.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri Wizara irejee tena katika aina hizi ili ieleze wazi wazi ni aina gani za vyuo vinavyotakiwa kuanzishwa hapa nchini. Lakini kuwa na mlolongo mrefu wa vyuo sita ambavyo maana yake kwa kweli ni ile ile moja havitusaidii sana. Kwa kweli, katika Ibara hii ya (19) sio tu kuna tatizo la aina nyingi ya vyuo, lakini vile vile Muswada hauonyeshi ni namna gani vyuo hivyo vitakavyoweza kuanzishwa, kwa mfano, baada ya kuzungumzia ile sehemu ya 4 ya kuanzishwa Chuo Kikuu ungetegemea kupata sehemu au Ibara ambayo inazungumzia namna ya kuanzisha vile vyuo vingine sita, vinaanzishwaje, ungetegemea kupata katika Muswada huu lakini hupati. Kwa msingi huo mimi nafikiri tume au Wizara ingekaa tena ifikirie ione upya namna ya kurekebisha aina hizi zote na kuona kama kweli ni muhimu kuwa na aina zote hizi za vyuo katika nchi yetu na katika hali ya sasa.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ya tatu inaweka vyeo vya wafanyakazi. Mimi nashukuru nilikuwa na hoja ya *Tutorial Assistant* kwamba kwa nini imeondolewa na nimeona katika nyongeza hapa wameirejesha. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hiyo sina matatizo nayo imewekwa vizuri na ilikuwa inaleta mashaka kidogo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 5 nakubaliana na Ibara ya (35) (2) (a) ya namna ya kumpata Mkuu wa Chuo au wakuu wa vyuo kwa sababu pale imeonyesha wazi kwamba itatumika *Search Committee* na vile vile katika kumpata wakuu wa vyuo vikuu watatumia *search Committee.* Lakini ukienda mbele kule kwa ma-*principals* Wakuu wa Vyuo vingine utaratibu huo unaachwa . Mimi nashauri tuendelee na utaratibu na pengine tuwe na *opening close* pale. Ibara ya jumla tu kusema kwamba utaratibu wa kuwapata Wakuu wa Vyuo vingine uwe wa kutumia *Search Committee.*

Mheshimiwa Spika, mwisho Ibara ya 51 inapiga marufuku mambo ya siasa katika vyuo. Mimi naunga mkono mia kwa mia. Jambo kubwa nafikiri walimu na wanafunzi waelimishwe kwamba wamekwenda pale Chuo Kikuu kusoma, kukuza taaluma, hivyo mambo ya siasa waachiwe wanasiasa wenyewe. Wasubiri mpaka watakapomaliza kuikuza ile taaluma pale Chuo Kikuu. Najua wanayo nafasi kubwa katika kushauri kwa kufanya *consultancies* na utafiti wa masuala mbali mbali. Lakini hiyo peke yake si sifa ya kujiingiza katika siasa wao wenyewe na kuvifanya Vyuo Vikuu mahali ambapo vyama vya siasa vinakimbilia kupata viongozi, kupata wanasiasa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi hili naunga mkono mia kwa mia lakini kama nilivyosema ni vizuri walimu na wanafunzi wakaelimishwa vizuri wakaelewa mantiki au hoja ya msingi inayojengwa katika Muswada huu. Hivyo wafanye yale tu ambayo yanaweza kusaidia katika jamii. Kwa kweli ukiangalia madhumuni ya vyuo vikuu yanatosheleza na yanawapa nafasi nzuri wanataaluma kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu badala ya wao wenyewe kuingia katika siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema tena naunga mkono hoja hii. Hoja ni nzuri imewasilishwa vizuri na itatusaidia kusimamia na kudhibiti uendeshaji wa vyuo vyetu vikuu hapa nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Jimbo la Uchaguzi la Mheshimiwa Omar Mjaka Ali limevunjwa huko Zanzibar, lakini yeye bado ni Mbunge mpaka Bunge litakapovunjwa rasmi na Rais Benjamin Mkapa. *(Kicheko)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Jimbo langu limevunjwa kwa mujibu wa Sheria ya nguvu ya Tume ya Uchaguzi na nasikia pia imepata kwa mujibu wa Rais kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kifungu Na. 75. Kwa hiyo, nakubaliana na maamuzi ya Tume ya Uchaguzi.

**SPIKA:** Na kwamba unaendelea kuwa Mbunge mpaka Bunge litakapovunjwa.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nashukuru kufika kwa Muswada huu na nilichosimama hapa ni kuunga juhudi za Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake. Hili ndilo suala moja kubwa ambalo limenisimamisha hapa ili na mie niweze kuchangia Muswada huu wa Sheria wa uendeshaji wa vyuo vikuu wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia na mimi naomba niungane na wenzangu kutoa pole kwa familia za Marehemu Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria na Marehemu Mheshimiwa Balozi Paul Bomani, kutokana na vifo ambavyo wenzetu wameshatangulia mbele ya haki. Mwenyezi Mungu alaze mahali pema huko peponi na *inshallah* tutakutana siku ya siku kama Mwenyezi Mungu alivyotuagiza.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga Muswada huu mkono kwa asilimia mia kwa mia na kwa kweli kwa kuwa taifa letu linapigania kwenda katika maendeleo nataka tuwaambie wenzetu wa elimu ya juu, kwamba sasa kigezo cha kufikia yale malengo ya taifa letu liko juu yao katika kuliletea taifa hili mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu ndio msingi wa maendeleo wa taifa lolote lile duniani na tusiangalie hapa juu juu tu. Labda kama tutatoa viongozi wa kisiasa, tunahitajia watalaam. Taifa ili liendelee linahitaji wataalam na tutawapata wataalam kupitia elimu ya juu katika taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naunga mkono Muswada huu ambao unakusudia kutunga Sheria itakayoweka utaratibu wa kuanzishwa kwa Tume ya Vyuo Vikuu itakayoratibu na kuainisha aina ya viwango na uendeshaji wa vyuo vya elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Spika, narudia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na ninaomba utaratibu huu ufanyike kwa nchi nzima. Tuondoe tofauti na kama kutakuw ana migogoro midogo midogo muweze muimalize ili tulete faida na mafanikio makubwa kwa taifa letu, baina ya Tanzania Bara na Zanzibar, baina ya watanzania wote kwa jumla.

Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba suala hili kwa niaba ya taifa alisimamie kwa nguvu zake zote na isiwe kuratibu ili tuweze kufanikisha yale malengo yaliyokusudiwa. Ni kuviimarisha vyuo hivi vitakavyoanzishwa, na kuviletea faida kubwa sana ya kupata elimu kwa watu wetu.

Ibara ya (21) hadi Ibara ya (33) inapendekeza masharti ya uanzishwaji wa vyuo vya elimu ya juu. Haya masharti ambayo sijayamalizia kwenye vitabu hivi, ni vizuri baadaye yakawekwa wazi Watanzania wote wakaweza kuyajua. Nafanya hivyo ili wale ambao watakuwa na wasi wasi wa kutaka kuanzisha vyuo vyao au kwamba wanataka kuona kwamba kuna kitu fulani ambacho kinaulazima anataka kukifuatilia

ili wajue. Hii ni kama hakuna kipingamizi ambacho kinaweza kuwabana wasiweze kuanzisha hivi vyuo vikuu.

Kwa hiyo, masharti haya ambayo yatakuwa yameainishwa kwenye Sheria hii tunaiomba Serikali iweke wazi kwa Watanzania wote ili waweze kuyaelewa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita ya Muswada huu yenye Ibara ya (48) hadi (51) inafafanua masuala ya jumuiya ya wafanyakazi na wanafunzi, utawala na ustawi wa wanafunzi naipongeza sana Serikali. Lakini sasa jumuiya hizi inaonyesha hapa ziko tatu zilivyojiweka ni vizuri tukaangalia zitafanya kazi vipi kwa umoja kwa sababu kuna jumuiya ya wafanyakazi na wanafunzi, utawala na ustawi wa wanafunzi.

Haya tunataka tuone Mheshimiwa Waziri haya yatafanya fanya vipi kazi hizi za jumuiya. Naomba utakapojibu unitoe wasi wasi kwamba hii jumuiya ya wafanyakazi na wanafunzi itakuwa vipi itajiunda vipi lakini sasa utawala na ustawi wa wanafunzi ule utawala utakuwa katika kiwango gani na malengo yake makubwa yatakuwa ni nini. Pamoja na kwamba *point* inanilenga kwa faida ya wanafunzi.

Kwa hiyo, hapa naomba kidogo unipe utakapo kuja kusahihisha au kutoa majumuhisho utueleze hapa tunaainisha nini kwamba hii jumuiya imefafanua masuala yanayohusu jumuiya ya wafanyakazi na jumuiya ya wanafunzi. Hii ni pamoja na au wakiwemo walimu na wanafunzi au wafanyakazi wote au pamoja na wizara kwa jumla. Hili naomba huo ufafanuzi utolewe.

Mheshimiwa Spika, chini ya mapendekezo haya inasema shughuli za vyama vya kisiasa katika maeneo ya vyuo vikuu vimepigwa marufuku Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lazima tuangalie mustakabali wa Taifa letu. Si vizuri kuwaingiza wanafunzi kwenye mambo ya kisiasasiasa tu, nchi haiwezi kuendelea kwa masuala ya kisiasa, lakini wataalam ndio watakaopeleka maendeleo ya nchi hii. Ni vizuri kunapokuwa na matatizo katika Vyuo vyetu, tukaangalia namna gani ya kuweza kuwasaidia wanafunzi wetu walioko katika hivyo Vyuo; kulikoni kujiingiza kisiasa tukaanza kuwagawa na kuwapotezea yale malengo ambayo tumeyakusudia? Tusifanye mchezo na suala zima la elimu. Hapa kuna baadhi ya Watanzania wanaanza kulalamika, kama wenzetu wa Kenya na Uganda, wako mbali sana kielimu!

Kwa hivyo kutokana na mfumo huu tunaotaka kuunzisha, ni lazima Watanzania tuwe wakweli tukianza sisi wanasiasa kwanza, siyo wanafunzi. Wanafunzi wanaweza kuwa na matatizo yao kule wakakawaalika, lakini ni vizuri tukaenda pale tukashughulikia lile tatizo la wanafunzi, si kwenda pale tukaingiza ya kwetu ya kisiasa, hatutafika pale ambapo tumekusudia na tutaweza kurudisha Taifa hili nyuma.

Kwa hivyo, sababu moja kubwa ni suala la elimu. Hata sasa hivi Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu alipokuwa akijibu suala la Mheshimiwa Kawawa alizungumza kwamba tutoe elimu zaidi kwa watu wetu. Kwa hiyo, cha msingi hapa tunachoasa ni elimu. Kwa hivyo mimi namuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia kwa kuweka kifungu hiki ambacho kwa kweli kinakataza kuingiza siasa katika Vyuo vyetu Vikuu. Tuangalie kiu yetu ni nini sasa hivi, Taifa letu la Tanzania linahitaji maendeleo, basi hakuna lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tukipata wasomi ndio tutakwenda kule mbele tulikokusudia, kupambana na rushwa, kupambana na umaskini uliokithiri katika nchi yetu, tutazidisha umoja wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hili ni suala la kuliangalia sana sisi Viongozi, tusiwatumie vijana wetu walioko Vyuoni kwa maslahi yetu binafsi. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba nisimame nikuunge mkono asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, lingine kwenye hili ningeomba masuala haya ya uanzishaji wa Vyuo, usilete mgongano wa maeneo yetu mawili ya Muungano. Sasa hivi hapa Msemaji wa Upinzani amesema kwamba inaonyesha Zanzibar kuanzisha Chuo Kikuu imevunja Katiba ya nchi. Lakini mimi naamini kwamba suala la kuanzisha Chuo Kikuu cha Zanzibar Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina taarifa zote. Nafikiri na Mheshimiwa Waziri atakuwa anajua. Kwa hiyo kama kuna mapungufu ni vizuri Serikali kuzirekebisha au kuziweka wazi kuliko kuja tukaulizana hapa Bungeni tena kwamba kuna Katiba iliyovunjwa, Serikali ijiuzuru haya yatakuwa hayana maana hata moja. Inawezekana kama kuna mambo yalikosekana huku mwanzo, kuyatolea ufafanuzi na leo mpaka sasa hivi tunajadili Mswada huu wananchi hawajui Chuo kile cha Zanzibar kilianza vipi.

Mheshimiwa Spika, kasoro kama zile sio vizuri kuziacha tukazifungia na baadaye zikaja zikatushtukizia tu kulazimisha Waziri atoe ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, nasema nimesimama hapa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri na kwa kweli tunamtegemea. Kwa niaba ya Serikali tunamtegemea yeye ndio kioo chetu na kwa kweli mimi nimemwamini sana. Ni mara nyingi nimefika hapa kuchangia Miswada yake na nimeona mafanikio makubwa sana, hata kile Chuo Kikuu Huria Pemba tayari kipo na vijana sasa hivi wanafanya kazi. Tunavyotaka sasa hivi ni elimu kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha maendeleo ya elimu, nimeiomba Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuharakisha mipango yake ya kutaka kuimarisha miundombinu katika Mkoa wa Rukwa hasa masuala ya barabara. Kwa sababu juzi Kamati yako ya Ulinzi na Usalama ilipokuwa kule tuliona kuna kasoro na suala la elimu inawezekana Rukwa wakawa nyuma sana kimaendeleo huko tunakokwenda. Hata sasa hivi wana upungufu wa Walimu katika Mkoa wa Rukwa. Kwa hiyo Serikali ifungue miundombinu haraka sana ya barabara na umeme kwa yale maeneo ili tuende sambamba. Tuhakikishe Mikoa yetu haipitani sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache nataka nirudie kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri. Nakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu muhimu. Lakini kabla ya kufanya hivyo kwa niaba yangu na kwa niaba ya Jimbo la Nkenge, niwape pole familia ya Mheshimiwa Balozi Diria na Balozi Bomani na tuwaombee kwa Mwenyezi Mungu ili wakae mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Muswada huu nina wasiwasi kwamba huenda nia yetu nzuri tuliyonayo isiwe hivyo mara tu Muswada huu ukishakuwa Sheria rasmi. Kwa sababu nia nzuri ni jambo moja na itakavyokuwa ni jambo jingine, sasa nitaomba Mheshimiwa Waziri baadaye anishawishi nimuunge mkono hoja kwa kunihakikishia kwamba nia nzuri tuliyonayo ndivyo hivyo itakavyokuwa itakavyokuja kwenye utekelezaji wa Sheria yenyewe.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu Sheria hii inafuta Sheria zilizoanzisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, inafuta Sheria inayoanzisha Chuo Kikuu cha Mzumbe, inafuta Sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu cha Sokoine na inafuta Sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Spika, lakini tunapokuwa hapa na tukasema chombo hiki kinaanzishwa kwa Sheria ya Bunge ni tofauti kabisa na chombo kinachoanzishwa na *charter* au na *regulation* au na Sheria nyingine inayotokana na Sheria kubwa ya Bunge. Chombo kikianzishwa na Sheria ya Bunge maana yake ni kwamba chombo hicho kinakuwa kinawajibika moja wa moja kwa Bunge hili. Lakini ukiwa unaanzisha chombo kizito kwa *charter* au kwa utaratibu mwingine unaotokana na Sheria ya Bunge, maana yake ni kwamba chombo hicho hakiwajibiki moja kwa moja kwa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, sasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni Chuo mama kwa elimu ya nchi hii na kilianzishwa na Sheria kubwa, Sheria ya Bunge. Kwa hiyo leo hii tunapofuta, lazima tuwe na uhakika Sheria mpya tunayoiweka haitavuruga mafanikio ambayo yametokana na Chuo hicho kuanzishwa na Sheria ya Bunge? Huo ndio wasiwasi wangu. Kwamba, leo hii tunapokuja na Sheria mpya, basi Sheria hiyo haitaondoa mafanikio yale yaliyotokana na kuanzishwa kwa vyombo hivyo na Sheria ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, lakini ndio maana ukiangalia Sheria hii kwa stahili nzuri kabisa, Sheria iliyoanzisha *State University of Zanzibar* haijafutwa. Haijafutwa si kwa bahati mbaya ni kwa sababu ya wasiwasi wangu nilionao. Kwa sababu nina uhakika kama Mheshimiwa Waziri angejaribu kufuta Sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu cha Zanzibar, basi Muswada wake usingekatiza hapa. Kwa stahili, nzuri akaamua aiache

hivyo hivyo pamoja na ukweli kwamba Sheria hii inasema kwamba itafanya kazi Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, ukisoma kifungu cha pili kwenye *applications,* pamoja na kifungu cha 19 inaeleza kwamba Sheria hii itafanya kazi Zanzibar pamoja na Tanzania Bara. Kwa sababu hiyo tungefikiri *University* zote zilizo Zanzibar na zilizo Bara zote zianzishwe kwa Sheria hii mpya tukishaiweka. Lakini hatuoni Sheria iliyoanzisha *State University of Zanzibar* ikifutwa. Mimi nakubaliana naye kutoifuta Sheria ile na kwa sababu hiyo hiyo iliyosababisha Sheria iliyoanzisha *State University of Zanzibar* isifutwe, basi na Sheria zinazoanzisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mzumbe, Sokoine na Chuo Kikuu Huria zisifutwe zibaki kama zilivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nasema yako mambo mawili. Moja, kuna ubora wa Elimu ya Vyuo Vikuu, hilo ni jambo moja. Lakini la pili kuna uanzishaji wa Chuo Kikuu, hilo ni jambo lingine. Sasa Sheria hii inajaribu kufanya kazi zote mbili kwa wakati mmoja. Inajaribu kuhakikisha kwamba inaangalia ubora katika Vyuo vya Elimu ya Juu na na wakati huo huo inaweka utaratibu mpya wa kuanzisha Vyuo Vikuu. Lakini kwa utafiti niliofanya kote Duniani, *Public Universities h*ata kama sio zote, lazima ziwepo zinazoanzishwa kwa Sheria za Mabunge ya nchi husika kote Duniani.

Zipo nyingine wanaita *Polytechnic*; ukienda Uingereza watakuwa wanasema *University* lakini ni *Polytechnic University,* utakuta watakuambia *University* lakini *Traditional University.* Kwa nini wanafanya hivyo? Ziko *Universities* kwa mfano Uingereza huwezi ukafanya kazi Wizara ya Mambo ya Nchi za nje kama hujapitia kwenye hiyo *University,* kwa sababu wanaamini kwenye Chuo hicho ndiko maadili ya Mwingereza yanakofundishwa tu. Kwa hiyo lazima Chuo hicho kilindwe.

Kwa hiyo haiwezekani leo hii Tanzania tukawa na mawazo ya kwamba Vyuo vyote vitakuwa sawa, si kweli hata kidogo. Kwa hiyo wakati tunafurahia kupitisha Muswada huo, lazima nieleze wasiwasi wangu. Ukienda Marekani viko Vyuo vinajulikana kwamba huwezi ukawa Rais wa Marekani kama hujafikia kwenye Chuo fulani. Pia huwezi ukaingia kwenye ile *Foreign Affairs* ya Marekani kama hujapata maadili ambayo wanajua maadili hayo unaweza ukayapata Chuo fulani kilichoanzishwa kwa utaratibu maalum na ambacho Serikali inakiangalia kwa jicho la karibu.

Lakini kwa leo hii tunajaribu kuviweka Vyuo vyote kwamba viko sawasawa na nini, tuendelee lakini huko mbele ya safari tutakuja kushangaa tutakapokuta nchi hii haina Vyuo ambavyo inaweza ikajivunia kwamba Vyuo hivi vinafanya shughuli hii na kwa sababu hii. Kwa hiyo Serikali inaweza ikahakikisha inavisaidia Vyuo hivyo lakini hata Bunge lenyewe linaweza likaingilia kati pale inapohisi kwamba labda kwa njia moja au nyingine uhuru wa *Academic freedom* unaingiliwa au mambo mengine ambayo hayastahili kuingiliwa yanaingiliwa. Sasa hilo ni wasiwasi wangu. Nia ni nzuri lakini lazima tuwe makini na hilo kwa sababu vinginevyo tutajikuta kwenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, sasa Sheria yetu pamoja na kwamba inasema itafanya kazi Zanzibar na Tanzania Bara, lakini ukisoma kwenye Sheria yenyewe, utaona kwamba tuna *Private University na Public University.* Lakini hakuna ambapo imeelezwa waziwazi

kwamba Sheria hii itazibana Vyuo vyote vya *Public* na *Private.* Kwa hiyo ingekuwa vizuri hilo likawepo kwa sababu vinginevyo kama hilo hujalitaja kwamba Sheria hii itazibana *Universities* zote za *Public* na *Private Universities*, siku moja Waziri anaweza akaagiza *Private University* na ikamjibu kwamba Sheria unayotumia hakuna popote ambako imetajwa kwamba wewe utalazimika kufuata Sheria hii. Sasa hiyo inaweza ikawa *technical knock-out* kwa nia nzuri inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ni kwamba tunaweka *Search Committee* za kuwapata *Vice Chancellors.* Lakini hatujaweka sifa za Wajumbe watakaokuwa kwenye hizo *Search Committees* na hatujaeleza waziwazi ikaeleweka kama kila Chuo kitakuwa na *Search Committee* au *Search Committee* itakuwa moja. Lakini vile vile ukienda kwenye *second schedule,* ukurasa wa 57 nataka hilo tuliweke vizuri ili baadaye lisije likasumbua. Inasema: *"The Vice-Chancellor* or *equivalent designation of each public and each fully accredited and Chartered Private University*."

Maana ya sentensi hii ni kwamba *Public University* si lazima iwe *fully accredited,* ukiisoma hapa. Lakini hoja hapa ni kwamba uwe *Public* ama *Private* lazima uwe *fully accredited.* Kwa hiyo ni vizuri ikasomeka kwamba: *"Of each fully accredited and Chartered Public and Private University",* ili wengine wasifikiri kwamba si lazima na wao wawe *accredited.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nimwombe sasa Mheshimiwa Waziri atusaidie kwamba *University* yetu ya Bukoba ambayo huko nyuma ilianzishwa kwa nia nzuri na hapa katikati ikakwama, basi tushirikiane kuhakikisha *University* hiyo inarejea na inafanya kazi yake kama ambavyo tulikusudia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nikiondolewa wasiwasi nilionao nitaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nichangie katika Muswada wa Vyuo Vikuu wa mwaka 2005.

Lakini kabla sijafanya hivyo, ningeomba nijiunge na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuchangia mada mbalimbali za Kikao hiki kwa kutuma rambirambi zangu kwa niaba ya wananchi wa Kisarawe kwa ndugu, jamaa na wananchi wa Jimbo la Raha Leo kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Hassan Diria. Pia, natoa rambirambi zangu kwa Ndugu na Jamaa wa Marehemu Balozi Bomani, Mwanasiasa Mkongwe katika nchi hii. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumpongeza mtani wangu Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Makamu wake Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu Mama Ruth Mollel na Wasaidizi wao kwa kuandaa Muswada huu kwa wakati, Muswada ambao umewasilishwa kwa ufasaha. Muswada huu utaimarisha sana usimamizi na maendeleo ya Vyuo Vikuu katika Taifa letu. Bila ya kuchelewa naomba nitamke kwamba ninauunga mkono Muswada huu mia kwa mia. *(Makofi)*

Hata hivyo, ninayo maoni machache ambayo shabaha yake si kukosoa bali kuuimarisha Muswada kama maoni yangu yatazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Sehemu ya Pili ya Muswada, Ibara ya Tano, zimeorodheshwa shughuli au kazi mbalimbali za Tume, kama sikukosea ziko karibu 17. Maoni yangu kwanza, ni mzigo mkubwa sana kwa Tume hii kuwapa majukumu hayo yote. Pili, nadhani baadhi yao yangeachiwa Vyuo Vikuu vyenyewe vikashughulikia. Kwa mfano, majukumu yaliyopo katika Ibara ndogo ya kwanza ya Ibara hiyo ya tano, kifungu (f), (i) na (k), si muhimu sana, kwa maoni yangu, kuiachia Tume ifanye haya mambo ambayo ingeweza kufanywa na Vyuo vyenyewe. Nimeona marekebisho yaliyofanywa katika kifungu (f) lakini bado marekebisho hayo hayatabadili mawazo yangu juu ya shughuli kama hii kuachiwa Vyuo.

Katika Ibara ya (4) (2) (c) limetajwa jukumu la Tume kukopa fedha na kuingia Mikataba mbalimbali. Lakini kwenye Ibara ya 16 ambayo inazungumzia vyanzo vya fedha, suala la mikopo halipo ingawa tena Muswada huu unaelezea katika Ibara ya 45 kwamba jukumu hilo lipo. Ningeshauri, basi katika Ibara ya 16 kiongezwe kifungu cha 16(a)(i) ambacho kitataja kwamba mikopo itakuwa ni baadhi ya vyanzo vya fedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli za Vyuo.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ibara ya 17(2)(b) kumetajwa matumizi ya fedha kama malipo kwa Wajumbe wa Tume. Lakini naona hapa imesemekana kwamba ni *reimbursement* kwa Wajumbe. Maana ya *reimbursement* ni kwamba watarudishiwa gharama zao zile walizotumia. Swali; Je, Wajumbe hawa hawatapata posho? Au watakuwa wao wanagharamia kisha wanarudishiwa? Ninafikiri kuna haja ya kulirekebisha hili kwa kuweka posho badala ya kuweka marejesho ya matumizi kwa Wajumbe.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 39(9) inaweka muda wa ajira wa Makamu wa Chuo Kidogo *(University College)* kuwa miaka mitatu. Mimi naamini kwa kazi nzito kama hii ya kumsaidia Makamu wa Mkuu wa Chuo, inahitajika utumishi wa muda mrefu. Lakini ukimweka mtu kwa miaka mitatu, kisha unamwondoa unaleta mwingine, kutakuwa na *instability* katika usimamizi wa Vyuo. Nafikiri tunaweza kuwa na usimamizi endelevu kama kipindi hiki kitaongezwa kufika miaka kama mitano hivi.

Vile vile kwenye Ibara ya 46 Sehemu ya Tano ya Muswada huu, inaelezea Muundo wa Baraza la Taaluma *(Senate Committee).* Wametajwa Wajumbe ambao mimi nakubaliana nao wote ambao wataingia mle. Lakini naona kuna kasoro moja. Siku hizi tunazungumzia sana suala la jinsia na ninajua kwamba tunao Maprofesa wanawake. Sioni sababu kwa nini suala la jinsia halikuzingatiwa hapa. Ningependa kumshauri Waziri kwamba katika hii *Senate Committee* ahakikishe kwamba kutakuwapo na uwakilishi wa akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nihamie kwenye Jedwali la Kwanza. Kwenye jedwali hili, Ibara ya 1(5) ya jedwali au sijui tuite kielelezo *(schedule)* kumetolewa nafasi mbili za Wawakilishi wa Serikali ya Mapinduzi. Kwa utaratibu ule ule, naomba uangaliwe mgawanyo wa kijinsia. Ningemshauri Mheshimiwa Waziri basi, kwenye Sheria hii aseme angalau katika hawa wawili mmoja awe mwanamke, kwa sababu tunaamini kabisa kwamba suala la elimu linawazingatia wote.

Kwenye Jedwali hilo hilo la kwanza kunatolewa madaraka kwa Waziri ya kumteua Mwenyekiti wa Tume. Mimi nadhani hii siyo sawa, kwani ndani ya Muswada huu huu kumeelezwa kwamba mwenye madaraka ya kuteua Makamu wa Vyuo Vikuu ni Rais. Mimi naamini kwamba Tume iko juu ya Chuo Kikuu kimoja kimoja. Sasa haiyumkiniki kwamba Mwenyekiti wa Tume anateuliwa na Waziri, lakini Makamu wa Vyuo wanateuliwa na Rais. Ningeshauri ili kuwa na *consistence,* basi huyu ambaye naamini yuko juu ateuliwe na Rais badala ya kuteuliwa na Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye jedwali la pili, Ibara ya Nne inazungumzia habari ya *constitution* ya ile Kamati ya Makamu Wenyekiti wa Vyuo Vikuu. Sina ugomvi na mapendekezo yanayowekwa ya kuweka Wenyeviti kwa mzunguko wa zamu kutoka Chuo kimoja hadi kingine kwa muda wa vipindi vya miaka miwili miwili. Lakini nina tatizo kuwafanya Makatibu wa hao Wenyeviti kuwa ndio Makatibu wa hiyo Kamati yao, tukizingatia kwamba katika Muswada huu kumeelezwa kuwa angalau kutakuwa na vikao viwili kwa mwaka. Maana yake ni kwamba Katibu wa Kamati hii atakuwa anafanya kazi kwa Vikao vinne tu, kama hakuna Vikao vya dharura.

Mimi nafikiri hili si sawa kwa sababu haitamwezesha Katibu kuzingatia maamuzi ya Vikao vilivyopita wala kuishauri Kamati kuendelea na mambo mengine kwa vile anabadilishwa na Katibu mpya baada ya miaka miwili, baada ya kuhudumia Vikao vinne. Nafikiri Mheshimiwa Waziri atakubali ushauri wa kuwa na Katibu wa kudumu hata kama hatakuwa wa kuajiriwa, lakini aweze kuchaguliwa kutoka katika Chuo kimoja na akadumu kwa miaka angalau minne mitano kwa ajili ya kutaka kupata *continuity*. Lakini kuwabadilisha badilisha kwa haraka namna hiyo nafikiri ni kwamba hautakuwa utaratibu mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikuwa na mengi. Nilitaka kujazia hayo tu, mengi mengine yamesemwa na wenzangu walionitangulia. Lakini napenda kurudia kusema kwamba naukubali Muswada na ninauunga mkono mia kwa mia. Ninawashukuru sana kwa kazi nzuri waliyoifanya. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu ulioletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuchangia Muswada huu naomba kutoa salamu zangu za rambirambi kwa familia za Marehemu ambao wametutoka katika kipindi hiki. Natoa salamu za rambirambi kwa familia za Marehemu Balozi Diria pamoja na familia za Marehemu Paul Bomani. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka, kwa sababu ni wakati huu tunahitaji Vyuo Vikuu vingi na hivi Vyuo Vikuu vingi vinavyotolewa viweze kudhibitiwa. Tunao wanafunzi wengi kwa wakati huu ambao wanamaliza Shule za Msingi kutokana na mpango wa Serikali wa *MMEM*. Vile vile, tunao wanafunzi wengi ambao wanazidi kuongezeka kutokana na mpango wa Serikali wa Shule za Sekondari *MESS. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili linafanya tuwe na wanafunzi wengi ambao wanamaliza Shule za Sekondari ambao wanahitaji kujiunga na Vyuo Vikuu ambavyo tunavyo hapa nchini. Lakini ongezeko hili limewafanya wanafunzi wengi wanaomaliza Shule za Msingi kutoweza kupata nafasi katika Vyuo Vikuu ambavyo tunavyo sasa. Vile vile, ongezeko hili la wanafunzi limesababisha mlundikano mkubwa katika Vyuo Vikuu ambavyo tunavyo na ongezeko hili limefanya Vyuo Vikuu vipya viweze kuanzishwa. Hivyo basi, tunahitaji tuwe na udhibiti mkubwa katika Vyuo Vikuu ambavyo vinaanzishwa na Vyuo ambavyo tunavyo.

Mheshimiwa Spika, mlundikano wa Wanachuo katika Vyuo vyetu Vikuu hasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam umekuwa ni mkubwa sana kiasi kwamba inakuwa ni vigumu kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa katika Vyuo vyetu. Kwanza majengo hayatoshi katika *lecture rooms,* Wanachuo wanakaa chini, wengine hawana ma-*desk*, wengine wanasikiliza kutoka madirishani. Hali ni mbaya sana katika Vyuo vyetu Vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wakati umefika ambapo Tume hii itakayoundwa sasa iweze kuangalia matatizo ambayo tunayo katika Vyuo vyetu Vikuu kusudi yaweze kutatuliwa kwa haraka. Nina wasiwasi kwamba mlundikano huu unaweza ukasababisha hata mlipuko wa magonjwa kama vile uti wa mgongo. Ni hatari kwamba katika Vyuo Vikuu katika *Hostel* zetu, Wanavyuo wamefikia kiasi cha kulala wawili wawili katika vitanda, eti wanabebana.

Mheshimiwa Spika, hali ni mbaya sana. Kwa hiyo Tume hii itakayoundwa itafanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba Wanachuo wanaojiunga na Chuo Kikuu wanapata elimu bora na sio bora elimu. Sitegemei kwamba wanapokaa chini wakiwa wengi kiasi hicho wanaweza kuelewa yale yanayofundishwa kwa sababu kutakuwa na vishawishi vingi humo humo. Vile vile, wanakuwa hawawezi kusikiliza kwa makini. Lakini vile vile hata Mwalimu hawezi kusahihisha wanafunzi 300 au 400 na akaweza kuwasahihisha kwa makini na hivyo kudhibitisha kwamba tunakuwa na Wanachuo ambao wamepata elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kinachohitajika ni kwamba Tume hii itakayoundwa iweze kuhakikisha kwamba Vyuo vinavyofunguliwa pamoja na Vyuo vilivyopo wanakuwa na majengo ya kuweza kutosheleza idadi ya Wanachuo ambao wanakuwa wamejiunga na Chuo. Hii itaweza kudhibiti usikivu pamoja na kuondoa milipuko ya magonjwa kama nilivyokuwa nimeshauri. Iweze kudhibiti idadi ya wanafunzi. Kama Chuo kinaanzishwa kijue kwamba kitapokea wanafunzi kadhaa, basi idadi hiyo ifuatwe

kila wakati wanapowasajili wanafunzi. Kama wanataka kuongeza wanafunzi, basi kuwepo na ongezeko la majengo kwa ajili ya wanafunzi hao pamoja na ongezeko la Walimu ambao watatosheleza kuwapa elimu iliyo bora wanafunzi wetu na Vyuo viwe na hadhi.

Mheshimiwa Spika, itakuwa tunaileteа aibu Serikali yetu ikiwa mtu yeyote anatoka nje na kuingia katika Chuo kuona jinsi walivyolundikana katika *lecture rooms.* Naomba Tume izingatie idadi ya wanafunzi watakaokuwa wamesajiliwa katika Chuo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 29 kinampa uwezo Rais kukifungia Chuo ambacho kitakuwa kimekiuka masharti ambayo yamewekwa. Nashauri mwaka mmoja ambao Chuo kitakuwa kimepewa kabla ya kufungiwa na katika mwaka huo kama Chuo kitakuwa kimejirekebisha, basi kiruhusiwe kuendelea kwa sababu wanachuo watakuwa ni wengi na haitakuwa rahisi kuweza kuwasajili katika Vyuo vingine. Pia ninashauri kwamba ikiwa kuna uwezekano wa kuwasajili katika Vyuo vingine, basi iwe ni jukumu la Serikali yenyewe kutafuta nafasi kwa ajili ya hao wanachuo ambao watakuwa wafungiwa Chuo chao.

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni vigumu kwa kila mwanafunzi kujitafutia nafasi katika Vyuo vingine na ikizingatiwa kwamba inawezekana masharti ya kujiunga na Chuo kingine yatakuwa ni tofauti na masharti ya Chuo kile kilichofungwa. Basi Serikali ihakikishe kwamba inawasaidia hawa wanachuo ili waweze kumudu masharti ya Chuo kipya, hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba wanachuo wa Vyuo hivi wanapewa mikopo ambayo itawawezesha kuendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa sina mengi ya kuongelea. Muswada ni mzuri na ninaunga mkono hoja hii iliyotolewa na kuletwa hapa mbele ya Bunge letu.

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Nami vilevile kabla ya kusema lolote, kwa niaba ya Wapigakura wangu wa Kigoma Mjini nitoe rambirambi zangu kwa Mzee wangu Mheshimiwa Diria na vilevile Mzee Bomani kwa vifo vyao vya hivi karibuni. Naomba Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru kupata nafasi hii kuchangia Muswada ulioko mbele yatu unaohusu *Commission* au Tume ya *Universities* na vile vile uanzishwaji wa *Universities* nyingi katika nchi yetu. Nadhani ni jambo la busara sana kwa kweli, mimi lazima niunge mkono hoja hii pamoja matatizo madogo madogo, lakini nadhani kitendo tu cha kufanya kitu hiki ni dhahiri kabisa kwamba tumeanza sasa kuelewa umuhimu wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nikisoma tu juzijuzi hapa nikakuta takwimu zinazoonyesha Afrika nzima watu wanaopata nafasi ya kuingia Vyuo Vikuu, hasa *Universities* ni asilimia 0.3 ya wale ambao wangependa kuingia; Ulaya ni asilimia 45; Marekani ni asilimia 87. Kwa hiyo sasa hata mtu angekuwa na wivu wa namna gani,

kuwachukia Waamerika wale, wako *very true* katika kila watu 100, basi 87 wamepata Elimu ya Chuo Kikuu. Lazima wawe wajanja sasa, hakuna namna! Wamesoma! Sasa sisi tuko kwenye asilimia 0.3. Kwa hiyo hii nafasi mimi inanifurahisha sana na ninasema tufanye kazi hiyo. Nakumbuka kuna wakati niliwahi kumkabili Mheshimiwa Ng'wandu pale Diamond Jubilee, nikamwambia bwana we, mbona mnaanzisha Vyuo Vikuu vingi? Msifanye kama India kila mwenye jengo moja na yeye anataka Chuo Kikuu itakuwa aibu!

Mheshimiwa Spika, kuna nchi ambako Chuo Kikuu kimefungwa, sasa ni kichekesho. Kweli inawezekana Chuo Kikuu kikafungwa? Mimi naona ajabu kubwa sana, kule kwa wenzetu unaambiwa bwana hiki Chuo bwana tangu mwaka 1400 au 1500, 1800 vipya kabisa! Labda mwaka 1920 sisi huku Chuo Kikuu kimefungwa na mtu anabakia na *degree* ya Chuo kile. Mimi nasema tuwe waangalifu sana. Hii *Commission* tunayounda hapa kwa kweli iangalie maana yake isije ikazuka tu ikawa Vyuo Vikuu vya kitapeli, Chuo Kikuu hakina vitabu. Hakuna vitabu kwenye Chuo Kikuu!! Walimu asilimia 70 hawana *Ph.D.,* sasa hicho ni Chuo Kikuu!!

Mheshimiwa Spika, tuwe waangalifu maana yake Elimu ya Chuo Kikuu inatakiwa ijitegemee. *Product* ya Chuo kile ipimwe na Chuo kingine. Mimi nakumbuka hadithi yangu, siku nilipokwenda kufanya mtihani wa *Masters* na mmoja wa Walimu wangu aliyekuwa ananifundisha mambo ya *Archives* naye alikuwa ameshapata alikuwa ameandika *dissertation* na kila kitu. Lakini tumefika siku ile kwenda ku-*defend Masters* tukaletewa *note* kutoka kwa *President* akasema, hapana hii haiwezi kutendeka leo kwa sababu kuna mmoja pale hana *Ph.D.* Basi tukangoja miezi mingine sita. Sasa mimi naomba hili suala kwa kweli tuliangalie kwa ukaribu sana maana tusije kuanzisha Vyuo Vikuu ambavyo baadaye vikaanza kutuvunjia tena heshima tukipimwa na wenzetu.

Mheshimiwa Spika, mtu anapotokea amemaliza Chuo Kikuu akaenda Uganda, Zambia, Uingereza, Marekani, tunataka awe ni *product,* ni mtu aliyesoma Chuo Kikuu huku Tanzania. Kwa hiyo mimi naomba hilo tulizingatie na tuwe waangalifu sana. Kuna *hang-ups* nyingi tu ambazo mimi nimeziona hazinifurahishi. Mimi sijui kwa nini Rais anakokotwa kwenye suala hili. Kila mahali Rais atateua na kutakuwa na *Vice Chancellor.* Maana ya cheo cha *Vice- Chancellor* ni nini sasa? Maana yake mimi sielewi Makamu wa Mkuu wa Chuo kwa sababu tumezoea utaratibu kama alivyosema Ndugu yangu Mutungirehi hapa, zamani ilikuwa Rais lazima adhibiti kwanza vyeo vyewewe vilikuwa vingapi na vyote vya Serikali. Kwa hiyo akawepo mtu ambaye anafanya ile kazi *fulltime* kwa niaba ya Rais ambaye hawezi kuwepo.

Sasa leo na sisi tunatunga sheria za *Vice-Chancellor* na atachaguliwa kwa hivi na itakuwa hivi, ili aje kufanya nini na yuko pale *Chancellor* jina la Kingereza! Mimi ningependa aitwe *President* wa *University*. Mimi ningesema kwamba katika hii, aidha *Chancellor* au *President* wa *University* ili watu wawe na uhuru wa kuchagua hata hicho cheo. Tutakuwa na Ma-*Chancellor* wangapi nchini, Ma-*Vice-Chancellor* na Kamati ya Ma-*Deputy Vice-Chancellor?* Mimi nadhani zile *Academic units* kama *School of Social Sciences* au *Engineering* zinakuwa na wale ma- *deans. Dean* ndiye anamsaidia *President* kwenye kazi zake za *day to day administration* kwenye shughuli zake zile. Huyu *Vice-*

*Chancellor* ambaye tumemwona tu katoka tangu *University* ya Dar es Salaam sasa anaingizwa na huku tutamweka sasa katika kila *University,* hata Shule yangu ninayotaka kuanzisha mimi naambiwa niwe na *Vice-Chancellor* na atateuliwa na fulani.

Mheshimiwa Spika, Mimi nasema tuwe waangalifu, tuyabebe haya mambo vizuri na tuelewe kwa nini tunaanzisha elimu ya juu. Kwa kweli lengo kubwa ni kuwasaidia Watanzania wapate elimu na waweze kuwa wazalishaji. Tuwe na elimu ambayo mtu akitoka pale siyo tena vichekesho tunavyoviona kwamba wanafunzi wamekosa kazi. Sasa wewe umemaliza *University* na umekosa kazi, inawezekana? Mtu alimaliza *degree* kweli kweli akakosa kazi! Hapana. Ila atatengeneza kazi kwa sababu amesoma. Ndiyo tunataka elimu ya hivyo tutengeneze kazi. Mtoto anatoka pale amemaliza anajua *accounting* zake, anajua anafika anafungua Ofisi yake, anakwenda Benki anachukua mkopo anafanya kazi, anazalisha na wale walioko kazini wanamuonea wivu kwa sababu ameendelea. Sasa tusitengeneze *University* legelege watu wanakwenda wanaingia na wanapata kazi hapana. Elimu ya *University* siyo ya kwenda kutafutia kazi ya Serikali. *(Makofi)*

Hata kama mimi nina Kampuni ya magari, nakuchukua wewe uwe *Transport Manager* kwenye Kampuni yangu ni kwa sababu nimekuchunguza, najua utaniletea faida na siyo kupeana. Mtu aliyesoma hapewi, ila aliyesoma anajitengenezea mkakati na anaishi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hayo mimi ningependa kabisa tuelewe na ndiyo maana tunajaribu kutoa *opportunities.* Sasa tukiwa na watu 90 waliopata elimu ya juu, uongo, tutakuwa kama Japan. Japan hawana miti, vyuma, mafuta, hawana chochote! Lakini wana elimu ya juu. Ukimpelekea mti yeye anaugeuza kinakuwa ni chombo cha kukalia. Ukimpelekea chuma anakigeuza kinakuwa kitu fulani. Wale wanajenga mpaka nyumba ya karatasi, gari la karatasi kwa kutumia elimu. Kuna gari la karatasi linatembea na *speed* zote kwa sababu wameweza sasa kutumia elimu kubadilisha kile kidogo walichonacho ndiyo maana elimu tunayoitafuta sisi hatutafuti elimu ya kuja kupeana vyeo.*(Makofi)*

Mimi ningeomba sana kwamba tunapotengeneza sheria hii, kwa kweli tuangalie lengo letu kubwa ni nini na mimi naiunga mkono kabisa kwa sababu najua sasa ndiyo mwanzo wa ufumbuzi wa matatizo yetu. Haya maneno ya kuondoa umaskini yote yako humu. Aliyesoma hawezi kuwa maskini bwana!

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo labda niongelee tu lile dogo ambalo nimeliona mwisho. Wamesema sasa mambo ya siasa hayawezi kuingizwa huku katika *Universities*. Mimi sijui kwa nini siasa inaogopwa. Mbona mambo ya uchumi yako kule? Mambo ya michezo pia yapo *University*. Ni jambo gani halipo *University*? Maana ya *University* ni nini? Ni *universal!* Acha kitu kije pale, wanasiasa machachari wafike pale wajaribu kuwa-*convince,* sasa tunawasomesha halafu hatuwaamini! Tuwasomeshe na tuwaamini. Kama wanaona huyu mtu ni *bogus* watakataa siasa yake, lakini kama wanaona anawaletea hoja, si ndiyo wakina Karlmaks wote walikotoka huko *University*?

Si ndiyo wote hao walioandika *Dascapital!* Bila kusoma yule Karlmaks angetuandikia hivyo?

Sasa ukisema hakuna siasa tena, au siasa sisi tunaziona tu ni Chama cha Wanafunzi na Kiongozi wao kagomesha na Rais kamfukuza, ndiyo siasa! Yale ni mambo ya vijana tu wanafanya, lakini kwa kweli hatuwezi tukasema kwenye *University* hatuwezi kuwa na siasa. Itakuwepo, tusitafute mchezo wa kufukuzana. Maana yake mchezo wa kufukuzana ni mkubwa sana, aah! Yule bwana yuko *CHADEMA*, kwa hiyo mwondoeni hapa, hapana. Awe *CHADEMA* na awepo *University* yeye anachotakiwa pale ni kupasi mitihani yake. Lakini akifeli kozi zake atafukuzwa kweli. Si ameshindwa?!

Mheshimiwa Spika, mimi nasema hivyo kwa sababu tusije tukatengeneza *loopholes* za baadaye mtu akaonewa tu kwa sababu ya siasa yake eti yuko *University*. *University* maana yake nini? Kuna watu wengine katika Shule zetu hapa tulizosoma wenzangu mmesoma *University,* hapa ni mahali utadhani ni adhabu kuingia mle.

Mimi nimesikia mtu mmoja anasema, kuna Shule nyingine zinatayarisha Viongozi. Sasa jamani, *University* haiwezi kuwa na kazi hiyo? Ni watu wenyewe, wakitoka pale ndiyo watajua cha kufanya. Rais mkubwa kabisa huyu ni kama Malaika kule Marekani, Abraham Lincolin. Yeye alifundishwa kusoma na kuandika na mke wake tena akiwa ni mtu mzima na akiwa ni Fundi Cherehani. Halafu akaenda tu kwenye *University* akasema, jamani mimi nataka kuwa Mwanasheria. Wakamwambia karibu na mtihani ni huu. Akauchukua akafanya mtihani. Kuangalia marks ni 99% wakasema ingia *University* umeweza.

Hapa kwetu mambo vipengele, sijui *principle* tatu na *point* 12 na *Advanced Level.* Mimi nasema *University* lazima ziwe wazi, zichukue watu kwa sababu lengo letu ni kuwaendeleza watu wetu waingie *University. University* ziwe huru kuchukua watu wenye uwezo, siyo kuletewa majina, vitabu, wala namba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii mchana huu na mimi kuwa mmoja katika wachangiaji wa Muswada huu uliokuwepo mbele yetu.

Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza, naomba nichukue nafasi hii kutoa rambirambi zangu za dhati kwako wewe kwa kufiwa na Mheshimiwa Mbunge wako Mheshimiwa Diria; kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na vilevile Rais wa Zanzibar kwa kufiwa na Mjumbe wao wa Baraza la Wawakilishi na Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na familia ya Marehemu hawa.

Vilevile, natoa rambi rambi kwa wafiwa wa *Chancellor* wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye nilifanya kazi naye kwa karibu kabisa katika muda huu nilipokuwa kwenye Bunge.

Baada ya hayo kabla sijaendelea, nichukue nafasi hii kuunga mkono kwanza Muswada huu wa sheria kwa asilimia mia kwa mia. Muswada kwa kweli umekuja kwa wakati na unastahili kufika kwa wakati huu. Kwa hiyo nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa kuuleta Muswada huu katika muda ambao tumekuwa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya dibaji hiyo kidogo, niliingiwa na wasiwasi kwa Wajumbe, sikuwa na nia kwamba nijibu hoja, lakini itanibidi kidogo na mimi nitoe mchango wangu kufuatana na Mjumbe ambaye alizungumza. Naweza kusema kwamba ni lawama au shutuma ya kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Zanzibar na kuitaka hata Serikali au Wizara ijiuzulu kwamba eti Chuo Kikuu cha Zanzibar kimenzishwa kinyume na taratibu. Mimi sidhani kama hii ndiyo hali halisi ilivyo.

Ningetegemea kwamba Mjumbe huyu aipongeze Zanzibar kwa kuanzisha Chuo Kikuu hasa baada ya miaka 40 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar na kutawaliwa huko nyuma kwa zaidi ya miaka 300. Kwani kulikuwa hakuna chombo kama hiki na leo katika kipindi hiki tumeweza kuanzisha Chuo Kikuu. Wanastahili pongezi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Vile vile, kwa ithibati kamili ni kwamba, aelewe kuwa Chuo hiki hakikuanzishwa kinyume na taratibu kwa sababu nimeshuhudia mimi mwenyewe Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu alikuwepo pale akishuhudia mambo yale. Kwa hiyo sidhani kama anaweza akaona kwamba kitu kimeanzishwa kinyume na taratibu na yeye awepo pale. Kwa hivyo ningeomba Mjumbe afute kauli yake hiyo ya kusema kwamba Rais ajiuzulu au Waziri ajiuzulu kwa kuanzishwa kwa Chuo cha Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo ningependa nitoe machache kuhusiana na Muswada wetu huu. Ilikuwa tegemeo langu kubwa sana na wasiwasi wangu mkubwa wa jinsi gani Zanzibar ingeshirikishwa katika kuundwa kwa Tume hii. Lakini baada ya kupitia na kufanya marekebisho, nitoe shukrani kwa kuona kwamba Waziri pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Watendaji wameyaona yale ambayo yalikuwa yananitia wasiwasi ingawaje mimi nilikuwa ni mmoja kati ya Wajumbe ambao katika Kamati ya Huduma ya Jamii tumepitia Muswada huu ipasavyo na kuona kwamba unafaa. Kwa hiyo nitoe shukrani kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wote wameyazingatia yale ya Zanzibar.

Si hayo tu, lakini tegemeo langu hasa katika siku zinazofuata ni kwamba, tutazidi kuwa pamoja na kuishirikisha Zanzibar katika kuona kwamba inaanzisha Vyuo vingine zaidi katika utaratibu huu ambao hivi sasa ni muafaka na unaelekea na kuleta mwelekeo wa kuwa na watu wasomi katika nchi yetu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kila jambo linalokuja linakuwa lina raha yake na matatizo yake. Tunaelewa wazi kwamba hivi sasa idadi ya wanafunzi ambao wanajiunga na Vyuo Vikuu ni ndogo sana na hii ni kutokana na kwamba hatuna Vyuo vya kutosha. Kwa hiyo

ningeiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwamba tuna utaratibu mzuri tu tuliojiwekea kwa sasa hivi ambao natumaini Wajumbe wote hapa tutaupitisha kwa moyo mmoja kuhakikisha kwamba Vyuo hivi na hasa vile Vyuo ambavyo ni vya Serikali vinapatiwa nyenzo za kutosha na nyenzo hizi si nyingine bali ni kuhakikisha kwamba vinapatiwa pesa za kutosha katika bajeti zao.

Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba wakati mwingine Vyuo vinashindwa kuchukua idadi ya wanafunzi kutokana na kwamba hakuna nafasi za kutosha katika Vyuo kwa hivyo. Ikiwa kama leo tunaji-*commit* kuanzisha Vyuo, zaidi vinaweza vikawa ni vya Serikali au vya binafsi, lakini tuhakikishe kwa vile ambavyo tunavianzisha sisi wenyewe tuvipatie nyenzo na kuzipangia bajeti ya kutosha ambayo natumaini kwamba Wabunge hapa itakapokuja mbele yetu hatutakuwa na mashaka ya kuipitisha ili kuona kwamba Vyuo vyetu hivi vinaendelea vizuri.

Zaidi ya hiyo ningependa kutoa wito tu kwa vijana kwamba wasome kwa sababu haitakuwa jambo la busara kwenda kusema kwamba mtu anakwenda Chuo Kikuu jamani kweli! Tuzingatie, kweli uingie Chuo Kikuu huna hata zile *passing marks* zinazoruhusu uingie Chuo Kikuu! Tuchukue mifano, Dunia inaachana na inakwenda na wakati, hakutakuwa na wasomi wa *Grade* tatu, yaani *Grade* ya I, *Grade* ya II na *Grade* ya III ukasema ukamchukue wa *Grade* ya III kwenda kujiunga na Chuo Kikuu. Ni lazima utachukua wa *Grade* ya I ukiwa na tamaa kwamba atafanya vizuri na kuwa na *product* nzuri ya kumalizia Chuo Kikuu na ukaweza ukampa kazi ambayo wewe mwenyewe utakuwa na matumaini kwamba inaweza ikatendeka vizuri.

Kwa hiyo vijana wasome na ninaamini ikiwa tutasoma na tutawasomesha watoto wetu, watakuwa na nafasi na ndiyo hapo Vyuo zaidi vitaanza kujengwa na vitaendelea kujengwa vikiwa vya *Private* au vikiwa vya Serikali na tutaona kwamba hao vijana ambao wanajiunga watakuwa ni vijana ambao wanaelekea na waliokuwa na mwelekeo wa kujiunga na Vyuo Vikuu vilivyokuwa tayari tumeshaviunga mkono.

Mheshimiwa Spika, mimi kama kawaida sitakuwa na mengi isipokuwa tu kwa mara nyingine niwapongeze tena Wizara kwa juhudi yao hiyo na msimamo wao na kuona kwamba wameanzisha sheria hii mpya ambayo itatumika katika nchi yetu hii pamoja na Zanzibar na kusema kwamba nawatakia kila la kheri na mafanikio na kuiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Ahsante. Si wakati muafaka kuomba mwongozo labda kama unahusu utaratibu. Lakini si wakati muafaka katikati ya mjadala namna hiyo. Mheshimiwa Talala Mbise.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia katika hoja hii. Kabla ya yote naomba kutoa pole na rambirambi kwa familia na ndugu wa Balozi Diria na Balozi Paul Bomani kwa kuondokewa na wapenzi wao. Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Amen.

Pili, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yao nzima inayoongozwa na Katibu Mkuu kwa kuandaa Muswada huu na kwa kazi nzuri ya kuongoza Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, nitajihusisha na kazi ambazo zimeainishwa kuhusu Tume inayopendekezwa. Kwanza, ni kuhusu ule ukurasa wa 11 na Ibara ya tano ambako ndiko zinakoainishwa hizo kazi za hiyo Tume.

Kwanza ni uwezeshaji wa kuhamisha alama za kufaulu kwenye somo fulani kutoka Chuo fulani kwenda kuongeza alama zinazohitajika Chuo kingine hasa kwenye mfumo wa *Semester.* Hii ni ile kwa Kiingereza inaitwa *credit transfer.* Hili naomba niwapongeze sana watu waliotunga huu Muswada na walioona hili suala. Suala la *credit transfer* ni ambalo limekuwa kero kubwa kwa Vyuo Vikuu na kwa wanafunzi kwa sababu kuna wanafunzi ambao wamependa kufanya *transfer* kama hizi lakini haikuwezekana kwa sababu haukuwepo utaratibu wa aina hiyo. Kwa hili kwa kweli nawapongeza sana.

Lakini pia naomba kama kuna uwezekano wa kufanya lingine ambalo linaendana na hilo, nalo ni kwamba kuna Vyuo ambavyo wanatoza ada kulingana na jinsi mtu anavyokuwa pale Chuoni kwao badala ya kufuata mfumo wa *credit hours* ambazo anachukua mtu. Kwa hiyo ningependekeza kwamba utazamwe mfumo wa kutoza ada kufuatana na *credit hours* badala ya mimi tu kuwa nalipa ada eti kwa vile nipo pale Chuoni badala ya kwamba mimi nalipia nini. Kwa hiyo mfumo uwe wa kulipia *credit hours* badala ya kwamba niko pale Chuoni.

Pili, ni mfumo wa kupokea wanafunzi. Zimeainishwa pale Kamati tatu katika Muswada. Moja ya hizo Kamati tatu ni Kamati ya *Admissions,* yaani Kamati ya kupokea wanafunzi wanaoingia Vyuoni. Hiyo iko ukurasa wa nane Ibara ya 12. Mimi pale nimeona, kitu ambacho kidogo najisikia siko *comfortable* nacho sana, ninazungumzia *Central Admission Services,* inanipa *impression* kwamba hii Tume itakuwa inapokea wale wanaopeleka maombi yao, yanapokelewa na Tume, Tume inayachambua yote, halafu ndipo inapeleka Vyuoni. Mimi nadhani hiyo haitakuwa muafaka sana. Si jambo zuri ku-*centralize admissions* kwenye *level* hiyo kwa Vyuo vyote vya Umma. Sidhani kwamba itakuwa muafaka. Tutakuwa tunaua ubunifu kwenye *level* ya Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, kuna Vyuo Vikuu ambavyo vina ubunifu wa hali ya juu mno. Vina ubunifu wa jinsi gani wanaweza kupata wanafunzi na kuhakikisha kwamba *products* zao zinapata wateja bila kutegemea *admissions* za *Commision* au Tume, Tume ambayo kwanza iko mbali na Chuo, hawajui mazingira ya Chuo, sidhani kwa kweli ingekuwa muafaka sana. Mimi nadhani Tume iwe tu kazi yake ni uratibu, lakini siyo kufanya hiyo kazi ya *admission,* hapana. Kama ndiyo maana yao hiyo, mimi nadhani inabidi itazamwe zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ule ukurasa wa 11 ile namba tano pia ambayo inahusu mambo ya *quality assurance* kwamba Tume ita-*promote quality assurance* kwenye *higher education, quality assurance* halafu pili, ita-*promote noble ideals* katika

ukurasa wa 12 (j) kwamba ita-*promote quality assurance* (ii), (iii) *noble ideals of National Identity*, ita- *promote cooperation* na *net-working among Universities.*

Mimi kidogo nina wasiwasi pale na ningetoa pendekezo kwamba, kwanza kabisa ningetazamia kwamba umoja wa nchi yetu mpaka kwenye Chuo Kikuu unakuwa kwa kweli, mpaka hapo tumeupoteza kwa kiasi kikubwa mno. Mahali pazuri pa kuanzia ni chini kidogo kabla ya Chuo Kikuu japo pale ni kwamba labda tunajaribu ku-*repair* mahali ambapo tumeshafanya *damage* kidogo huku tulikotoka. Mahali pazuri ni pale kwenye Sekondari, bahati mbaya sera yetu ya Sekondari kwa kila Kata nina imani hiyo ime-*compromise* kwa kiasi kikubwa umoja wetu. Kwa hiyo, kwa kweli sijui *mechanism* gani itatumika, lakini sidhani kwamba mahali pazuri ni hapo. Sijui Tume imependekeza hiyo itakuwaje?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *assurance,* mimi sidhani kwamba *Commission* ambayo kwanza hai-*participate* katika kufundisha watu wanaoweza ku-*guarantee quality* ni Chuo chenyewe. Tume inaweza ikatoa *guidance* kwa maana ya kutoa maelekezo na *criteria* za kutekeleza labda na kuweza ku-*monitor* kidogo kwamba zinafuatwa vipi, lakini kwa kweli *eventually* ni Chuo chenyewe na Walimu wake ndio wanaweza ku-*determine* kuhusu *quality*.

Mheshimiwa Spika, suala la kuhusu *Curriculum* kwamba Tume iwe ina-*regulate curriculum* ya Chuo Kikuu, mimi nadhani hicho kidogo baada ya Tume kutoa *umbrella guidance* ya *Curriculum,* wangejiondoa katika ku-*regulate*. Mimi nadhani katika vitu ambavyo vinaathiri utendaji katika Chuo Kikuu ni kukisimamia na ifikie Chuo Kikuu kwamba kinakuwa *controlled* katika utendaji wake wa kutoa elimu. Hiyo ipo katika ukurasa wa 11 ibara ya (5)(c)(ii) kwamba *Commission* ita-*provide guidance* na *general regulation of Curriculum submitted.* Mimi sijui kama kweli hiyo ni kazi yake ya ku-*regulate Curriculum,* lakini wanaweza kutoa *guidance.* Lakini sidhani kwamba ni vizuri sana Chuo kikajisikia kwamba kiko *under the control* ya *Commission* kuhusu *Curriculum* na *product* wanazozitoa na wanazitoa vipi.

Mheshimiwa Spika, ningejisikia vizuri kama nikiwa Chuo Kikuu najisikia kwamba niko huru wa kutoa elimu jinsi ninavyoona inafaa na ninachofuata tu ni kwamba nina *general guidelines* za kufuata. Lakini sijisikii kwamba nina *overall authority* juu yangu inayoni-*supervise* na kuni-*pressurize* kwamba mambo ndiyo hivi yawe au hivi yasiwe. Hayo napendekeza kwanza yatazamwe kwa maana ya kuboresha elimu na kuondoa kama vile *Press* isivyotaka Serikali ndivyo pia navyo elimu na hasa elimu ya juu isivyotaka Serikali kuwa karibu naye na hasa Walimu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niwe miongoni mwa wachangiaji wa Muswada huu ulio mbele yetu asubuhi hii. Kwanza, nami niungane na wenzangu waliotangulia kutuma salam za pole kwa familia za marehemu Diria pamoja na marehemu Bomani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja katika Muswada huu ulio mbele yetu. Kimsingi huu Muswada nasema ni mzuri na ni imani yangu kwamba utatusaidia kwa kiwango kikubwa sana katika kuratibu mtiririko mzima wa mwenendo na utawala wa Vyuo Vikuu katika nchi yetu. Kuja kwa sheria hii kuna umuhimu wa aina yake ukiangalia historia ya Tanzania na mahali ambapo sasa hivi tumefikia kwa idadi ya Vyuo tulivyonavyo.

Ukiangalia hapo zamani ilikuwa panapoanzishwa Chuo, wakati ule Vyuo vikitawaliwa na Serikali zaidi, basi huwa tunatunga sheria ya kuanzishwa Chuo hicho. Kuepukana na mtiririko huo, ndio katika Muswada huu kuna maeneo ambayo yanafuta mtiririko huo wa zile sheria ambazo zilitungwa kuanzisha hivyo Vyuo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, lakini kuna maeneo ambayo kidogo nahisi yalihitaji kufanyiwa marekebisho madogo madogo. Naanza na kifungu cha nne katika *schedule* ile, katika sehemu ndogo ya 3(e) kwa kuzingatia kwamba Muswada au sheria hii inakusudia kutumika Tanzania nzima ambao ndio utakaoratibu mtiririko mzima wa masuala haya ya Vyuo Vikuu, hicho kipengele (e) kinazungumzia *Director of Higher Education.*

Sasa ushauri wangu ni kwamba katika mtiririko wa kielimu kwa upande wa Zanzibar yupo vilevile Mkurugenzi wa Elimu ya Juu. Kwa hiyo ili kuunganisha huu mtiririko ili tufike juu katika *level* ya Chuo Kikuu maana yake tunatoka chini, hizi elimu zinazoanzia huku chini mpaka kufikia katika Vyuo Vikuu, sasa ni vyema kuona haja ya kuweka watu wawili, Wakurugenzi wa Elimu ya Juu ili uratibu uende vizuri katika hii Tume.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili, kwanza hapo nipongeze ile hatua ya kuongeza katika ile Ibara ya 3(b), kushirikisha mshiriki kutoka Vyuo Vikuu vya Zanzibar. Ufahamu wangu sasa hivi ni kwamba kule Zanzibar kuna Vyuo Vikuu vinne. Sasa kuingiza mshiriki mmoja katika hivi Vyuo vya binafsi kwa kweli ni suala ambalo nalipongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hiyo hiyo *first schedule* kipengele (c) na (g) kinazungumzia *one member nominated by the Tanzania Association of the Employers* na (c) kinazungumzia *one member nominated by Tanzania Private Sector Foundation.* Hapa naona lengo ni kuzishirikisha Sekta binafsi pamoja na Waajiri, lakini bahati mbaya sana mtiririko wa sheria zetu za Tanzania, hii sheria inayohusu Waajiri haitumiki pande zote za Muungano. Kwa maana hiyo, upande wa pili wa Muungano utakuwa haukushirikishwa kikamilifu katika suala hili kwa sababu hapa tunapozungumzia hii *Tanzania Association of Employer* itachukuliwa ile *ATE* ambayo inatumika Tanzania Bara.

Sasa kwa upande wa Zanzibar pia ipo *Employer Association.* Hii tunaitazamaje? *Employers* wale watakuwa wameshirikishwaje au sheria hii inawaangaliaje? Vile vile, *private sector* ambapo pia ni sheria tofauti zinazotumika, nazo tunawaangaliaje? Kwa

hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja, naomba atupatie ufafanuzi vipi ataweza kushirikisha upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, halafu katika hiyo hiyo *first schedule* ukienda katika kifungu cha sita ambacho kinazungumzia *quorum*, anasema: *"The quorum at any meeting of the Commission shall be half of the members."* Sasa ikichukuliwa nusu ya hawa Wanachama wa hiyo *Commission* wanaweza kuwa na maamuzi. Nadhani hapa kidogo pana tatizo. Kama nusu itakuwa ni *quorum* wanaweza kuendesha Kikao. Tatizo ni kwamba, ina maana robo itakuwa na uwezo wa kutoa maamuzi. Hili ni tatizo na maamuzi yenyewe ni mazito kama yanayohusiana na utawala mzima wa Vyuo Vikuu.

Kwa hiyo ushauri wangu hapa nadhani *quorum* ingekuwa *too third* ili kuikuza hii namba. Kuweka nusu kama ilivyo, maana yake robo itaweza kuamua. Kwa hiyo, hiyo nadhani si busara njema katika maamuzi mazito kama haya yanayohusiana na utawala mzima wa Vyuo Vikuu na maelezo hayo pia yanakuwa *supported* na hicho kifungu cha saba kinachofuata hapo chini yake ambacho kinaonyesha namna gani maamuzi yanavyoweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya mambo ya *remunerations,* kwa kweli nilivyojaribu kuuangalia huu Muswada naona kama umekaa kimya wakati vile Vikao vya *Commission* vinapokaa. Kwa kawaida tunategemea vikao vinapokaa kunakuwa na posho zinazolipwa, lakini naona hii sheria ipo kimya, haikufafanua kwamba atakayeamua walipwe ni nani, ni Waziri au ni *Commission* yenyewe na ni nani atakaye-*state* hizo *rates* za kulipwa hao wahusika.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia sheria hii hata katika kifungu cha 62 ambapo kimetajwa tu, mambo mengi mbali ya haya ya *remunerations*, kuna mambo ya hizo *benefits, terminal benefits* katika kifungu cha 62(h)(i). Hapa kidogo mimi nashindwa kufahamu. Kwa kawaida masuala yanayohusiana na mafao, zipo sheria zinazotawala. Hii ni Taasisi ya Umma. Pengine kuna zile sheria kama *PPF* na zipo nyingine ambazo zinahusiana na masuala ya *benefits* zinalipwalipwaje. Sasa hapa hatuzungumzii vipi zitalipwa *terminal benefits,* sijui wata-*set* kinamna gani hizo *rates* na kwa utaratibu upi wakati zipo sheria ambazo zinazungumzia mambo ya *terminal benefits*.

Kwa hiyo na hili pia ningemwomba Mheshimiwa Waziri kidogo atusaidie ufafanuzi, hivi kawaida masuala kama haya yanakuwaje wakati sheria zinazohusika na mambo kama haya zipo. Hata wenzangu wamelizungumzia suala hili. Katika hiyo *first schedule, section* ya pili inazungumzia zile sheria ambazo zinafutwa. Wamezungumza na hata Msemaji wa Upinzani alizungumzia ile Sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu cha Zanzibar.

Kwanza kuwepo kwa sheria ile mimi sina tatizo nayo kwa sababu pamoja na kuelezwa kwamba masuala haya ni ya Muungano lakini vilipoanzishwa Vyuo Vikuu vingine vyote zilitungwa sheria. Chuo Kikuu cha Mzumbe ipo sheria; *Open University* ipo sheria, kwa maana hiyo haikuwezekana na hakukuwa na njia nyingine ya sheria ile kwamba uanzishe Chuo Kikuu bila kuwa na sheria, kitu ambacho hakiwezekani. Lakini

sasa katika huu utaratibu mpya tunaouzungumzia sasa hivi utawala wake utakuwaje? Hapa nadhani kidogo panahitajika ufafanuzi na pengine Mheshimiwa Waziri angekuja kutufafanulia uendeshaji wake utakuwaje.

Mheshimiwa Spika, halafu kifungu cha 51 kinachozungumzia kuhusiana na Vyuo kujiingiza katika mambo ya kisiasa, hapa kidogo napata matatizo kwamba kwa tafsiri ya hii sheria naona imekwenda mbali sana kiasi ambacho katika kifungu kidogo cha pili inazungumzia: "*Staff association includes its members"* na (d) inazungumzia: *"Student organization includes its member"*. Sasa naona imekwenda mbali zaidi mpaka inawabana mtu mmoja mmoja. Wasiwasi wangu nilionao hapa ni kwamba, ile *freedom of association,* kiujumla hiyo haina tatizo, lakini ile nafasi ya mtu mmoja mmoja. Kwa maana hiyo hapa hata kama watu wamekutana wa Chama kimoja pengine wamekaa katika chumba chao ndani ya Chuo wanaangalia mkanda unaohusiana na shughuli za kisiasa, ninavyoona kwa kifungu hiki kitazuia.

Sasa kidogo tungeangalia zaidi kwa kiwango gani kifungu hiki hatutapingana na matakwa ya Katiba kuhusiana na uhuru wa mtu binafsi kwa sababu hapa tunazungumzia *staff association* ina *include its members* na *student organization includes its member.* Sasa hapo tungeangalia kwa kina ili kutoingilia uhuru wa mtu binafsi kwenye masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 35 cha sheria hii kidogo naomba tufanye masahihisho pale kinapomtaja *President* ikiwa inamaanisha wa *United Republic of Tanzania* na *Revolutionary Government of Zanzibar*, inakuwa ni *President of Zanzibar* siyo *President of Revolutionary Government of Zanzibar.* Hili neno *Revolutionary* na *Government* yanaondoka. Hiyo ipo katika kifungu cha 35, *subsection (1) and (2).* Vile vile, hiyo inajitokeza tena katika *section (3)* kwenye *interpretation*. Katika *interpretation* pale ukurasa wa tisa neno la mstari wa pili inapokuwa *defined President,* pale napo kidogo nahisi maneno hayo yangefanyiwa masahihisho ili hilo neno lisomeke kwa usahihi wake na pia kama lilivyoelezwa katika Katiba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo kufanyiwa kazi, mimi nitaiunga mkono sheria hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza naomba nami niungane na wenzangu kutoa pole na salaam za rambirambi kwa misiba iliyotupata na Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema Peponi waliofariki. Amen.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wizara kwa kufikisha Muswada huu Bungeni na tunaujadili hivi sasa. Muswada ni mzuri na madhumuni yake, malengo yake ni mazuri kwa maana kwamba unataka ku-*keep standards* na ku-*standardize* vitu ambavyo tutakuwa tunavielewa kwa namna moja. Basi hilo ndilo ambalo nilikuwa nafikiri lilitakiwa kuonekana vizuri zaidi ndani ya huu Muswada.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwanza kwa yale ya ujumla, labda tu niseme kwanza suala la Rais kuwa *Chancellor* mimi nafikiri Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza hapa. Nafikiri kwa kweli sasa hivi muda si muafaka kwa Rais kuwa *Chancellor* na sababu zilizofanya wakati ule *Chancellor* awe ni Rais, ni tofauti sana na sasa hivi. Sasa hivi kuna *dynamism* ambayo inafanya kabisa Rais awe kwanza hana nafasi, lakini pia, kama unataka ku-*standardize*, ni kuondoa ile *inferiority* ya Vyuo hivyo ambavyo havitakuwa na *Chancellor* ambaye ni Rais kwa sababu tayari utakuwa ni kama umeviweka kwenye *awkward position.*

Lakini niseme tu pia kwamba kwa mfano, kuna mahali ambapo sasa hivi sikumbuki wanasema, Rais atakuwa *Chancellor* na mimi nasema haifai, lakini wanasema anapoondoka madarakani anakoma kuwa *Chancellor*. Sasa nataka niseme kuna *confusion.* Pia nafikiri anayekuwa *Chancellor* sio mtu, ni Rais na nafasi ya Urais ipo kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi na hata vipindi vinavyomalizika vya uchaguzi nafasi ya Urais haisiti inaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, nianze kuzungumzia Muswada wenyewe kwa kiwango ambacho nitafanikiwa kufanya. Nianzie kwanza kwenye *functions* za *Commission* kwenye hiyo Ibara ya tano. Nasema nafikiri *functions* hizi zinakubalika isipokuwa iliyo chini ya 5(1)(c), kidogo nafikiri na kwa kweli ingependeza kama isingekuwepo kabisa. Kama itaondolewa hakutakuwa na madhara na kama unataka *Universities* kwanza ziwe na *identity* yake kwa sababu pamoja na kuwa tunataka ku-*standardize* lakini hatuna maana kwamba tunataka wote kuwaweka wawe wanafanana kwa kiwango ambacho itakuwa bakuli ni bakuli, sahani ni sahani, rangi ile ile, hapana. Kila Chuo bado kinatakiwa kuwa na *minimum necessary standards*, lakini kinaweza kikiwa na nafasi hiyo ya kuwa na vitu ambavyo vinakifanya kiwe *peculiar* na *more interesting.*

Sasa unapokuwa kwa mfano unasema *criteria for student admission to University,* unaweza uka-*set minimum standards* ambazo zinafahamika. Hata hivyo, kwa mtindo wetu wa elimu lakini haya ndio mengine ambayo nafikiri huwa yanaharibu hata *purpose* yenyewe ya kuwa na Chuo Kikuu. Unapokuwa unasema hivi, maana yake ni kwamba unataka utamke kabisa kwamba atakayeingia Chuo Kikuu ni mtu fulani.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niwape mfano. Nilipokuwa nafundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tulikuwa tunafanya hizi ma*triculation examinations*, wamekuja watu ambao wana viwango vizuri kweli kweli vya kufaulu lakini walivyokaa pale mbele unaongea naye unashangaa kabisa amepita wapi huyu mpaka akapata hizi *credits* zote? Kwa kweli unashangaa. *On the same coin* unaweza kuzungumza kile alichokizungumza Mheshimiwa Kabourou kwamba, wanakuja watu ambao wamepita ulimwenguni wamekusanya *experience* na maarifa ambayo sasa wanataka kuya-*formalize* kwenye *education* ya kiwango cha Chuo Kikuu, wanakuja pale hawana hizi *credits* ambazo wewe umezitamka. Unawaweka kwenye *matriculation examination,* wanafanya vizuri lakini bado unataka u-*demand* tena vitu vingine.

Nafikiri hii ina-*defeat purpose* nzima ya kuwa na Chuo Kikuu. Chuo Kikuu panatakiwa kuwa ni mahali ambapo kwanza inawezekana kabisa mtu anakuja na falsafa

yake isipokuwa anataka kwenda kui-*formalize*. Siyo lazima pawe ni mahali ambapo mtu anakwenda kukaa darasani na kuanza kufundishwa vitu kama Darasa la Kwanza, ila hasa ni mahali ambapo pia inawezekana mtu pia amepita ulimwenguni lakini anataka kwenda ku-*formalize* maarifa yake.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ningependa kusema tu kwamba ile Ibara ya 5(1)(c) kwa kweli mimi nafikiri inaweza kuondoka bila utata wowote na ile (iv) wanasema: *"Recurrent and development budget for public universities."* Mimi nafikiri hii italeta matatizo.

Kwanza hivi sasa tu Vyuo Vikuu vyote wana matatizo kweli kweli ya kupeleka mahitaji yao Wizarani na hatimaye kusikilizwa na kupata viwango wanavyotarajia. Sasa unapoongeza mtu mwingine katikati hapa, ndio kabisa kabisa inaanza kuwa-*subject* kwenye *censorship* ambayo haitakuwa na maana kabisa. Mimi nilikuwa nafikiri hili nalo kwanza litaongeza mlolongo na nafikiri moja kati ya vitu ambavyo tunatakiwa ku-*achieve* katika kupitia hii sheria ni pamoja na kupunguza mlolongo huu ambao wakati mwingine unachelewesha tu na ufanisi unakuwa mdogo. Kwa hiyo, nafikiri hili nalo linaweza kuondoka bila madhara yoyote.

Mheshimiwa Spika, kile kifungu cha 5(1)(f), mimi nakipongeza sana na ndicho nilichoongea kwamba iwe *possible* kwa mtu ku-*transfer* kutoka Chuo kimoja kwenda kingine na vile vile tulishakuwa na wanafunzi wanao-*transfer* kutoka hapa wanakwenda Vyuo vya nje. Kwa nini isiwe inawezekana kufanya kitu kile kile hapa hapa nchini? Kwa hiyo nafikiri nalipongeza hilo. Isipokuwa hili la (g) kidogo limenistua. Hapa wanasema: *"To levy fees or any other form of charges for specific services, facilities and documents rendered or supplied to Institutions".*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nafikiri hapa kama hii *Commission* ipo, kwanza ipo juu ya *Universities*, kwa hiyo ina-*dictate. In fact* ukiangalia *functions* zake ni kama hivyo itakuwa ina-*dictate* tu *under* hiyo sifa kwamba ina-*advise* halafu wata-*render services* ambazo hazitakiwi kabisa na *Universities and then* bado itawa-*bill*. Hii uliona wapi? Nafikiri hii haifai kabisa! Inatakiwa kuondoka tu!

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa 12 *under the same functions of the Commission*, kifungu cha (n) wanasema: *"To initiate, regulate and standardize."* (i) anasema: *"Promotion criteria, designations and titles over academic and senior administrative staff."* Nafikiri hii ni nzuri na hii naipongeza sana kwa sababu hii haswa ndio italeta vile viwango ambavyo mimi naviita *minimum necessary* kwamba ukimwona *Senior Lecturer* hapa atakuwa na viwango vile vile kama alivyonavyo *Senior Lecturer* mwingine.

Ukimwona Profesa atafahamika vile vile, sio kama sasa hivi tuna Maprofesa ambao wana viwango tofauti au tuna *Lecturers* ambao wanakuwa na sifa tofauti vile vile. Kwa hiyo hii naipongeza sana. Isipokuwa tu nilikuwa nafikiria pale wanaposema: *"To initiate, regulate and standardize,"* mimi nilikuwa nafikiri lile neno *"initiate"* waliondoe kwa sababu nafikiri anayetakiwa ku-*initiate if at all* wanatakiwa kuwa ni *Universities* ambao watasema kwamba *now, look;* tume-*grow* kiasi hiki, sasa tunafikiri tunahitaji kitu

fulani, *and those are ones who were going to initiate not the Commission as such.* Sasa watakuwa *advised* wao wasiseme kwamba wame-*initiate,* wata-*initiate* kule chini.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda sasa nizungumzie kuhusu ibara ya 12(2)(c) inayohusu *Admission Committee*. Hii *Admission Committee* ni moja kati ya Kamati tatu zilizotamkwa mwanzo hapa kwenye hii *Commission.* Sasa hii A*dmission Committee* ina kazi ambazo itazifanya hiyo ya (c) ambayo na Mheshimiwa Dr. Mbise ameiongelea amesema *the provision of central admission services to Universities,* nafikiri hii ni *wrong* kabisa.

Kwanza ina-*defeat* tena kama nilivyosema *purpose* ya kuwa na Chuo Kikuu na ile *individualism* ambayo unataka kila Chuo ki-*attain* kama kinaweza na kwa kweli utawezaje kufanya hivyo. Utakuwa na mtambo wa *admission* ya wanafunzi hapa halafu unapeleka huko! Haijawahi kutokea hiyo na sidhani kama utakuwa unafanya! Hiyo siyo elimu ya Chuo Kikuu. Chuo Kikuu anakwenda mtu yeye mwenyewe anajieleza pale pale na anaonekana pale pale na anapewa nafasi inayolingana na yeye na anakuwa *admitted* kwenye level ambayo inafanana na kiwango alichonacho na kwa *attainment* anayoitaka. Kwa hiyo nilikuwa nafikiri hili halistahili kabisa kuwepo.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna hiyo sehemu ya (g) wanasema: *"Development of strategies for curbing cheating and forgery in higher education."* Mimi nasema nimefundisha, *I really wonder!* Unawezaje ku-*develop strategy* ya *cheating* in a *centralize manner! How can you do that! You can't!* Haiwezekani kwa sababu wewe ni Mwalimu unafundisha, una mtihani wako, kama ume-*leak*, ume-*leak* kwako wewe mwenyewe. Ni *ethics* tu ambazo zinatakiwa kumwongoza huyu anayekwenda ku-*examine* hawa wanafunzi.

Sasa ku-*standardize,* sijui uta-*standardize* namna gani kwenye *level* hii. Mimi nafikiri hii labda kama ina maana nyingine, lakini nafikiri haina haja kabisa kuwepo hapa. *There is no way,* unaweza kuwa na njia ya ku-*centralize* ya ku-*curb cheating*. Zile *ethics* ambazo ziko pale zinatakiwa kumwongoza *Lecturer* na kufahamu kabisa kwa sababu amepewa majukumu na lazima aaminiwe na kama *"if at all",* basi kunatakiwa kuzungumza kwenye *level* hiyo, siyo kwenye *level* ya kuja kuangalia wanafunzi. Maana yake mitihani ya Chuo Kikuu na taratibu ya Chuo Kikuu ni tofauti kabisa na Shule hizi za awali ambazo nafikiri ndiyo kuna matatizo hasa ya udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka niseme kwamba nitafanya *submission* tena kidogo ya maandishi kwa baadhi ya maeneo ambayo *specifically* nilikuwa napenda niyaongelee. Labda nirukie tu hili moja la *political party activities* kwenye *campus*. Mimi nili-*support.* Nafikiri wenzangu walioliongelea labda hawakuliangalia kwa makini. Hawajazuiliwa watu kufanya siasa kwa sababu *by nature human being* na *particularly* unapokuwa na maarifa zaidi wewe ni *homopoliticus.* Ikiwa huwezi kufikiria kwenye *level* hiyo, basi *you have no use being in any University.*

Lakini kinachoongelewa hapa ni jinsi gani uta-*channel* vitu vya namna hiyo na kama unaruhusu sasa mtu awe na upande pale pale kwenye *campus* unaleta vurugu. Maana yake hilo ndilo linalozuiliwa hapa na mimi nasema kifungu kimekaa sawa sawa kabisa. Nafikiri watu wasiliangalie kwa jazba kidogo, waliache hivyo hivyo nafikiri limeangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naona bado nina muda, kuhusu hizi *appointments* na *qualifications*, kuna mahali wamesema, kwa mfano, *Chancellor* awe *equivalent* au *Deputy Vice Chancellor* awe *equivalent* au *Principal* awe *equivalent*. Nilikuwa nafikiri kwa sasa hivi wala haina haja na hilo neno *equivalent.* Nafikiri lingeondoka tu kwa sababu ni hili neno *equivalent* ndio linasababisha na *standards* zinaanza kuwa *double standards*.

Nilikuwa nafikiri hili neno liondolewe kila mahali lilipo na *particularly* kwa mfano ukija kwa *Vice-Chancellor, Deputy Vice-Chancellor, Principals, Deputy Principals* na watu wengine wa *rank* ya kiwango hicho zile sifa zilizoainishwa kwenye *Clause* 36(3) ndiyo zinatakiwa ku-*apply* kwao wote, watakuwa watatu, watakuwa wamepatikana kuzi-*assist Committee,* wawe na sifa na viwango vile vile, maana yake nimeona vinakwenda vinabadilika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Msekela, kama ulivyosema kwamba una *points* nyingine unataka kuziwasilisha kwa maandishi, bado unaweza ukafanya hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi na Wasemaji wote walioomba kuchangia kwa mdomo wamemalizika. Kwa hiyo, Mheshimiwa mtoa hoja ajiandae tu, tutakaporejea saa 11 aweze kuhitimisha hoja yake. Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilifungwa saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*(Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**Muswada ya Sheria ya Uendeshaji wa Vyuo Vikuu wa Mwaka 2005**
***(The Universities Bill, 2005)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu muhimu. Napenda kuchangia haya yafuatayo:-

Kwanza naomba utekelezaji uzingatie dhamira nzuri iliyomo kwenye Muswada na mabadiliko yafanywe kwa uangalifu ili yasilete migogoro na malalamiko miongoni mwa wadau. Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa rambirambi kwa ndugu na jamaa wa Marehemu Ahmed Hassan Diria na Mzee Paul Bomani, napenda kukupongeza wewe, Naibu wako, Katibu Mkuu na Wasaidizi wenu kwa Muswada uliotayarishwa na kuwasilishwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kuboresha Muswada kama mtakubaliana na maoni yangu yafuatayo:-

Kwanza, katika ibara ya tano kumeorodheshwa shughuli 17 za Tume. Mimi naona ni nyingi na ninashauri shughuli zifuatazo ziachiwe Vyuo vyenyewe: (i), (f), na (k)

Pili, kwa kuwa kwenye ibara za 4(2)( c) na 45 Sehemu ya V (2)(d) kumetajwa suala la mikopo kama vyanzo vya fedha. Lakini kwenye Ibara ya 16, mikopo haikutajwa. Nashauri iongezwe ibara 16(e) itakayoorodhesha mikopo kama moja ya vyanzo vya fedha.

Tatu, Ibara ya 17(2)(b) imetamka malipo kwa Wajumbe wa Tume kuwa *REIMBURSEMENT (marejesho)*. Hii siyo sawa. Wajumbe wanastahili kulipwa posho ingawa ndani yake inawezekana kuwemo marejesho ya gharama.

Nne, Ibara ya 39(9) inaweka muda wa ajira ya Makamu wa Chuo kidogo *(University College)* kuwa miaka mitatu. Huu ni muda mfupi usioruhusu usimamizi endelevu. Nashauri iwe miaka mitano.

Tano, Ibara ya 46 Sehemu ya Tano inayoelezea Muundo wa Baraza la Taaluma *(Senate Committee)* haizingatii suala la jinsia. Nashauri Wanawake wahusishwe.

Sita, kwenye ibara ya 1(5) ya Jedwali la Kwanza *(1st schedule)* kumetolewa nafasi 2 mbili za Wawakilishi wa Serikali ya Mapinduzi. Kwa misingi ya Na(5) hapo juu nashauri sheria itamke kuwa mmoja wa hao awe mwanamke.

Saba, Jedwali hilo hilo Na. 1(i) linampa madaraka Waziri ya kumteua Mwenyekiti wa Tume. Sikubaliani na madaraka hayo kupewa Waziri, kwani Mwenyekiti wa Tume anaongoza Vyuo Vikuu. Haiwezekani yeye ateuliwe na Waziri wakati wadogo zake wanateuliwa na Mheshimiwa Rais. Nashauri Mwenyekiti wa Tume ateuliwe na Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, katika Jedwali la pili, Ibara ya Nne inasema kuwa Ukatibu wa Kamati ya Makamu wa Vyuo Vikuu utafuatana na Uenyekiti ambao utakuwa wa mzunguko wa miaka miwili miwili. Sina tatizo na mzunguko wa Uenyekiti. Lakini sikubaliani na mzunguko wa Ukatibu kwa kuzingatia kuwa kila Katibu atasimamia vikao viwili tu kufuatana na Ibara ya 6(i) ya Jedwali hilo.

Mheshimiwa Waziri naiunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo ninayo machache ya kuboresha Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kutunza viwango sawa na kurahisisha usimamizi na utambuzi, pale palipoandaliwa: *"or equivalent designation"* maneno hayo yafutwe na ibakie jina moja tu linalotambulisha cheo kwa madaraka yaliyokusudiwa kwa cheo hicho. Mfano ni ibara ya 34 ambapo napendekeza hayo maneno ya *"or equivalent designation"* yafutwe. Kwa mantiki hiyo basi, hilo lifanyike katika vifungu vingine vyote vilivyoandikwa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 35(1) kinatamka kwamba Rais wa Muungano au Rais wa Zanzibar aweza kuwa *Chancellor* wa *University* ya Serikali. Nadhani umuhimu wa hilo sasa haupo. Isitoshe, kwa kuwa Vyuo Vikuu vipo chini ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ambayo inaongozwa na Waziri aliyeteuliwa na Rais, basi mtiririko wa uongozi unapoteza murua wake pale tena Rais anapokuwa Kiongozi wa Taasisi iliyo chini ya Waziri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama matokeo ya mabadiliko ninayopendekeza katika ibara ya 35(1), basi ibara ya 35(2) itarekebishwa ili isomeke kwamba, *"Chancellor wa Chuo Kikuu cha Serikali atateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano au Zanzibar, kama itakavyotegemea kilipo chuo hicho, ama Bara, ama Visiwani."* Kwa mantiki hiyo hiyo ya mabadiliko niliyopendekeza katika ibara ya 35(2), basi sehemu ya (b) ya 35(2) ifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 35(5) kinatamka kipindi cha *Service* cha *Chancellor* kwamba kitaainishwa katika *Charter of the University.* Nadhani hii haina madhara kama marekebisho niliyopendekeza katika 35(1) yatazingatiwa vinginevyo kipindi hicho tayari kipo na ni milele, kipindi ambacho Rais anadumu katika madaraka kwa Vyuo vya Serikali. Kwa Vyuo binafsi, busara inaonyesha kuwa miaka mitano itakuwa ni kiwango cha juu ambacho *Charter* zinaweza kuonyesha. Hata hivyo, kwa ajili ya mlingano wa usimamiaji, ni bora 35(5) itamke miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 35(6) hakina ustahili wa kuwepo kwani "Rais" ni nafasi ambayo mtu huitumikia kwa kipindi kilichoainishwa na Sheria ya Uchaguzi, lakini sheria hiyo haisitishi kuwepo kwa Rais baada ya mtu huyo kuondoka katika madaraka ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 36(5) napendekeza isomeke:-
*"A V.C. of any University shall hold office for a term of 5 years and be elegible for re-appointment for only one more such term".* Pendekezo hili linatoa nafasi ya uendelevu wa uongozi wenye mafanikio katika utekelezaji wa mikakati ya muda wa kati lakini pia pendekezo linalenga katika kuhimiza uongozi shirikishi na pia kukuza ubunifu na kukaribisha ari mpya na ubunifu mpya mapema zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uteuzi na sifa za *Deputy Vice-Chancellor,* napendekeza kifungu cha 37(4)(a) kiandikwe upya ili kifanane na kifungu cha 36(3). Kuhusu kipindi cha *Deputy Vice-Chancellor* kutumikia nafasi hiyo, napendekeza iwe kipindi kimoja tu cha miaka mitano. Baada ya kipindi hicho, watu hawa wanaweza kuchaguliwa tena katika nafasi hiyo baada ya kuwa nje ya nafasi hiyo kwa walau kipindi kimoja cha miaka mitano. Pendekezo hili linalenga katika kujenga *pool* ya Viongozi na nafasi sawa kwa wanataaluma ambao ni wengi sana. Tutumie uwingi wao kupata *diversity* ya Uongozi ambao hakika utakuwa *dynamic* na *innovative*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Mkutano huu kuchangia hoja naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge walionitangulia kutoa rambirambi kutokana na vifo vya Waheshimiwa Ahmed Hassan Diria, Mbunge wa Rahaleo na Balozi Paul Bomani, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa niaba ya Wanawake wote wa Mkoa wa Dodoma natoa pole nyingi kwa ndugu, jamaa, marafiki na familia ya Marehemu. *Subhana-huwa-taala* awape subra na tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho zao mahali pema Peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kusema kuwa naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Ningependa kuchangia kwa kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambazo zimejibiwa kwa kuzingatia *theme*.

Mheshimiwa Prof. Mwaga na Mheshimiwa Lubeleje walikuwa na hoja zifuatazo kuhusu orodha ya aina ya Vyuo iliyopo, ibara ya 19 kifungu cha pili, kuwa havina tofauti. Tofauti ya Vyuo iliyopo ibara ya 19(2) ni ya kimuundo zaidi ambapo inatoa fursa kwa Vyuo Vikuu vilivyopo kushirikiana na Vyuo ambavyo sio Vyuo Vikuu kamili au kuanzisha Vyuo vishiriki ambavyo vitasimamiwa na Vyuo Vikuu vyenye Ithibati. Utaratibu huu si mpya na unatumika sehemu nyingi duniani. Orodha ya sheria za kufutwa Baraza la Ithibati imesahauliwa. Sheria hiyo imeorodheshwa katika jedwali la tatu katika *amendments*. Aidha, kuhusu namna ya kumpata Mtendaji Mkuu haijaelezwa wazi. Walipendekeza utaratibu wa *Search Committee* utumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kumpata *Executive Secretary* upo katika jedwali la marekebisho fungu (f). Pia kulikuwa kuna hoja walipendekeza kuwepo kwa utaratibu mwingine kutoa fursa ya wafanyakazi kulipwa mafao yao. Katika kipindi cha mpito Tume itachambua idadi ya wafanyakazi inayokusudia kuendelea nao. Hii ni kutokana na sababu mbalimbali. Moja, kuepuka Tume kushindwa kutekeleza majukumu yake; pili, kuipa Tume muda wa kujenga uwezo na tatu, ni sababu za kibajeti.

Mheshimiwa Talala Mbise alikuwa na hoja mbili zifuatazo: Kwanza alitoa hoja ya *centralised admission* ibara ya 5(1)( c)(i ). Kitakachofanywa na Tume kuhusu udahili ni kuratibu shughuli za udahili ili kuona kwamba viwango na vigezo vinavyohitajika katika udahili vinazingatiwa na wala sio kufanya udahili kwa niaba ya Vyuo.

Kulikuwa na hoja pia ya ulipaji wa ada kwamba utokane na *credit hours* badala ya wanafunzi kudahiliwa Chuoni. Wazo hili ni zuri lakini linahitaji kufanyiwa utafiti kabla ya kutekelezwa, kwa sababu hoja hii imejengwa katika dhana kuwa Vyuo vyetu vina wanafunzi wa kutosha na kuna ufanisi mkubwa katika Vyuo hivyo. Aidha, hali halisi ya Vyuo vyetu vingi hasa vya binafsi ni vichanga na gharama za uendeshaji ni mkubwa. Utaratibu wa kulipa ada kwa kutumia *credit hours* unaweza kuathiri uendeshaji wa shughuli za Vyuo.

Mheshimiwa Athumani Janguo yeye alikuwa na hoja ifuatayo:- Alipendekeza kuwa miaka mitatu ya Uongozi wa *Deputy Principal* ni mfupi na uwe miaka mitano. Ili kuhakikisha maendeleo wa shughuli za Chuo wakati Viongozi wanapoacha madaraka ni muhimu. Vipindi vya Uongozi kutoka ngazi ya juu yaani ya *Vice-Chancellor* hadi kwenye cheo cha *Deputy Chancellor* viwe tofauti.

Mheshimiwa Kamala, Mheshimiwa Haji Mwita, Mheshimiwa Mutungirehi na Mheshimiwa Zahor walikuwa na hoja zifuatazo na ilikuwa masuala ya kisheria. Kufutwa sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu cha Zanzibar, Sheria hii haijatajwa kati ya sheria zinazohitaji kufutwa katika Muswada huu kwa vile sheria hiyo haikutungwa na kupitishwa na Bunge hili. Hata hivyo sheria hii ikianza kufanya kazi sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu cha Zanzibar itakuwa *redundant*. Hoja ya msingi baada ya sheria kuanza kutumika ni wakati wa *accreditation* ambapo vigezo sharti vifuatwe. *State University of Zanzibar* watahitajika pia masharti ya sheria hii.

Mheshimiwa Mutungirehi alikuwa na hoja kwamba kuwepo chombo cha Kitaifa kitakachounganisha wanafunzi. Pendekezo hili limekubaliwa na litazingatiwa katika ibara ya 62(1) kinachompa mamlaka Waziri kutengeneza Kanuni. Kwa hiyo wazo limechukuliwa.

Mheshimiwa Kamala alikuwa na hoja kwamba sheria iliyoanzisha Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu haijatajwa kati ya sheria zinazofutwa. Sheria iliyoanzisha Baraza ni kati ya sheria zinazofutwa na imetajwa katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwaga, Mheshimiwa Zahor na Mheshimiwa Mjaka wao walikuwa na hoja inayohusu suala la wafanyakazi wa Baraza. Baada ya sheria hii kuanza kutumika, wafanyakazi wa Baraza watakuwa wafanyakazi wa Tume. Hivyo, madai yao yote kama yatakuwepo yatashughulikiwa na Tume na sio Baraza tena maana Baraza litakuwa halipo tena mara baada ya kuanza kutumika kwa sheria hii.

Mheshimiwa Mutungirehi, Mheshimiwa Mjaka, Mheshimiwa Kabourou na Mheshimiwa Dr. Msekela wao walikuwa na hoja ya kupigwa marufuku shughuli za kisiasa katika Vyuo. Serikali inaamini kuwa ni muhimu kudhibiti shughuli za kisiasa katika maeneo ya Vyuo kwa mujibu wa ibara ya 5(2)(b). Vyuo Vikuu ni sehemu ya taaluma na sio sehemu ya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mahali pengine shughuli za kisiasa zilikuwa na athari kubwa na hata kutishia amani na utulivu. Hivyo ni muhimu shughuli za kisiasa zikadhibitiwa ili kutoa fursa kwa wanafunzi na wahadhiri kushughulikia zaidi masuala ya taaluma.

Mheshimiwa Ndaboine, Mheshimiwa Janguo, Mheshimiwa Zahor, Mheshimiwa Mbise, Mheshimiwa Dr. Msekela na Mheshimiwa Prof. Mwaga walikuwa na hoja inayohusu majukumu ya Tume kwamba suala la ubora wa elimu na mitaala liachiwe Vyuo badala ya Tume. Ubora wa elimu na mitaala utaendelea kuratibiwa na Tume kwani Tume ni chombo cha udhibiti.

Vile vile, kulikuwa kuna hoja kwamba kwenye kifungu 16(e) kiongezwe kifungu kingine kinachohusu mkopo kama vyanzo vya mapato. Pendekezo hili limezingatiwa sasa katika jedwali la marekebisho. Pia, kulikuwa kuna hoja katika kifungu cha 17(2) kwamba kisomeke “Posho za Wajumbe wa Tume.” Pendekezo hili pia limezingatiwa katika jedwali la marekebisho kwamba katika jedwali 1.5 kuhusu Wajumbe wa Tume. Jedwali hilo sasa limefanyiwa marekebisho ambapo kumeongezwa Wajumbe wengine ambao ni wanafunzi wawili, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mkurugenzi wa Elimu ya Juu kutoka Zanzibar. Vile vile, kulikuwa kuna hoja kwamba jedwali la pili, Katibu wa Kamati ya Makamu Wakuu wa Vyuo na Vyuo Vikuu Vishiriki awe wa kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapendekeza pasiwepo Katibu wa kuajiriwa kwa sababu za kibajeti na pia kwa sababu Kamati hii hukutana kwa wastani wa Vikao vitatu tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Kamala alizungumzia kuhusu uteuzi wa *Chancellor*. Katika uteuzi wa *Chancellor* sifa zinazohitajika kwa majina matatu yanayopendekezwa zitabainishwa katika *regulations* ambazo zitakuwa mwongozo wa *Search Committee.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena nashukuru kwa nafasi uliyonipa na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kuwashukuru wote waliochangia katika hoja hii. Ninapenda niwatambue waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati za Huduma za Jamii; Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Msemaji wa Upinzani; Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Dr. Aman Kabourou, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mheshimiwa Zahor Mbaruk Khamis na Mheshimiwa Dr. James Msekela. *(Makofi)*

Napenda kuwashukuru sana kwa michango mizuri kabisa ambayo nawahakikishieni imeboresha sana hoja yetu kwenye Muswada huu na mengi tumeyazingatia kama mlivyoona katika majibu yetu ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri. Napenda kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa hapa mbele yetu katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitakuwa na mengi ya kusema. Aidha, ningependa niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa Dr. James Msekela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inathamini michango yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambayo imechangia sana kuboresha Muswada wa Sheria ya Vyuo Vikuu. Kamati ya Huduma za Jamii ilitoa mapendekezo 13 kuboresha maeneo mbalimbali ya Muswada. Maeneo hayo ambayo yamezingatiwa ni majukumu ya Tume ya Vyuo Vikuu, idadi ya Kamati za Tume, uteuzi wa Viongozi wa Tume wa Vyuo Vikuu, hatma ya wafanyakazi wa Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu wakati kipindi cha mpito na viwango vya adhabu kutokana na ukiukwaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni yote ya Kamati yamezingatiwa katika jedwali la marekebisho ya Muswada ambalo limewasilishwa mbele ya Bunge lako. Katika kutafakari wakati wa kujibu hoja hizi tulipokutana, tumeona mambo mengine mengi baadaye ambayo tutayafanyia marekebisho lakini kuboresha zaidi Muswada wetu. Lakini kwa leo haya ambayo tunayapata hapa yameweza kuboresha hoja yetu. Aidha, Kamati ilipendekeza kuwepo kwa kiwango cha adhabu kwa makosa ya kuendesha shughuli ya kisiasa katika maeneo ya Chuo. Nafurahi kuliarifu Bunge lako kuwa maoni haya yamezingatiwa katika ibara ya 58. Hoja zifuatazo zilipendekezwa na Msemaji wa Upinzani Mheshimiwa Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa *(TLP)*. Kwanza Umoja wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu *Upper Students Organisation* itawekwa bayana katika Kanuni.

Pili, Mjumbe mmoja wa Baraza la Wawakilishi anachaguliwa na Baraza husika naye atakuwa Mjumbe wa Tume ya Vyuo Vikuu. Wawakilishi wawili kutoka Umoja wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu mmoja kutoka Zanzibar na mwingine kutoka Tanzania Bara watakuwa Wajumbe wa Tume ya Vyuo Vikuu. Ibara ya 35 aya ndogo ya kwanza

mapendekezo ya Rais kutokuwa Mkuu wa Chuo Kikuu imekubaliwa. Sasa Rais hatakuwa Mkuu wa Chuo ila atateua Wakuu wa Vyuo katika Vyuo vya Umma. *(Makofi)*

Chuo cha Taifa cha Zanzibar kilichoanzishwa kwa sheria Na.8 ya mwaka 1999 sheria yake haiwezi kufutwa na Sheria ya Vyuo Vikuu kwa sababu haikupitishwa na Bunge hili kama Naibu Waziri alivyosema. Hivyo Chuo kilichotajwa na vingine vimepewa miezi 18 kama vilivyoorodheshwa katika *fourth schedule clause seven* kuzingatia utekelezaji wa sheria hii.

Pia ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mutungirehi na Bunge lako Tukufu kwamba hakuna sheria yoyote ambayo inapitishwa ama imevunja Katiba ya Tanzania kwa sababu kama watu binafsi wanaweza kuanzisha Vyuo wakavimiliki, bado wanahitajiwa kupata kibali kutoka kwetu. Serikali ya Zanzibar inaweza kuhimili Vyuo vyake lakini haviwi Chuo Kikuu mpaka vimepata Ithibati kutokana na Sheria ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo kwa hali hiyo masuala ya Muungano hayatavunjwa Kikatiba kwa sababu bado udhibiti unakuwa hapa hapa na ndiyo maana ya sheria hii kuhakikisha kwamba Vyuo vyote vinadhibitiwa kutoka hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 36(2) uteuzi wa Makamu wa Mkuu wa Chuo kwa kuhusisha *Senate* na Baraza ni utekelezaji wa sera ya Elimu ya Juu ya kuipatia Vyuo mamlaka zaidi ya kuendesha mambo yao ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadau wengi katika uteuzi wa Viongozi wao. Utaratibu huu utasaidia wapatikane Viongozi wenye sifa na wanaowajibika. Kwa makusudi kabisa tumefanya majibu yetu yawe mafupi kwa kuzingatia kwanza muda; pili na kuheshimu mawazo na ushauri uliotolewa na Wabunge. Kwa hiyo, napenda kuhitimisha kwa kutoa hoja kwamba baada ya maelezo yangu haya naomba sasa Muswada huu ukubalike kwenye Kamati na baadaye ufike katika hatua ambazo zinafuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Shughuli za Kamati zinaanza, lakini kabla Katibu hajaendelea, niwaarifu tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna marekebisho ambayo yanaendelea kugawiwa sasa hivi, nadhani baada ya michango yenu asubuhi Serikali imeona ni vizuri ifanye marekebisho. Ndiyo hayo yanagawiwa sasa hivi naomba myaangalie.

Waheshimiwa Wabunge, pia kama mnavyoona Muswada huu ni mrefu sana, kwa hiyo tutapitia sehemu kwa sehemu. Kwa hiyo kila mmoja anayetaka kuchangia awe makini kwa sehemu ambayo angependa kutoa mchango wake.

Sehemu ya 1

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipendekeza kuhusu neno *"Student Organisation"* litafsiriwe. Pamoja na kwamba kimsingi Mheshimiwa Waziri amekubaliana na hilo, lakini sioni kama amekubaliana katika hiyo tafsiri. Sijui kama aliipata vizuri au hakuipata. Maana yake katika *section* inayohusika ya kuweka hiyo *apex* ya wanafunzi amekubali apeleke kwenye Kanuni japo kuna mgogoro hapo baadaye. Lakini kwenye tafsiri sasa sioni kama amekubali kufanyia marekebisho.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuweza kuiweka kwenye tafsiri ingawa tumeiongeza katika Jedwali na tumekubali kwamba mabadiliko yawepo ambapo kutakuwa na *Apex Organisation* na kwa sababu kuna kifungu ambacho kinahusika na Vyama vya Wanafunzi ni kifungu nadhani cha 49, kwa hiyo tunaomba atuachie katika utekelezaji hiyo, tutaiweka tafsiri katika Kanuni zetu.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wadau walipendekeza kwamba *Student Organisation,* wacha ya kwangu ninayoongeza iwe *defined* huku. Kwa sababu Vyama vya Wanafunzi, sijui Rais wa Chuo na tunaowaita wadau ni vitu vya msingi huwezi kuviacha hivi hivi. Pale kwenye *University* kuna wengine wana Chama chao cha Wanyambo, Wahaya, Wasukuma kutoka Bariadi. Sasa hivi hatuvitaki huko vitakuwa na sehemu yake. Lakini *Student Organisation* si kitu cha kupuuza na kutokiweka kwenye tafsiri hii. Kwa hiyo mimi sioni kama kuna dhambi yoyote kwamba isiwe *defined* kwenye hii sehemu ambayo wame-*define* hizi sheria.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu niungane na Mheshimiwa Mtoa Hoja kwa maelezo aliyoyatoa. *Student Organisation* sio lazima uipatie tafsiri kama anavyosema yeye Mheshimiwa Mutungirehi. Katika orodha ya marekebisho tunaitambua katika eneo tunatafsiri kwamba itakuwepo *Student Organisation* ambayo itakuwa na maana kama inavyofafanuliwa katika kifungu cha 49 cha Muswada huu. Sasa lazima uende kwenye kifungu cha 49 ukapate mahudhui ambayo lazima yatatokana na upatikanaji wa chombo hicho. Kwa maana hiyo tafsiri ipo na sidhani kama tuna haja ya kulirudiarudia hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mutungirehi naona bado hajaridhika.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni kitu kidogo, kwa sababu tunapoku-*address* wewe, unajua taratibu za adhabu. Mimi sioni dhambi kwa sababu chombo cha wanafunzi, *Student's Organisation* ni chombo kikuu katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na amani, mahusiano na Uongozi, ni chombo cha Uongozi. Mimi sioni dhambi iliyopo kukataa kukiweka kwenye *definition* kama sheria ambavyo inatamka. Kwa sababu vinginevyo anavyosema yeye *Chancellor* ametajwa si angemwacha! Sijui *Academic Staff,* angeacha huku!

Mimi sioni dhambi ni nini, kama tumekosea mahali tuseme basi tutaweka. Lakini lazima tui-*define* ni nini! Kwa sababu nimeshawaeleza pale itafika mahali nyinyi mmezoea mambo ya kisiasa wataingiza humu kwamba sisi watu wa Chama fulani, *TLP*, Chama cha Wanafunzi wa *TLP* hapa tumeweka itakuwa fujo. Lazima tuweke hapa ni nini hasa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni tatizo kubwa sana kwamba kwa sababu *definition* tayari mwanzoni ilikuwepo lakini ikafanya *cross reference* kwa ile ibara ya 49. Tukiisoma ibara ya 49 katika vifungu vyake vyote inajitosheleza kabisa kueleza *StudentS Organisation* nayo ikitajwa hapa. Sio Vyama vya Ukabila, sio Vyama vya Kanda kwenye Chuo Kikuu, ni Vyama ambavyo vinatokana na Katiba iliyokubalika na *Council*.

Bado utawala wa Vyuo Vikuu tunaukasimu kwenye *Council*. Kwa hali hiyo hata *definition* tuiachie *Council*. Ndiyo nikasema kwenye Kanuni kwamba kama haitaonekana kwamba inaeleweka tutaweka vizuri lakini leo kwa haraka haraka hapa *definitions* ni masuala ya sheria na sheria ni maneno ambayo yako tasinifu ambayo lazima yawekwe kwa uhakika. Sasa ukiona kwamba kuharakisha sasa hivi tungezua mjadala mwingine hapa wa *semantic* ambao utatufikisha mbali sana. Naomba tu Mheshimiwa Mutungirehi kwamba utuelewe, hivyo tutalifanyia kazi na kwa sababu kifungu hicho 49 kinajitosheleza.

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 2

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Kuna jedwali la marekebisho yameletwa ambalo linaongelea hii *clause* ya 12 na nafikiri wamekosea wamesema *sub clause one. In fact* kwanza ni *sub clause two,* ni 12.2. Nafikiri hilo wameliona, lakini ni kosa la kawaida tu na walikuwa wanaongelea kwenye *paragraph (c)* ambayo ndiyo iliyokuwa inasema: *"The provision of central admission services Universities."* Wanaleta marekebisho kwamba wa-*substitute* lile neno na *facilitation*.

Mimi bado naona hilo neno pia lina maana ile ile kama hilo *provision*. Ku-*facilitate* na ku-*provide actually to me is the same thing* kwenye *environment* kama hii. Nafikiri kikubwa ni ule uelewa unaotokana na matamko haya kwamba ni kitu cha kawaida kabisa mtu akisoma hapa ataelewa hivyo kwamba udahili utafanywa *centrally*, kwamba watadahiliwa hapa kwenye Kamisheni halafu watapelekwa huko wanakokwenda lakini udahili utafanyika na hilo nafikiri ndiyo ilikuwa *concern* yangu mimi na Waheshimiwa Wabunge waliozungumza. Kwa hiyo lingeondoka kwa sababu sioni neno ambalo linaweza likaandikwa hapa lisimaanishe hivyo kwamba udahili *as long as* hili neno *central admission services* liko pale. Mimi nilikuwa nafikiria ni bora ikafutwa kabisa hii sehemu ili kuondoa utata.

*After all* kama dhamira ilikuwa ni kwa kiasi fulani ukiangalia ile (b) pale juu inasema *conditions for admission to different categories of Universities* hiyo nafikiri tayari iko *catered for.* Kwa sababu nafikiri anaongelea *conditions,* lakini sasa wamekwenda *further,* hapa wanaongelea ku-*centralize* ile *process.* Nafikiri hapa ndiyo panapoleta utata. Napendekeza iondolewe kabisa.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelewa hoja ya Mheshimiwa Mbunge. Lakini katika majibu yetu ni kwamba tunachofanya hapa siyo kudahili wanafunzi katika kituo kimoja. Kila Chuo kitadahili wanafunzi wake. Hapa ni vigezo *(criteria)* hizo kuzi-*motor* na kuziangalia ndiyo hasa msingi wa Muswada huu kuhakikisha kwamba kuna vigezo vya ubora wa elimu. Kama hautajua ubora wa wanafunzi wanaoingia katika Vyuo Vikuu, basi unavunja kabisa ule moyo wenyewe wa sheria hii.

Lengo siyo kwamba tuwadahili sisi. Vile vigezo vya kudahili walau chombo hiki kiweze kuweza kutawala na kwenda kuona. Sasa wanafunzi wasiingie tu holelaholela, bado Vyuo Vikuu vina nafasi kama alivyokuwa amejieleza Mheshimiwa Mbunge katika kuchangia kwake na sisi tumeheshimu sana mchango huo, nakubaliana naye kwamba Vyuo Vikuu viwe na uhuru wa kuweza kudahili wanafunzi kwa vigezo mbalimbali ambavyo haviko nje kabisa ya vigezo ambavyo vinakubalika. Kwa mfano, wanafunzi ambao wana sifa ambazo zinatosheleza na nyingine ambazo ni mbadala, Vyuo Vikuu vyenyewe viwe na uwezo huo, lakini visiwe tofauti mno ndiyo maana yake hapa.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nina *reservations* lakini baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kama anavyosema kwamba hapa anachoongelea ni *criteria* na mimi nilikuwa nafikiria ile (b) ina *cater for that.* Basi kama *interpretation* ndiyo hiyo mimi nakubali. Lakini nilikuwa nina wasiwasi kwamba ikisomwa nje ya watu tulioko huku ndani wanaweza wakaelewa visivyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hii nadhani haina haja ya kujibu, alikuwa anakubali tu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Pengine kabla hajasoma hii sehemu ya pili nitoe tu ufafanuzi wa jambo dogo. Wakati ule wa mjadala wakati anahoji Mheshimiwa Mutungirehi kuhoji vifungu niliruhusu muda mrefu wa majadiliano kwa sababu Serikali mpaka mchana huu imeleta *amendments.* Kwa hiyo, ndiyo maana nilitoa ile nafasi ili kujaribu kupata ufafanuzi zaidi. Namna nyingine ingebidi iletwe mapema. Lakini kwa sababu Serikali nayo imeleta yakwao humu humu, kwa hiyo, inawapa nafasi Waheshimiwa Wabunge kuhoji zaidi na zaidi kwa faida ya kuingia kwenye Hansard kupata fafanuzi mbalimbali. *(Makofi)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia katika sehemu hiyo na hususan katika kifungu cha 29 kuhusu *revocational of a charter.* Sasa wasiwasi wangu ilikuwa ni kwamba tunavyojaribu kupata uzoefu, kuna watu wanaanzisha Vyuo kwa madhumuni mbalimbali, anaweza kufika mahali Chuo kile anakitelekeza anakimbia halafu kama ilivyoelezwa hapo kwenye kipengele 29 (4) *where the charter is revoked under this section the Commission shall make arrangement for re-admitting of existing students in some other universities.* Sasa sheria hii haisemi na imetajwa huku ni vitu gani unaweza kupelekea ile hati yake iwe *re-advocated.* Sasa havisemi ni *penalty* gani anaipata, ni taratibu gani zitaendelea ili aweze kudhibitiwa. Kwa sababu vinginevyo nadhani uzoefu wa nchi hii umetuonyesha kwamba mtu anaweza kuanzisha kitu akishafaidi anakitupa pale kwa sababu ya udhaifu uliopo katika sheria. Sasa nilitaka kujua Mheshimiwa Waziri hilo amelifikiria au ameona si la msingi?

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mutungirehi kwamba yanayosemwa na kupendekezwa na Bunge hapa yote yanatiliwa maanani. Lakini kuna utaratibu vile vile wa kurekebisha kuweka hiyo adhabu, *drafting* hiyo. Kwa sasa hivi tumefikiria ile adhabu kwa kuanzia, kwa sababu tunaanza na sheria, ni safari ya wakati wote. Unapoweka *registration* katika Bunge siyo kwamba ndiyo mwisho wa dunia. Unaanza, inafanya kazi katika vitendo na itanyumbuka namna gani.

Tumeona kwamba kule kunyang'anywa usajili wa Chuo, kwa kuanzia ni adhabu tosha. Lakini tumetilia maanani vile vile kwamba inahitajika adhabu zaidi baadaye ambayo tutaifikiria kuiweka kwa kuiangalia kwa makini zaidi katika *drafting* ambayo muda unahitajika kui-*draft* vizuri zaidi. Lakini namwomba Mheshimiwa Mutungirehi kwa sasa adhabu hii ya kunyang'anywa ule usajili itosheleze kwa sasa.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu bahati nzuri ni *diplomatic*. Lakini tunachosema, kweli mtu aanzishe Chuo na Mheshimiwa Mwenyekiti unaelewa vitu vya binafsi kwa sababu sheria hii ya ku-*revoke* Ibara ya ku-*revoke* inahusu Chuo binafsi, kuna watu kwa mfano Shule ya Sekondari au Shule ya Chekechea anachukua karo Shilingi laki nane au laki saba na ni hela nyingi na mtu anaweza akaanzisha mradi kama huo kwamba sasa hapa nitawakamua. Akawakamua akakimbia. Halafu sasa sisi kwenye sheria tumenyamaza kimya tunaona ni kitu ambacho muda haupo na kadhalika.

Labda kama anasema tukasimu, tuwape madaraka waende wa-*draft* waweke hapo baadaye watatuonyesha hii tukubaliane. Lakini kuiacha hivi hivi nadhani si vizuri. Nadhani *experience* nimeitoa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *concern* ya Mheshimiwa Mutungirehi inaeleweka, hasa unapokuwa na haya matatizo ya *e.g ampler*. Lakini niseme hivi, kwa mfano alioutoa kwanza kifungu cha 58 cha Muswada huu kinaweka haya makosa ya jumla ambayo yametajwa na Muswada huu. Hilo hakuna tatizo. Lakini makosa mengine kama kukusanya ada, sheria nyingine za nchi zipo, huyo mhusika atashughulikiwa tu kama mhalifu mwingine. Mwizi wa fedha atafikishwa Mahakamani na ushahidi ukithibitika atafungwa.

Kwa hiyo, hilo wala lisimnyime usingizi katika eneo hili la Muswada. Hoja kubwa tunaanza na *revocation*, utaendelea na shughuli uliyokuwa umesajiliwa nayo. Lakini kama una matatizo mengine yatafuata sasa uamuzi huo ukiwa shughuli ya kuwa chuki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mutungirehi, wanakati anajibu Mheshimiwa *Attorney General,* alisema neno mimi sikulielewa ilibidi nimwulize, *ampler* sijui kama ulielewa? *(Kicheko)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetunga sheria hapa na mimi sitaki nionekane *I am amuses* kwa Wabunge. Tunachosema katika kila sheria tunaitunga tunasema anaye-*valuate* hii kitu tunampa adhabu hii. Sasa kwa mfano Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu anachokisema hapa hicho kifungu cha 58 hatujafika huko, nikusomee chenyewe kinachekesha. Anasema, naomba nisome kwa ruhusa yako. *"A person who commits an offence or an act decleared to be unlawful under the provisions of this Act for which no particular punishment has been provided for under any specific section is liable on conviction to a fine not exceeding 1,500,000/= shillings or to imprisonment for a period not exceeding six months or both such a fine and such imprisonment."*

Sasa huko hakuna adhabu yoyote na yeye akikwepa hapa, yaani analipa milioni moja na nusu mtu mhuni ameandikisha watu akawatupa hapo kwa sababu anajua Serikali itawachukua iwapeleke kwenye Vyuo vingine.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri anayoitoa Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na kifungu cha 58 ni *partly right* lakini nusu nyingine ni kwamba hiki kifungu cha 58 ni cha ziada huwezi ukafuta *penal code* kwa utaratibu huu, kwa hiyo itategemea sasa na mazingira mahususi ya tukio lenyewe. Nimesema mfano mzuri tu alioutoa ni hiyo kukusanya ada za wanafunzi halafu ukatoweka. Sasa hilo tunasema sheria zipo na zitaendelea kuwepo kuwashughulikia watu wenye matatizo ya namna hiyo.

Sasa hapa tunasema tu kwamba Muswada huu umetaja katika vifungu fulani fulani kwamba ukifanya hivi itakuwa ni kosa. Lakini kuna vifungu vingine havisemi katika eneo hilo kwamba ni nini kiwe. Kwa hiyo, tunasema iwapo litatokea jambo ambalo halitajiwi adhabu yake basi adhabu inatajwa katika ibara ya 58 ndiyo inatumika. Ni hiyo tu, nashukuru.

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Ibara ya 34

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 36
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 42

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 48
Ibara ya 49

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 50

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 51
Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 62

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima pamoja na marekebisho yake)*

**Jedwali 1**

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu. Nimetoa mapendekezo kwamba viongezwe vifungu katika hii *schedule* ya kwanza ambavyo vitaruhusu kuteuliwa Mwakilishi kutoka Baraza la Wawakilishi kuingia kwenye Tume. Niliacha makusudi nafasi mbili walizokuwa wamepewa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu ninajua tutakavyoanza kuteuana hapa sijui *Tanzania Private Sector Foundation* inawezakana *Director of High Education* akawa anatoka huku, akatoka *Tanzania Association Employers* wakajichagua wao kwa sababu hawana Kanuni kama za kwetu za Bungeni na mawasiliano nayaona hapa.

Lakini alichofanya Mheshimiwa Waziri, zile nafasi mbili Serikali ya Zanzibar ndiyo amezigawa, moja akaibakiza Serikali ya Zanzibar na moja akawapa Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi hoja yangu ni kwamba zile nafasi za Serikali ya Zanzibar zibaki na Baraza la Wawakilishi wapewe nyingine moja. Yale mengine sina ugomvi nayo.

**MWENYEKITI- MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Sijui kama *amendments* walizoleta mchana huu umeziangalia.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Ndiyo nimeziona. Anachosema yeye ni kwamba, *"Two members nominated for education Zanzibar* halafu akai - *break* (j) *one member representing the revolutionary government and one member representing the House of Representative of Zanzibar."* Sasa yeye amefanya labda kama tunaielewa vibaya, kwa sababu hoja yangu ni kwamba wale aliokuwa amewataja kwenye Muswada wa kwanza wabaki vile vile wachaguliwe na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini aongezeke mmoja kutoka Baraza la Wawakilishi. Labda kama naelewa vibaya.

**MWENYEKITI:** *Attorney General* ungependa kutoa ufafanuzi au Mheshimiwa Waziri! Watu wanasema *Attorney General* lakini Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeongeza wengine tena wadau wakubwa zaidi ambao tuliwasahau hili hakuna mtu aliyezungumza hapa. Kama nilivyosema tulipotafakari tukaona tumesahau wadau wengine. Wanafunzi Vyuo Vikuu na malengo yake makubwa ni wanafunzi na wakati wote huwa tunawasahau. Tukaona kwamba tutoe hizo nafasi mbili tuzigawe kama tulivyozigawa na kuongeza wanafunzi ambao mmoja atatoka Zanzibar na mwingine anatoka Union. Sijui kama Mheshimiwa Mbunge, asingependa wanafunzi wakawakilishwa katika kitu kama hiki.

Tungependa vile vile Baraza hili au *schedule* hii wasiwe watu wengi mno ikawa sasa inaleta gharama na usumbufu mkubwa katika kukutana. Haya yalikuwa mantiki ya mabadiliko haya.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo anayoisema ya wanafunzi nilipendekeza mimi na nimempongeza kwa kuwa *diplomatic* kwamba ameiweka imo humu. Sasa mimi ninayosema ni ile ya Zanzibar, ninamwomba kabisa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awaachie nafasi mbili pale. Mtu mmoja hawezi kuongeza bajeti hii mpaka Serikali ikafa. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia nzuri ya Mheshimiwa Mutungirehi, naomba aziachie Serikali mbili hizi zifanye mambo haya na kama nilivyoeleza jana katika Muswada mwingine na nikianzia na hiyo hoja yake ya uwakilishi kupitia Baraza la Wawakilishi unaona katika (f) ni Mjumbe mmoja atakayetokana na Bunge kama Taasisi na hivyo hivyo tunapendekeza katika Baraza la Wawakilishi kupitia hiyo *additional amendments.*

Pili, kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi, ndiyo inasema ipewe hiyo nafasi moja. Katika chombo hiki, hoja siyo wingi wa mkusanyiko wa watu unaowapeleka pale, hoja ni ule uwezo wa watu unaowapeleka pale, kuweza kujenga hoja na kusaidia katika majadiliano ya muhimu ya chombo hiki. Kwa hiyo, Serikali bado inashawishi Kamati yako ikubali marekebisho ya Serikali kama yalivyoletwa katika hii *additional schedule of amendments.*

*(Jedwali lililotajwa hapo lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko)*

Jedwali la 2
Jedwali la 3

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia, nilisema Jedwali hili katika kifungu cha pili, *the following act are hereby repealed* kwamba iongeze kile ambacho kinahusu *The State University of Zanzibar Act Na. 8 of 1999* na nilisema kwamba katiba ilivunjwa. Sasa nashukuru kwamba Waziri ameli-*handle* kwa ustaarabu wa hali ya juu, kwamba hakutaka nifute kauli na haina mjadala tena waliovunja wanajua walivunja kwa sababu hii ni Katiba ya Jamhuri, inasema *Tanzania is one State* na hapa ni ile sheria iliyoanzisha kile kinachoitwa *an Act to establish the State University of Zanzibar.* Ni vizuri kule *State of Coroma* sawa kwa sababu *They are United State.*

Lakini hapa ni *Republic* ambayo inajumuisha sehemu zile mbili. Sasa sheria ilikuwa imevunjwa. Ninachoomba, kwa sababu Waziri ameshakiri na sioni haja ya kuendeleza mjadala kwamba tunaiweka hapa siyo kusema itakuwa *redundant,* ife na kama wanataka kwa sababu kwa mujibu wa sheria hii inaruhusu, sasa hata Mkoa wa Mbeya kuanzisha Chuo chake, inaruhusu hasa Manispaa ya watu kuanzisha Chuo chake lakini kwa utaratibu fulani. Sasa kwa sababu hii ni *Act* ya Baraza la Wawakilishi kule na

ilikuwa imevunja utaratibu na wao wangeandika *Government of Zanzibar University,* mimi nisingepiga kelele kwa mujibu wa haya. Lakini kusema *"state"* na kutunga hapa wakati wakijua kulikuwa na sheria ile ambayo inasema katika orodha ya mambo haya yalikuwa ya Muungano walivunja, sasa mimi nawasamehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachoomba tuweke hapa ni kwamba, hiyo nayo inakuwa *repealed* kwa sababu mtu ambaye alikaidi katiba akaivunja hata hii ataikataa. Nasema hivyo kwa sababu tutafika mahali hiki chombo kina *accreditation council* kitataka ku-*apply,* wataweza kusema kama tulivunja Katiba, hakuna aliyetugusa; hebu toka hapo hiyo sheria yenu hatuitambui sisi tunaendelea huku.

Tusichukulie mambo haya hivi hivi. Sasa naomba kusikia msimamo unasemaje, kwamba wanawaachia waendelee kuvunja au tunai - *repeal* hapa hapa kama wanalalamika waende Mahakamani.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ni nyepesi sana. Bunge lako Tukufu linashughulika na sheria ambazo zimetungwa na Bunge lako Tukufu kwa mambo ambayo ni ya Muungano na mambo ambayo siyo ya Muungano, lakini yanahusu Tanzania Bara. Sheria ya *State University of Zanzibar* ni sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi. Pamoja na maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Mutungirehi mimi nisingependa nifike huko, lakini nasema kwa hoja iliyo mbele yetu hapa hatuwezi kutumia Muswada huu kufuta sheria ambayo iko nje ya mamlaka yako. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitu nadhani kinaudhi kama watu wazima kutokukubaliana kwamba huu utaratibu hapa umekiukwa. Sasa kama tukikubaliana, kuna mtu anamnyonga mwingine? Sasa wewe ukisema ilitungwa kule, kwanza mimi nakwambia walitunga kwa kuvunja katiba, hujani-*disapprove* kwamba *you are shouting* toka walichofanya ni wao wana *state* hilo la kwanza.

Lakini la pili, ninachosema, kuna *indication* kwamba watu hawa walishavunja, sasa wanaweza wakakaidi hii; sasa tutawafanyaje kwa mfano kama hatuwezi kutaja hapa, maana yake unaniambia itakwenda *automatically.* Ilikuwepo *automatically! This is constitution, i*nasema na nimekusomea. Sasa endapo watakaidi kuna Kikao kingine cha mtu kuja kuwashtaki? Tunachoogopa ni nini? Kwa sababu nimeshasema kwamba kama ni hivyo kuna hii hapa wao waende wakarekebishe watakuwa ni *Government of Zanzibar* ambayo iko kwenye Katiba *Government* ile inatambuliwa halafu walete pale, lakini tukubaliane hapa kwamba tunafanya hivyo na yaishie hapa, hakuna atakayekwenda kushitakiwa ajibu kwa nini alivunja Katiba ya nchi.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Mutungirehi ungependa hapa sisi Bunge hili liseme sheria iliyotungwa Zanzibar imefutwa na Bunge hili?

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inasema zile *Act* ambazo zilikuwa zimetungwa na kuna mahali inataja wale wengine ambao walikuwa wana *private universities* watafuata masharti haya. Wale wa *Private*

*Universities* hawakuwa na Sheria za Bunge. Lakini imetaja kwamba itabidi wafuate masharti ya sheria hii. Sasa hii sheria ambayo ilikuwepo japo kinyemela hatujataja hapa kwamba ifutwe. Sasa wasiwasi wangu wa kutaka tuweke kwamba tunaifuta hapa kwenye *schedule of amendment* inayosema, nadhani kwenye Muswada ni ukurasa wa 59 amezitaja pale. Sasa tunaiorodhesha pale kwamba itafutwa. Sasa hata kama mnakataa lakini katiba ilivunjwa.

**MWENYEKITI:** Mimi sijui tufanyeje kwa sababu sheria hii anazozisema hapa ni zile ambazo zimetungwa na Bunge hili, hizi zilizoorodheshwa hapa. Sasa ugomvi wako na Serikali ni kwamba unataka watamke kwamba sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi imekuwa *repealed* kwa kufuata sheria hii tunayotunga leo, *is that what you want to say?* Hebu *Attorney General* naomba ufafanue hilo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa taratibu zetu tunakwenda kwa hoja, hoja yake hiyo, haiko mbele ya Bunge lako na wala kwenye Kamati. Lakini kwa maneno yake mwenyewe kama tungelikuwa tunafika katika hoja hiyo, kwamba anasema ni batili kwa sababu inakinzana na Katiba, basi haipo hoja ya kushughulikia kwa sababu kitu ambacho kinapingana na Katiba ni batili. Kwa hiyo, mimi sioni tatizo. *(Makofi)*

*(Majedwali yalilotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali 4

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Hebu tuone kwanza. Tumemaliza vifungu na majedwali yote. Hili unalitaka ni la vifungu huku ndani au lingine ili nirudi tujadili?

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hilo nilitaka unipatie mwongozo wako. Wakati tunazungumzia sehemu ya pili mimi ndiyo nilikuwa nazungumza, nilipitiwa tulipofika sehemu ya tatu. Sasa nilikuwa nataka nieleze, kuna mabadiliko ambayo hayabadilishi maana isipokuwa yanabadilisha uzani. Nafikiri ni muhimu sana kama unaweza ukanisikiliza halafu ukaamua kama yakubaliwe au yakataliwe. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI - MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Mheshimiwa Mbunge, nadhani unajua na ndiyo maana umesikia watu wanapiga kelele ni nje ya utaratibu kabisa. Tulishapita, kwa hiyo, tumepita. Ni kuwa makini tu katika sheria zijazo katika kuangalia vipi tunakwenda. Kwa hiyo, hatuwezi kurudi nyuma. *(Makofi)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Vyuo Vikuu wa Mwaka 2005 *(The Universities Bill, 2005)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imefikiria Muswada wa Sheria wa Vyuo Vikuu wa mwaka 2005 pamoja na marekebisho yake yaliyofanywa. Hivyo, sasa naomba kwamba Muswada huo kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, shughuli ambazo zilikusudiwa zishughulikiwe leo, tumemaliza tumeishia hapo. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 14 Aprili, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*